# Nipashe

Jumanne Oktoba 4, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581088


www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



SUPA JACKPOT
TZS.1,037,361,877
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#

**Ang'atwa** ulimi na mpenzi wake wakiwa faragha

UKURASA 24



**ANCELOTTI AKATAA KUMLAUMU BENZEMA**

UKURASA 30

# Samia aonya mambo matatu kwa mawaziri

• **Anena** kupitia hotuba ya dakika nne... *Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akimwapisha Angellah Kairuki kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika hafla fupi iliyofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## Wauana kwa fimbo kugombea mwanamke

UKURASA 4



## Ujenzi Daraja la Jangwani waiva

UKURASA 9

**MICHEZO** **TFF YAVUNA MIL. 376/- MAPRO SIMBA, YANGA** UK.32 **KABWELA** UK.7

# Samia aonya mambo matatu kwa mawaziri

**Na Beatrice Moses**

RAIS Samia Suluhu Hassan ametoa angalizo kwa mambo matatu kwa mawaziri wakati wa utekelezaji wa majukumu yao, ikiwa ni muda mfupi baada ya kufanya mabadiliko machache kwenye Baraza la Mawaziri.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Nchi huyo, mambo hayo ni utunzaji siri, kutetea Katiba na kutambua mipaka yao ya mamlaka.

Alitoa angalizo hilo jana Ikulu jijini Dar es Salaam wakati wa viapo vya wateule wapya, baada ya kufanya mabadiliko madogo ya baraza lake la mawaziri kwa kuwahamisha wawili, kumwondowa mmoja na kumrejesha Angellah Kairuki bungeni kisha kumteua kuwa waziri.



Juzi usiku Rais Samia alimteua Angellah kuwa mbunge na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), huku akimwondoa Balozi Liberata Mulamula aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Rais Samia pia alimwapisha Dk. Stergomena Tax aliyechukua nafasi ya Balozi Mulamula pamoja na Innocent Bashungwa aliyekuwa Waziri wa TAMISEMI alimhamishia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuchukua nafasi ya Dk. Tax.

Akizungumza baada ya kuwaapisha viongozi hao, Rais Samia alitumia muda wa dakika nne kufikisha ujumbe wenye angalizo kwa mawaziri wake, akiwataka waishi katika viapo vyao kwa kulinda Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Rais alisema: "Katika viapo vyetu hapa tunaapa kuilinda na kuitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni dhana yangu kwamba waheshimiwa mnapoapa hapa inakuwa ni kweli. Muungano wenye pande mbili na mtatumika sehemu zote, sawa kwa jinsi Katiba ilivyogawa majukumu.

"La pili, kujua mipaka, kwamba nchi hii ina mamlaka na mamlaka uliyowekewa ina ukomo wake. Unapotaka kuvuka ni lazima upate rukhsa ya mamlaka ya juu, sasa mjue mipaka yenu ya kazi kwenda juu na kwenda chini.

"La tatu ni usiri, siri iwe imesemwa katika Baraza la Mapinduzi au umeitwa ukaelezwa hiyo ni siri. Na unapotaka kuisema au kuifanyia kazi, ujue jinsi ya kuitumia hiyo siri kufanya kazi.

"Linaloamuliwa na serikali, wewe waziri, ni lako na unatakiwa ulibebe na ukalifanyie kazi kwa misingi ile uliyoelekezwa. Huwezi kusema nimeelekezwa hivi, mimi sikutaka hivi lakini imebidi nifanye hivi kwa sababu nimeelekezwa. Huwezi kujitoa!"

Hafla hiyo ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiwamo wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama, viongozi wa kisiasa na dini.



Mhariri Mtendaji wa Gazeti la The Guardian, Wallace Maugo, akizungumza na wageni kutoka Chama cha ACT-Wazalendo walipotembelea ofisi za Kampuni ya The Guardian inayochapisha magazeti ya Nipashe na The Guardian, Mikocheni, Dar es Salaam jana. Kushoto ni Waziri Mkuu Kivuli wa chama hicho, Doroth Semu. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Waomba wapelekwe jela Keko

**Na Grace Gurisha**

WASHTAKIWA wawili wanaotuhumiwa kukutwa na vipande tisa vya meno ya ndovu yenye thamani ya dola za Marekani 30,000, wameiomba Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu iwapangie Gereza la Keko kwa kuwa ni pazuri na pana usafi.

Washtakiwa hao ni Hassan Sangari (22), mkazi wa Kingula mkoani Dodoma na Nassoro Mbuguni, mkazi wa Kibasila, Pwani ambao pia wameiomba mahakama wapewe vitu vyao vilivyopotea katika Kituo Kikuu cha Polisi mkoani Dar es Salaam.

Sangari na Mbuguni walidai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Huruma Shaidi wa mahakama hiyo baada ya kusomewa shtaka moja la kukutwa na nyara za serikali na Wakili wa Serikali Faraja Ngukah.

Baada ya Ngukah kumaliza kuwasomea shtaka lao, washtakiwa walinyoosha vidole na kumwomba Hakimu Shaidi kuwapangia mahabusu ya Gereza la Keko kwa kuwa ni pazuri na pana usafi wa hali ya juu, pia wameshapata marafiki ambao wanawasaidia sabuni na vitu vingine.

Hata hivyo, Hakimu Shaidi aliwaeleza kwamba hahusiki na masuala ya kuwapangia gereza na kuna kiongozi anayehusika. Kuhusu vitu vyao walivyoviacha kwenye gereza hilo, watakapokwenda watapelekwa.

Washtakiwa hao pia hawakutaka kusomewa maelezo ya awali kwa madai kwamba wanaumwa, mshtakiwa wa kwanza akidai walikuwa gerezani kwa kipindi cha miaka mitatu na ana dozi ya kifua hivyo hawezi kuendelea na kesi hiyo.

Kutokana na hali hiyo, Hakimu Shaidi aliahirisha kesi hiyo hadi Oktoba 18, 2022 kwa ajili ya usikilizwaji. Ilidaiwa kuwa Juni 9, 2018, eneo la Kimara Stopover, washtakiwa walikutwa na vipande tisa vya meno ya ndovu vyenye thamani ya dola za Marekani 30,000 sawa na Sh. milioni 66.72 bila kuwa na kibali cha Mkurugenzi wa Wanyamapori.

# IGP aingilia kati sakata askari aliyekatwa panga

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

MKUU wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Camilius Wambura ameingilia kati sakata la askari polisi wa wilayani Siha mkoani Kilimanjaro, Koplo Wilfred Kavishe aliyejeruhiwa kwa kukatwa panga kichwani na mtuhumiwa wa mauaji.

IGP Wambura amemtuma Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), Ramadhan Kingai, kuongoza timu ya wataalamu kwenda kuchunguza tukio hilo.

Koplo Kavishe alijeruhiwa kwa kitu chenye ncha kali na kushonwa nyuzi 12 kichwani, alipokutana na mkasa huo usiku wa Septemba 27, mwaka huu, wakati wa purukushani za kumkamata Pancras Shirima, mkazi wa Kijiji cha Naibili.

Taarifa iliyotolewa Oktoba 2, mwaka huu na Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, David Misime, inabainisha kuwa DCI Kingai atafanya uchunguzi wa kilichotokea na kuwahoji waliokuwapo eneo la tukio.

Sehemu ya taarifa hiyo inaeleza: "Mkuu wa Jeshi la Polisi Tanzania, IGP Camilius Wambura tayari amemtuma DCI Kingai kuongoza timu ya wataalamu kwenda kuchunguza tukio hilo.

"Koplo Wilfred alijeruhiwa vibaya na kitu chenye ncha kali kichwani na kulazwa hospitalini, kushonwa nyuzi 12 wakati walipokwenda katika nyumba hiyo kumkamata mtuhumiwa aitwaye Pancras Vernard Shirima aliyekuwa akituhumiwa kwa kosa la mauaji."

Shirima ni miongoni mwa watu wanaotuhumiwa kwa mauaji yaliyotokea Kijiji cha Naibili hivi karibuni.

Inaelezwa kuwa baadhi ya wananchi wa kijiji hicho walimshambulia kwa mapanga mtu aitwaye Serafini Mrama na kufariki dunia, wakimtuhumu kumkata ng'ombe wa jirani yake mguu wa nyuma na kuondoka nao kwa ajili ya kitoweo.

Juzi Nipashe lilichapisha habari kuhusu mke wa mtuhumiwa huyo, Silvia Lyimo, kugoma kuhama na watoto wake kwenye nyumba yake inayodaiwa kulipuliwa kwa bomu wakati wa purukushani za kutaka kumkamata mumewe, Pancras Shirima anayetuhumiwa kwa mauaji.

Mwanamke huyo alisema hataondoka katika nyumba hiyo iliyoharibiwa hadi hapo atakapojua hatima yake na familia yake kwa kuwa polisi wameharibu nyumba yake na samani za ndani.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji hicho, Melikiao Patrick, alinukuliwa akisimulia mkasa huo akisema: "Nilipigiwa simu na polisi muda wa saa mbili usiku kwamba wanakuja kijijini.

"Walipofika walisema kuna watu kadhaa wanawatafuta kwa tuhuma za mauaji na wakatutaka kwenda kwa Pancras Shirima. Tulipofika tuligonga mlango lakini mtuhumiwa aligoma kufungua mlango, ndipo askari huyo aliposukuma mlango na kujikuta akikatwa na kitu chenye ncha kali kichwani na damu nyingi kuvuja.

"Baada ya kuona damu, mimi nilikimbilia kwenye gari la polisi na baada ya muda nikaona moshi ukifuka kwenye nyumba hiyo. Wakati wa purukushani hizo mtuhumiwa alifanikiwa kukimbia na kutokomea kusikojulikana."

## HABARI KITAIFA



Ofisa Mwandamizi Huduma kwa Wateja wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma ya Nishati na Maji (EWURA), Getrude Mbilingi, akizumgumza na wateja waliokwenda kupata huduma kwenye ofisi za kanda Kinondoni, jijini Dar es Salaam jana, ikiwa ni wiki ya huduma kwa mteja. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Serikali yaweka nguvu kudhibiti ebola mpakani

**Na Mary Geofrey,** BUKOBA

SERIKALI imechukua hatua za kudhibiti watu wanaoingia na kutoka nchini kwa kuwapima kama wana viashiria vya tishio la ugonjwa wa ebola katika mpaka wa Mtukula mkoani Kagera.

Mganga wa Halmashauri ya Misenyi, Dk. Daniel Chochole, alibainisha hayo jana wilayani Bukoba mkoani Kagera alipozungumza kwenye mafunzo ya elekezi yanayotolewa na Wizara ya Afya kwa madaktari na watoa huduma za afya wa halmashauri nane za mkoa huo.

Lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wa namna ya kudhibiti, kubaini na kuripoti matukio ya tishio la mlipuko wa ugonjwa wa ebola.

Dk. Chochole alisema wameanza kuchukua vipimo vya watu wanaoingia na kutoka mipakani katika Halmashauri ya Misenyi iliyopakana na Uganda ili kuangalia kama wana viashiria vya ugonjwa huu ili kudhibiti usiingie nchini.

"Tumeanza kufanya matayarisho endapo katika halmashauri yetu ya Misenyi tutapata mgonjwa mwenye viashiria vya ebola tuwe tayari kumhudumia.

"Hadi sasa hakuna mtu anayehisiwa kuwa na ebola, hivyo kazi kubwa wanayoifanya ni kutoa elimu ya namna ya kujikinga na maambukizi," alisema Dk. Chochole.

Pia alisema wameweka gari la kubebea wagonjwa ili ikitokea amebainika mwenye dalili awahishwe katika hospitali iliyoandaliwa kuwahudumia wagonjwa wa aina hiyo.

Awali Mkurugenzi wa Huduma za Kinga wa Wizara ya Afya, Beatrice Mutayoba, akifungua mafunzo hayo ya siku saba, aliwataka wataalamu hao kuimarisha ufuatiliaji na kutoa taarifa kwenye maeneo yao kuhusu viashiria vya mlipuko wa ugonjwa huo kwenye maeneo yao.

Alisema mafunzo hayo yatawasaidia kutoa elimu kwenye vituo vya afya, ngazi ya jamii wakiwamo watendaji, viongozi wa kata na vijiji na madereva wa bodaboda na kuziingiza kwenye mfumo.

"Bodaboda ni wasafirishaji wa abiria, wanamtoa sehemu moja kwenda nyingine hivyo ni kundi muhimu ambalo litasaidia kufichua taarifa za watu watakaohisiwa kuwa na ebola, hata nchini Uganda ndiyo walisaidia kuwafichua wagonjwa wa ebola kwa sababu walishapewa elimu," alisema Dk. Beatrice.

Alisema pia watagawa simu janja kwa watumishi wa afya 90 ngazi ya jamii kwa ajili ya kuzitumia kutoa taarifa za viashiria vya ugonjwa huo pamoja na kuingiza taarifa hizo kwenye mfumo maalum wa taarifa wa wizara ya afya ili kuzihifadhi.

Alitaja dalili ambazo wataalamu hao wanatakiwa kujifunza ni homa kali, maumivu ya viungo na dalili nyingine za homa na kwamba zile za kutoka damu puani na maeneo mengine ya mwili ni za mwisho.

"Wagonjwa 35 waliogundulika Uganda walikuwa na homa kali na dalili nyingine zote ni za homa ya kawaida, hivyo watumishi wa afya mnatakiwa kujifunza dalili hizi na wenye hizi dalili waripotiwe haraka kwenye vituo vya afya," aliagiza Dk. Beatrice.

Aliwataka wananchi kuepuka misongamano, kutoshikana mikono, kunawa mikono na sabuni na maji tiririka mara kwa mara, kutoingiliana na wanyamapori, kutokumbatiana, kutoshika matapitishi na maji maji yoyote ya mwili ili kuepuka kupata maambukizi.

Kaimu Mkurugenzi wa Maabara Kuu ya Taifa, Menadi Beyanga, alisema mbali na kufunga mtambo wa kupima ebola katika Hospitali ya Kabyaire, wamefunga mashine nyingine za kupima magonjwa mbalimbali ili mgonjwa atakapofikishwa kituoni huko apate huduma za vipimo vingine na matibabu.

Alisema lengo ni kutoa huduma muhimu za vipimo kwa watu wanaohisiwa kuwa na ebola ili kuwasaidia wataalamu kutoa huduma za matibabu.


Chama cha Waendesha Shughuli za Anga Tanzania

**Chama cha Waendesha Shughuli za Anga Tanzania**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI/UMMA**

Mnamo tarehe 14 Septemba 2022, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA) alitoa notisi/agizo ambalo liliipa kampuni binasfsi ya Dubai - DNATA Zanzibar Aviation Services Limited, mkataba wa usimamizi pekee wa kuendesha jengo jipya la Terminal III lililojengwa hivi karibuni katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume Zanzibar (AAKIA).

Kulingana na notisi hiyo, DNATA itakuwa mtoa huduma wa pekee wa utunzaji ardhini na huduma za Marhaba Lounge. Kuanzia tarehe 01 Desemba 2022, watoa huduma wengine watazuiwa kufanya kazi (au kutoa huduma) kwenye Terminal III ya AAKIA.

Jumiya ya Sekta Binafsi ambayo hutumika kama sauti wakilishi kwa wadau na watendaji wote kwenye tasnia ya kutoa huduma ya anga ndani ya Tanzania ('TAOA/ Jumuiya'), inatambua kuwa DNATA imepewa kandarasi hiyo bila uwazi wa zabuni hiyo kuruhusu ushiriki wa washindani wengine katika manunuzi ya huduma hizo.

Jumuiya inaiona notisi hiyo ni ukiukwaji wa kanuni na taratibu za manunuzi ya zabuni na kanuni za usafiri wa anga. Miongoni mwa kanuni zilizovyunjwa ni pamoja na kanuni ya 20 ya Kanuni za Usafiri wa Anga kwa Wapakia na Washusha Mizigo kwenye Ndege za Mwaka 2012, zinazoelekeza tarabibu za kumchagua mtoa hududma kuwa za uwazi bila upendeleo na zenye kuendana na viwango vya ushindani vya kimataifa na zenye kufuata kanuni na sheria za zabuni za umma

Kwa mjibu wa agizo la ZAA, kuanzia tarehe 1 Desemba 2022, huduma katika terminal III ya AAKIA zitatolewa na DNATA pekee na mashirika ya ndege yatalazimika kutumia mtoa huduma mmoja tu. Hii ni kinyume na uamuzi wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) Namba 01 ya mwaka 2022 inayokataza pamoja na mambo mengine ukiritimba na mgawanyo wa vituo vya viwanja vya ndege. Agizo hilo litafifisha ushindani wa kibisahara na hivyo kutowalinda watumiaji wa huduma ambao sheria inakusudia kuwalinda.

Kwa kuwapa kandarasi DNATA bila kuwepo mchakato wa zabuni, ZAA sio tu kwamba inaweka mfano mbaya kwa sekta ya usafiri wa anga bali pia kutia doa kubwa katika jitihada za kuvutia wawekezaji wa kimataifa. Hii inaenda kinyume na mienendo bora ya biashara ya kimataifa katika huduma za anga. Mwenendo huo pia utaathiri imani ya wawekezaji kwa nchi yetu.

Ikumbwe ni hivi karibuni tu, TCAA iliipatia ZAA kibali cha kuwa na watoa huduma watatu pale AAKIA kutokana na ongezeko la biashara. Kwa hivyo, notisi ya ZAA inaonekana si tu kwamba inakiuka moja kwa moja maelekezo iliyopokea kutoka TCAA bali pia sheria za ushindani na inakaribisha ukiritimba.

Juimuiya inatambua TCAA ambayo imeanzishwa chini ya kifungu cha 20 cha Sheria ya Usafiri wa Anga, ina jukumu la kukuza ushindani mzuri, kusimamia utekelezaji wa Sheria za Usafiri wa Anga na kuwezesha utatuzi wa malalamiko na migogoro.

Hivyo basi, Jumuiya inaiomba TCAA kuingilia kati suala hili na kuiamuru ZAA kufikiria tena agizo lake kutokana na athari kubwa itakayotokea kwa waendeshaji wa mashirika ya ndege ndani na nje ya nchi, wahudumu wa viwanja vya ndege na watumiaji wa viwanja vya ndege kwa ujumla.

**IMETOLEWA NA USIMAMIZI**
**4.10.2022**

217074802

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
TANZANIA RURAL AND URBAN ROADS AGENCY (TARURA)

TANZANIA RURAL AND URBAN ROADS AGENCY
TARURA
Improved Roads For Sustainable Development

P.O. BOX 11042,
**DODOMA.**

## REQUEST FOR EXPRESSION OF INTEREST (EOI)
## (CONSULTING SERVICES – FIRM SELECTION)

| | |
|---|---|
| **Country:** | **Tanzania** |
| **Name of Project:** | **Tanzania Roads to Inclusion and Socioeconomic (RISE) Project** |
| **Credit No.:** | **IDA-6867 – TZ** |
| **Assignment Title:** | Provision of Consultancy Services for Feasibility Study, Economic Assessment, Detailed Engineering Design, Preparation of Tender Documents and Construction Supervision for upgrading of 58km Roads in Mbogwe District Geita Region into the appropriate sealing Standard. |
| **Reference No.** | **AE.092/WB-RISE-P164920/276630/2022/23/C/02** |

This request for expression of interest follows the General Procurement Notice for this Project that appeared in the United Nations Development Business (UNDB) No. WB-P890351-12/21 of 14th December 2021.

The Government of the United Republic of Tanzania through Tanzania Rural and Urban Roads Agency (TARURA) has received a credit from the International Development Association (IDA) towards the cost of Roads to Inclusion and Social Economic Opportunities (RISE). It is intended that part of the proceeds of the credit will be used to cover eligible payments under the contracts for Consultancy services.

The consulting services ("the Services") intent is to carry out Feasibility Study, Economic assessment, Detailed Engineering Design, Preparation of the Bidding Documents and Construction Supervision for Masumbwe - Iponya – Nyashimba (20km), Lulembela - Kiseke - Isebya (17.00km) and Mkweni - Nhomolwa - Nyanhwiga (21) in Mbogwe District.

The Feasibility study shall determine the technical and economic feasibility of upgrading the existing gravel/earth road(s) to appropriate sealing standard. Depending on the results of the feasibility study, the Consultant shall undertake detailed engineering design, and preparation of tender documents for International Competitive Bidding (ICB) or National Competitive Bidding (NCB) according to the latest World Bank Standard Procurement Document (SPDs). The construction supervision will involve direct on-site supervision of the construction works and supervision during the Defect's Liability Period (DLP).
For Phase 1 the assignment will include carrying out Feasibility Study, Economic assessment, Detailed Engineering Design and Preparation of the Tender Documents and confidential Cost Estimates for 58km roads in Mbogwe District Geita Region. The work is expected to be completed within eight (8) months from contract effective date.

For Phase 2 the assignment will cover direct on-site supervision of the construction works and supervision during the Defect's Liability Period (DLP) of all roads designed in Phase I. This Phase is expected to be completed within Eighteen (18) months after commencement of Construction contract followed by twelve (12) months of DLP.

The detailed Terms of Reference (TOR) for the assignment can be found at at TARURA's website **www.tarura.go.tz** or upon request in the following email address **pmurise@tarura.go.tz**. All requests for clarification should be sent through office email **pmurise@tarura.go.tz** and the Client will respond to the requested clarifications.

The Chief Executive TARURA, now invites eligible consulting firms ("Consultants") to indicate their interest in providing the above services. Interested consultant should provide information demonstrating that they have the required qualifications and relevant experience to perform the services. The short-listing criteria are: -

A. Core business and 10 years in business

B. Relevant similar experience, which should specifically include the below:

   a) Experience of at least two (2) similar assignments completed in the past 10 years. Information to be provided should include name of assignment, name and full contact address of the client, contract value (in equivalent US dollars) and period (dates) of execution of assignment and the role played in the assignment (Lead or JV partner)

   b) Demonstration of experience of work in similar conditions in developing countries.

C. Technical and Managerial Capability of the firm (Provide only the structure of the organization, general qualifications and number of key staff). Do not provide CV of the staff. Experts will not be evaluated at the shortlisting stage).

The attention of interested Consultants is drawn to Section III, paragraphs, 3.14, 3.16, and 3.17 of the World Bank's "Procurement Regulations for IPF Borrowers" Fourth Edition, November 2020 ("Procurement Regulations"), setting forth the World Bank's policy on conflict of interest.

Consultants may associate with other Firms to enhance their qualifications but should indicate clearly whether the association is in the form of a Joint venture and/or a Sub-Consultancy. In the case of a joint venture, all the partners in the joint venture shall be jointly and severally liable for the entire contract, if selected. Therefore, each member of JV shall independently meet the requirements of the evaluation criteria. The experience, technical & managerial capability of the Sub-Consultant shall not be evaluated to enhance the qualification of the Lead Firm or JV.

A Consultant will be selected in accordance with the ***Quality and Cost Based Selection (QCBS) method*** set out in the Procurement Regulations.

Further information can be obtained at the address below during office hours from 08.00 to 17.00 hours Local time Monday to Friday except public holidays.

Expressions of interest must be delivered in a written form to the address below in person, or by e-mail **pmurise@tarura.go.tz** by **21st October, 2022 14:30 Hours East African Time.** The firms that will submit their EOI via e-mail must get confirmation of the receipt of their documents. In case the firm does not receive acknowledgement within two days of after sending the documents via email they should call +255759348494/+255622759393 or +255745810140 for follow-up.

***The address referred above is:***
***The Secretary, TARURA HQ Tender Board***
***Street Address: Mtaa wa Kazi 41207 Mtumba,***
***Building: TARURA House***
***Address: P.O. Box 11042, Dodoma, Tanzania.***
***Floor/ Room no: Ground Floor room no. 10, PMU Office***
***City/Town: Mtumba Government City Area***
***Country: United Republic of Tanzania***
***Electronic mail address: pmurise@tarura.go.tz***

**CHIEF EXECUTIVE OFFICER**
**TANZANIA RURAL AND URBAN ROADS AGENCY (TARURA)**

21705102

# Wanaume wauana wakigombea mpenzi

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

MUSSA Bakari (21) na Ibrahim Shabani (28), wote wakazi wa Kijiji cha Mkangaula, Kata ya Namalenga wilayani Masasi mkoani Mtwara, wameuana baada ya kupigana kwa kutumia magongo wakigombea mwanamke aliyetambulika kwa jina la Hadija Msamati, kila mmoja akidai ni mpenzi wake.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Nicomedus Katembo, alisema lilitokea mwishoni mwa wiki majira ya saa 12 jioni katika Kijiji cha Mkangaula wilayani Masasi mkoani hapo.

Kamanda Katembo alisema vijana hao waliuana baada ya kugombea mwanamke ambaye kila mmoja alidai ni mpenzi wake, hivyo walipofumaniana walianzisha ugomvi na kupigana kwa kutumia magongo.

Alisema kuwa baada ya ugomvi wao, wote wawili walipigana na kusababisha kuuana, vifo vyao vikisababisha taharuki kwa jamii kwa kuwa tukio hilo siyo la kawaida katika maeneo hayo.

Alisema baada ya kufumaniana, waliamua kila mmoja kuchukua gongo na kuanza kumshambulia mwenzake huku kila mmoja akifanikiwa kumpiga mwenzake hadi alipofika hatua ya wote kuanguka chini na baadaye kupoteza maisha.

"Ni kweli kuna tukio la watu wawili ambao wameuana wao kwa wao wakigombea mpenzi wao aliyetambulika kwa jina la Hadija Msamati ambaye baada ya tukio hilo alikimbilia kusikojulikana. Jeshi la Polisi tunamtafuta kwa ajili ya tukio hili," alisema.

Kamanda Katembo alisema jeshi linatoa wito kwa jamii kuacha vitendo vya kujichukulia hatua mkoani badala yake wafuate kanuni na sheria ili kuepuka mambo ambayo yanaweza kujitokeza kama hayo ya mauaji.

Katika tukio lingine, Kamanda Katembo alisema watu 24 wakazi wa Chimbuko, Kata ya Mkonjoano wilayani Tandahimba wanashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma sababu za vurugu za kugombania mipaka na kusababisha watu wanne kujeruhiwa.

Alisema watu hao wanne wamelazwa katika Hospitali ya Wilaya ya Tandahimba na alikuwa amepata taarifa kuwa wanaendelea kuimarika kiafya.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Nicomedus Katembo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mawaziri wazingatie kauli ya Rais kuhusu viapo, kutunza siri

**RAIS** Samia Suluhu Hassan jana aliwaapisha mawaziri watatu aliowateua katika mabadiliko madogo ya Baraza la Mawaziri aliyoyafanya juzi. Hafla hiyo ya kuwaapisha mawaziri hao ilifanyika Ikulu, Dar es Salaam, na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali wakiwamo wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama.

Mawaziri walioapishwa ni Innocent Bashungwa ambaye amekuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Stergomena Tax wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Angelah Kairuki Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kabla ya mabadiliko hayo, Bashungwa alikuwa Waziri wa Nchi TAMISEMI, Dk. Tax Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa wakati Kairuki ameteuliwa kuwa mbunge na waziri.

Akizungumza baada ya kuwaapisha, Rais Samia aliwahimiza mawaziri hao pamoja na wengine walioko kwenye nafasi mbalimbali kuheshimu viapo, mipaka yao ya utendaji na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na kutunza siri za Baraza la Mawaziri na serikali kwa ujumla.

Rais alisema mawaziri hao wameapa kwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano, hivyo wanapaswa kutambua kwamba wanafanya kazi katika nchi yenye pande mbili. Kwa mantiki hiyo wanapaswa kuzingatia mipaka ya kazi zao pamoja na kujishusha na pia wanatakiwa kuheshimu viapo vyao.

Lakini kubwa na pengine alilisisitiza kwa umakini mkubwa ni kutunza siri kama walivyoapa au zile za Baraza la Mawaziri na wanazoambiwa katika utendaji wao wa kila siku. Bila kuuma maneno, Rais alisema baadhi ya wateule wamekuwa wakitoa siri jambo ambalo ni makosa.

Aliweka bayana kuwa mwingine anaagizwa kutekeleza jambo, lakini anatoa siri kwamba haikuwa dhamiri yake kutekeleza suala hilo kwa namna linavyofanyika isipokuwa ametakiwa kufanya hivyo.

Kutokana na utoaji huo wa siri, aliwataka kutambua kwamba jambo linapotolewa kwa ajili ya utekelezaji ni la watu wote na si la aliyotoa maagizo. Kwa maana hiyo, katika jambo hilo, Rais alisisitiza uwajibikaji wa pamoja ndani ya serikali badala ya kiongozi wa ngazi fulani kulifanya kama si lake kwa shingo upande.

Rais, kwa kauli yake hiyo, ametoa somo kwa wateule wa kila ngazi kuhakikisha wanatimiza wajibu wao kwa weledi pamoja na kutunza siri za ndani ya serikali. Katika kutekeleza majukumu yao, wanatakiwa kufanya kazi kwa kusimamia viapo vyao na kuheshimu miiko ya uongozi ikiwamo kutokutumia nafasi zao vibaya au kwa upendeleo kama walivyoapa viapo vya maadili.

Pamoja na kuheshimu hayo, mawaziri walioteuliwa na kuapishwa pamoja na wale ambao hawakuguswa katika mabadiliko hayo madogo, watambue kwamba Rais amewaamini kwamba wana uwezo wa kumsaidia katika majukumu mbalimbali ya kisekta, hivyo wafanye kwa nguvu, uwezo na maarifa ili kuthibitisha kwamba wana uwezo.

Kadhalika, kwa Bashungwa, Dk. Tax na Kairuki ambao wamepewa wizara za kuzisimamia, wanapaswa kuelewa kuwa majukumu waliyopewa ni mazito kutokana na unyeti wa nchi. Kutokana na hali hiyo, wanatakiwa kutekeleza majukumu yao kwa weledi na ufanisi wa hali ya juu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253 676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge

# Bila elimu ya maadili ukatili utaumiza taifa

Na Golden Kisapile, (TUDARCo)

**NYAKATI** hizi Watanzania wameshuhudia matukio mbalimbali ya ukatili wa kila aina ukiwamo wa kijinsia, kutoka mikoa karibu yote, ambayo huenda chanzo cha haya yote chaweza kuwa ukosefu wa maadili hasa kwa wanaotenda uovu huo.

Kuna matukio ya wazazi kuua watoto, wanandoa kuuana na hata kuangamiza familia zao, watu wazima kunajisi watoto na panyaroad kujeruhi, kuua na kupora mali za watu mijini.

Aidha, wapo wanaohusishwa na mauaji na wengine kwa madai ya kuwa na hasira kali au kujichukulia sheria mkononi kupiga mawe wahalifu na kuwaua lakini, watoto nao wakiwaua wazazi kwa madai ya kutaka urithi.

Pengine yafuatayo yanaweza kuwa suluhisho la ukatili huu ambao umekithiri mno katika taifa letu ambalo pamoja na kuathiriwa na utandawazi pia lina kundi kubwa la watu wasiopenda kufanyakazi kwa bidii.

Nianze kwa kutoa rai kwa Wizara ya Elimu kuangalia uwezekano wa kuingiza somo la kuukabili ukatili wa kijinsia katika mitaala ya elimu ya msingi, sekondari na vyuo vikuu.

Ninaamini hili linaweza kusaidia watoto kuufahamu ukatili, vyanzo vyake na hivyo kupunguza uovu huo kwa sababu mtu anakuwa na uelewa wa madhara tangu akiwa mdogo.

Pili, kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake, Watoto na Makundi Maalumu, kuboresha mikakati mbalimbali kama vile kutoa elimu kwa upana zaidi na kutumia wadau kuanzia viongozi wa vijiji, dini, makundi maalumu na kualika wageni mahsusi kutoa muhadhara.

Watafahamu athari za ukatili katika jamii, kupitia wataalamu wa wizara na wadau hivyo kupunguza ukatili wa aina zote ukiwamo wa kijinsia katika jamii kwa ngazi mbalimbali.

Kupitia mashirika ya kiserikali na ya kiraia serikali iongeze nguvu ikiwamo bajeti za kufunza wananchi katika ngazi mbalimbali ikitumia warsha, semina na makongamano hata mikutano inayofikia ngazi zote kwa lengo la kufundisha na kubadilisha jamii ili kupunguza madhara ya ukatili wa kijinsia.

Uwe ni mkakati wa kitaifa, mikoani, wilayani, kata na vijijini ili kukomesha ukatili ambao kila mara unakua na kuota mizizi ambayo ni pamoja na kuangamiza maisha.

Viongozi wa dini wanatakiwa kutumia majukwaa yao ya kidini kufundisha na kukemea ukatili ambao unaendelea kutokea katika jamii, hii itasaidia kukemea na kurekebisha hali katika jamii na maeneo mengine.

Wanahabari na wadau wa mawasiliano nao wana jukumu kwenye kuandaa maudhui na vipindi mbalimbali katika vyombo vya habari kuanzia redio, runinga, machapisho ya aina zote, mitandao ya kijamii kama Facebook, Whatsapp, Blog, redio na runinga za kijamii.

Aidha, watoe matangazo kwenye vipaza sauti vinavyozunguka mitaani ambavyo vinahusu kupinga, aina na athari za ukatili wa kijinsia katika jamii.

Yote yangesaidia watu kuelimika kwa kiwango kikubwa kwa sababu utandawazi umechangia kupotosha jamii pia, utafanikisha juhudi za kukomesha ukatili huo kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ambao ni utandawazi pia.

Aidha, Jeshi la Polisi nalo litumike pamoja na watu mashuhuri, viongozi wa kisiasa na wasanii, wafanyabiashara maarufu, wanamichezo na hata wageni wa kimataifa wasisahaulike kwani wanaweza kuwa chachu ya kupinga ukatili mbalimbali na kuwa na Tanzania yenye upendo.

Wazazi na walezi kutoa elimu ya ukatili katika familia zao, ni jambo jema pia, kuanzia baba, mama, mjomba, shangazi, bibi na babu wahusike na malezi hayo.

Ninaamini balozi wa kwanza kumwelimisha mtoto kuhusu madhara ya ukatili katika jamii ni mzazi, mlezi na familia anayoishi nayo, watimize wajibu wao.

Inamaana kila mmoja awe moto nyumbani na jamii wafunzwe, kupiga vita mambo kama vile vitendo vya ushawishi na ulaghai, lugha za vitisho dhidi ya mtu mwingine, ubakaji na unyanyasaji watoto wa kike na kiume, wazee, utumikishwaji wa watoto, vipigo hususan kwa mwanamke, ndoa umri mdogo, ukeketaji na mauaji ya wazee kuua wahalifu na vitendo vyote vinavyoashiria ukatili ili Tanzania iwe salama kila mtu aishi kwa amani.



Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo TIB, Lilian Mbassy (katikati), akikata utepe kuashiria uzinduzi wa maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja iliyoanza jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Meneja Uhusiano na Masoko, Said Mkabakuli (kushoto) na Ofisa Sheria, Rose Mponguliana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Viongozi wapya wa CCM kupewa mafunzo

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, amesema chama kimeona umuhimu wa kuwajengea uwezo viongozi wote wapya.

Amesema kuwa baada ya kukamilika kwa uchaguzi unaondelea kote nchini, viongozi hao watapatiwa mafunzo ili watekeleze majukumu yao kwa ufanisi.

Shaka pia amesema, CCM ni eneo muhimu katika kuzalisha viongozi bora na tegemeo kwa maendeleo ya nchi na ndiyo maana chama hicho kimeendelea kuaminiwa na Watanzania katika kushika hatamu ya kuliongoza taifa.

Shaka, alibainisha hayo juzi aliposhiriki mkutano mkuu wa uchaguzi wa viongozi wa CCM Wilaya ya Dimani, Mkoa wa Magharibi kichama.

Alisema viongozi wanapaswa kufanya kazi kwa kuzingatia mipaka kulingana na Katiba ya CCM, kanuni na miongozo ya chama, hivyo ni lazima kujengewa uwezo kuanzia ngazi ya shina hadi taifa ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo ya Mwenyekiti wa CCM na Rais Samia Suluhu Hassan, katika hatua ya kujiimarisha.

"Wengi tuliopo hapa ni viongozi wapya, tumekabidhiwa dhamana hii muhimu ya uongozi. Chama kimeweka mpango maalum, kama alivyoelekeza Mwenyekiti wetu Samia Suluhu Hassan, ndani ya muda mfupi ujao wa kuwapatia mafunzo elekezi viongozi katika ngazi zote ili kumudu vyema kazi zenu," alisema Shaka.

Chama hicho kiko kwenye mchakato wa uchaguzi wa ndani ambao mwishoni mwa wiki uliingia hatua ya uchaguzi wa wenyeviti wa CCM ngazi ya wilaya.

Katika uchaguzi huo, kumeshuhudiwa baadhi ya vigogo waliokuwa wanataka kutetea nafasi zao, wakiangushwa katika wilaya mbalimbali nchini.

Baada ya hatua hiyo kukamilika, uchaguzi huo utaingia ngazi ya mkoa kuwapa wenyeviti wa CCM mkoa na baadaye ngazi ya taifa.

# Benki yautambua mchango wa wateja

**Na Mwandishi Wetu**

BANK OF AFRICA inaadhimisha Wiki ya Huduma kwa Wateja kwa kuwashukuru wateja wake kuendelea kuiamini na kufurahia huduma zake mbalimbali.

Benki hiyo ya kimataifa yenye mtandao mkubwa wa shughuli zake barani Afrika, itatumia maadhimisho haya kwa kuwatambua wafanyakazi wake ambao wanaendelea kutoa huduma nzuri kwa wateja katika matawi yake yote nchini.

Maadhimisho haya yenye kauli mbiu ya 'Sherehekea Huduma', yataambatana na shughuli mbalimbali katika matawi yote ya benki nchini kote kama vile kutoa zawadi kwa wateja.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa wiki hiyo kwenye tawi kuu la benki, Posta jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mtendaji na Ofisa Mtendaji Mkuu wa benki hiyo, Adam Mihayo, alitoa shukrani kwa wateja kwa kuendelea kuiamini benki yao kwa miaka mingi.


Alisema: "Kutoa huduma za kuridhisha wateja na kupata mrejesho na maoni ndiyo msingi wa shughuli zetu. Tunaamini kwamba siku tunapoacha kutathmini biashara yetu na jinsi huduma yetu inavyoathiri wateja, tutakwama kibiashara. Ndiyo maana tunaendelea kujitoa kuwapatia huduma bora na kuboresha shughuli zetu."

Maadhimisho ya kila mwaka ya Wiki ya Huduma kwa Wateja hutumiwa kuleta mkazo katika masuala yanayowakabili wateja na kutafuta njia bunifu za kuyashughulikia.

Mihayo alisema kuwa kama benki inayozingatia wateja, BANK OF AFRICA kwa miaka mingi inatumia maadhimisho hayo kuweka mkakati wa kuimarisha huduma bora kwa wateja, kipengele muhimu cha maadili yake ya msingi na kupata maoni ya wateja huku ikiwathamini kwa uaminifu wao na uamuzi wa kufanya biashara na benki.

Kwa kuelewa umuhimu wa ushirikishwaji katika mfumo rasmi wa kifedha na kuonyesha uzoefu wa kutoa huduma bora kwa wateja, Mihayo alisema benki imefanya uwekezaji ili kuboresha mifumo yake ya kidijitali ikiwa ni pamoja na majukwaa ya huduma za kibenki kwa njia ya simu na mtandao wa intaneti, ili kusaidia kujenga jamii isiyotumia fedha taslimu kupata huduma mbalimbali.

## KABWELA



# CRDB yashukuru wateja kwa mafanikio utoaji huduma bora

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI kampuni na taasisi nyingi duniani zikiadhimisha 'Wiki ya Huduma kwa Wateja' mwaka 2022, Benki ya CRDB imeianza wiki hiyo kwa kuwashukuru wateja wake kwa maoni na ushauri ambao umeiwezesha kutoa huduma bora na zenye viwango vya kimataifa kwa jamii.

Salamu hizo za shukrani zilitolewa jana na Ofisa Mkuu wa Fedha wa Benki ya CRDB, Fredrick Nshekanabo wakati wa hafla iliyofanyika katika tawi la benki hiyo lililopo Oysterbay jijini Dar es Salaam.

Nshekanabo alisema, wateja wamekuwa msingi mkubwa kwa CRDB kufikia mafanikio ambayo imekuwa ikiyapata kufikia kuwa 'Benki Bora zaidi Tanzania'.

"Tukiongozwa na kaulimbiu yetu ya 'Benki Inayomsikiliza Mteja' tumekuwa tukipokea maoni na ushauri wa wateja ambao kwa kiasi kikubwa umechangia ubora wa huduma na bidhaa zinazotolewa na benki yetu.

"Hii inaonyesha ni kwa namna gani mteja amepewa kipaumbele kikubwa katika mkakati wa biashara yetu," alisema Nshekanabo.

Mkuu wa Kitengo cha Huduma kwa Wateja wa Benki ya CRDB, Yolanda Uriyo alisema, pamoja na kuwashukuru wateja katika Wiki ya Huduma kwa Wateja mwaka huu wamedhamiria kusherehekea kwa kuwatambua wale wote walio mstari wa mbele kuiwezesha benki hiyo kutoa huduma bora.

"Wakati dunia nzima ikiadhimisha wiki hii kwa kaulimbiu ya 'Celebrate Service' inayomaanisha kusherehekea huduma, kwetu CRDB hii ni zaidi ya kaulimbiu kwani mafanikio tuliyonayo yanatulazimisha kuwasherehekea wanaotufanya tuwe bora zaidi; wateja na wafanyakazi wetu," alifafanua Uriyo.

Alisema, CRDB itaitumia wiki hii kuwashukuru na kusherehekea kwa kuwatambua wateja ambao wamekuwa chachu ya huduma bora zinazotolewa na benki hiyo.

Pia alisema, watakuwa wakisherehekea kwa kuwatambua wafanyakazi ambao wamekuwa wakitoa huduma bora kwa weledi na ubunifu mkubwa.

Benki ya CRDB inatajwa kuwa benki inayoongoza kwa huduma bora kwa wateja. Mwaka huu benki hiyo imetunukiwa tuzo ya 'Benki Bora Tanzania' na jarida maarufu duniani la Uingereza la Euromoney.

Mwishoni mwa mwaka jana, benki hiyo ilitunukiwa 'Tuzo ya Ubora' na Taasisi ya Utafiti wa Ubora barani Ulaya (European Society for Quality Research).

Katika miaka ya hivi karibuni, Benki ya CRDB imeweka kipaumbele na kufanya uwekezaji mkubwa katika huduma kwa wateja.

Benki hiyo imewekeza katika mifumo ya kisasa na ya kidijitali ya utoaji huduma, ikiwamo mifumo ya mawasiliano, ambayo imesaidia kuongeza ufanisi katika matawi yake zaidi ya 260 yaliyosambaa kote nchini.

Uwekezaji huu pia, umeongeza ufanisi katika njia




Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe (wa pili kulia), akimkabidhi zawadi mmoja wa wateja wa Benki ya CRDB, Dk. Redempta Mbatia (kushoto), katika hafla ya ufunguzi rasmi wa Wiki ya Huduma kwa Wateja yenye kauli mbiu 'Sherehekea Huduma' iliyofanyika kwenye tawi la benki hiyo, jana Oysterbay, Dar es Salaam. Wengine ni Ofisa Mkuu wa Fedha, Fredrick Nshekanabo (wa pili kushoto) na Mkuu wa Kitengo cha Huduma kwa Wateja, Yolanda Uriyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ACT yataka hatua kuwanusuru wananchi kuvamiwa na ndovu

**Na Mwandishi Wetu,** TUNDURU

CHAMA cha ACT-Wazalendo, kimeitaka Wizara ya Maliasili na Utalii kuchukua hatua madhubuti kuwanusuru wananchi wanaoishi karibu na maeneo ya hifadhi na mbuga za wanyama dhidi ya mauaji na uharibifu wa mazao unaofanywa na ndovu.

Katibu Mkuu wa chama hicho, Ado Shaibu alitaka kuchukuliwa kwa hatua hizo alipozungumza na wanachama wa ACT- Wazalendo katika Kata ya Marumba wilayani Tunduru jana.

"Mwaka huu nimefanya ziara katika maeneo yanayozunguka Mbuga ya Selous. Kuna wimbi kubwa sana la tembo wanaotoka mbugani na kuvamia mashamba na vijiji hasa kwenye mikoa ya Lindi na Ruvuma.

"Hapa Tunduru kwa mfano, tembo wanavamia vijiji mara kwa mara, kuharibu mazao ya wakulima, kujeruhi na kuua watu.

"Hali hii haikubaliki. Ni lazima serikali iwajibike. Mosi, lazima Wizara ya Maliasili na Utalii ifanye utafiti wa kina kubaini chanzo cha kuongezeka kwa matukio ya tembo wengi kukimbia maeneo ya mbugani na kuvamia vijiji katika miaka ya hivi karibuni.

"Pili, ni lazima serikali iimarishe Idara ya Wanyamapori kuwezesha kuwapo kwa askari wanyamapori wa kutosha kwenye maeneo yaliyoathirika zaidi.

"Tatu, ni lazima wananchi wapewe mbinu na uwezo na kujihami na pale mazao yao yanapoharibiwa, wapewe fidia ya kutosha na ya mapema," alisema.

Katika hatua nyingine, Ado amewataka viongozi na wanachama wa ACT-Wazalendo katika mikoa ya magharibi mwa nchi (Tabora, Katavi, Kigoma, Shinyanga na Mkoa wa kichama Kahama) na kusini mwa nchi (Pwani, Lindi, Mtwara na Mkoa wa kichama wa Selous) kujiandaa kwa operesheni kubwa ya ujenzi wa chama itakayofanyika Oktoba na Novemba 2022.

"Halmashauri Kuu Taifa katika kikao chake kilichopita imeelekeza viongozi wote wa taifa kwa kushirikiana na viongozi wa mikoa husika tukapige kambi kwenye mikoa hiyo kujenga chama kwenye ngazi za matawi, kata, majimbo na mikoa. Viongozi wa mikoa husika wajiandae," aliagiza.

Kwa mujibu wa Janeth Rithe, Naibu Katibu Idara ya Habari, Uenezi na Uhusiano wa Umma ACT Wazalendo, Ado anaendelea na ziara ya wiki moja ya kuimarisha chama kwenye majimbo ya Tandahimba, Tunduru Kusini na Tunduru Kusini.

# Wanawake wahasibu walivyoikosha serikali

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imesema inafurahishwa na idadi kubwa ya wanawake wanaojitokeza kusomea fani ya uhasibu, ikibainisha kuwa sasa wamekuwa idadi sawa na wanaume.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Lawrence Mafuru, alibainisha hayo wakati wa mahafali ya 44 ya Bodi ya Taifa ya Uhasibu na Ukaguzi (NBAA).

Alisema, kwa miaka mingi fani hiyo ilikuwa imetawaliwa na idadi kubwa ya wanaume lakini inafurahisha kuona kwa sasa wanawake wengi wamechangamkia na kuwa 50/50.

"Takwimu ambazo nimetajwa hapa zinaonyesha kwamba sasa wanawake wengi wameamua kwa dhati kabisa kuchangamkia fani hii ambayo kwa muda mrefu tuliona ikihodhiwa na wanaume pekee," alisema.

Mafuru alisema, jitihada zilizochukuliwa kuwahamasisha wanawake kusomea fani hiyo zinapaswa kuwa endelevu ili kuhakikisha idadi inaongezeka hata ikiwezekana kuwapita wanaume.

Aliipongeza NBAA, kwa kuendeleza taaluma ya uhasibu kwa weledi na kwa ubunifu wa hali ya juu licha ya vikwazo mbalimbali wanavyokabiliana navyo ikiwamo rasilimali watu.

"Kwa miaka miwili iliyopita tulipata shida ya UVICO-19 na katika hali ya kawaida ungetarajia mitihani isimame lakini waliendelea online (kwa njia ya mitandao) na kuzalisha CPA, ninawapongeza sana.

"Zipo taasisi zilizosimamisha shughuli sababu ya COVID lakini hapa tunajifunza kwamba katika shida tunapaswa kufikiri zaidi," alisema.

Aliongeza kuwa, serikali inahitaji wahasibu wengi wenye viwango vinavyotakiwa watakaofanya kazi kwa weledi na kwa kufuata maadili ya taaluma zao.

Alisema taaluma ya uhasibu ni fani iliyotukuta, hivyo wanapaswa kulinda taswira yake kwa jamii kwa kuacha kufanya mambo ambayo yataifanya idharauriwe kama vile kuandaa ripoti za kihasibu za ujanja ujanja.

"Kuna wahasibu wanakula njama na wateja wao kwenye kuandaa hesabu tofauti tofauti, anaandaa hesabu ya kupeleka TRA, hesabu ya kupeleka benki kwa ajili ya kupata mikopo, sasa ukigundulika ni wewe umefanya unapoteza sifa yako na unaweza kupokonywa cheti na NBAA.

"Ukitaka kujua kwamba hii ni fani muhimu na yenye heshima ya kipekee, angalia idadi ya Watanzania na idadi ya wahasibu waliopo tangu kuanzishwa kwa NBAA mwaka 1972.

"Nimeambiwa hapa na Mkurugenzi wa NBAA kwamba mpaka sasa mko 12,000 kati ya Watanzania milioni 60, hivyo lazima mheshimu fani yenu," alisema.

## Tanzania yachaguliwa mjumbe Baraza la Mawasiliano

**Na Mwandishi Wetu,** BUCHAREST

TANZANIA imechaguliwa kuwa Mjumbe wa Kamati Tendaji ya Shirika la Mawasiliano Duniani (ITU), uchaguzi uliofanyika jana wakati wa Mkutano Mkuu wa Shirika hilo uliofanyika jijini Bucharest, Romania.

Tanzania imeshinda nafasi hiyo kwa kura 141 kati ya 180 zilizopigwa. Akizungumzia ushindi huo, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye alisema umetokana na jitihada ambazo serikali imekuwa ikizifanya kuwezesha ushindi huo kupatikana.

Katika mkutano huo, Tanzania imewakilishwa na wataalamu wa sekta ya mawasiliano kutoka Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari walioambatana na wataalamu wengine wa taasisi za mawasiliano wakiwamo wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) na TTCL.

Mchakato wa kuwania nafasi hiyo ulianza baada ya kuundwa kwa kamati ya kitaifa ya mkutano huo ambayo iliratibu kazi mbalimbali zilizowezesha Tanzania kurejea tena kwenye baraza hilo muhimu katika sekta ya mawasiliano.

Kuchaguliwa kwa Tanzania kwenye baraza hilo kuwa mjumbe anayewakilisha Kundi 'D' linalohusisha nchi za Afrika kwa mwaka 2023-2026, unaipa nchi nafasi muhimu na adhimu kutetea masuala ya mawasiliano yanayohusu ukuzaji wa teknolojia za mawasiliano na namna zinazovyoathiri maisha ya wananchi kila siku.

Kabla ya uchaguzi wa wajumbe wa Baraza hilo Tendaji, wajumbe wa nchi 193 wanachama wa shirika hilo walimchagua, Doreen Bogdan-Martin wa Marekani kuwa Katibu Mkuu Mtendaji wa ITU, Shirika la Umoja wa Mataifa lenye dhamana ya kusimamia masuala ya mawasiliano duniani, ukiwamo mgawanyo wa masafa ya mawasiliano, masuala ya mawasiliano ya satelaiti, usambazaji wa huduma za mawasiliano na ukuzaji wa teknolojia za mawasiliano miongoni mwa masuala mengine.

# Mradi ujenzi wa Daraja la Jangwani kuanza Desemba

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAKALA wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) umetaja miradi mbalimbali itakayotekelezwa kwa mwaka 2022/23 huku ukibainisha ujenzi wa Daraja la Jangwani mkoani Dar es Salaam utaanza rasmi Desemba 31, mwaka huu, ili kuondokana na tatizo sugu la mafuriko.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapo, Mtendaji Mkuu wa TARURA, Victor Seff, alisema mradi wa ujenzi wa daraja hilo na uendelezaji Bonde la Mto Msimbazi unagharimu dola za Marekani milioni 260.

"Mradi upo katika hatua za maandalizi ambapo usanifu wa Daraja la Jangwani umekamilika na maandalizi ya nyaraka muhimu za mambo ya kijamii na mazingira yamekamilika," alisema.

Mtendaji Mkuu alisema upembuzi yakinifu pamoja na usanifu wa miundombinu ya mto umekamilika na mkataba wa mkopo kati ya Serikali ya Tanzania na Benki ya Dunia ulitiwa saini Septemba 30, mwaka huu.

"Mradi unatarajiwa kuanza rasmi Desemba 31, mwaka 2022, taratibu za kuwapata makandarasi wa ujenzi zitaanza mwezi Novemba 2022. Kazi za ujenzi za mradi huu zinatarajiwa kuanza ndani ya mwaka wa fedha 2022/23," alisema.

Alibainisha kuwa mradi wa daraja hilo utachukua takribani miaka mitatu.

Awali alisema kuwa mwaka wa fedha 2022/23 ni mwaka wa pili wa utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Pili ambapo TARURA imetengewa bajeti Sh. bilioni 838.16.

"Lengo kwa mwaka huu wa fedha ni kufanya matengenezo ya kawaida kilometa 21,595.72, kujenga au kukarabati kilometa 422.07 kwa kiwango cha lami, kujenga au kukarabati kilometa 11,074.56 kwa kiwango cha changarawe na kujenga au kukarabati madaraja 269," alisema.

Alibainisha kuwa katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2022/23, zabuni 1,706 zenye thamani ya Sh. bilioni 621.66 zimepangwa kutangazwa.

"Awamu ya kwanza tulitangaza asilimia 60 ya bajeti sawa na zabuni 1,085 zenye thamani ya Sh. bilioni 378.56, ikiwa ni ununuzi wa asilimia 60 ya bajeti ili kazi zianze mapema kabla ya msimu wa mvua kuanza," alisema.

Akizungumzia mradi wa uendelezaji wa miji 45 (TACTIC), alisema unagharimu dola za Marekani milioni 268 ikiwa ni mkopo nafuu kutoka Benki ya Dunia.

"Mradi uko kwenye hatua za mwisho za maandalizi ambapo usanifu wa miradi katika miji 12 ya mwanzo umekamilika. Mkataba wa mkopo kati ya Serikali ya Tanzania na Benki ya Dunia, ulitiwa saini tarehe 16 Juni, 2022," alisema.

Mtendaji Mkuu huyo alisema mradi unatarajiwa kuanza rasmi Oktoba 14, 2022 ambapo taratibu za ununuzi ili kuwapata makandarasi wa ujenzi pamoja na wataalamu washauri wa usanifu wa miradi ya kundi la pili la miji 15 zitaanza Novemba, 2022.

Awali Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa alisema kwa miaka miwili TARURA na Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) zimepewa Sh. trilioni 4.7 za kuimarisha barabara nchini.



Mkurugenzi Mtendaji na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bank of Africa, Adam Mihayo, akiongea na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi wa Wiki ya Huduma kwa Wateja katika tawi kuu la benki hiyo jijini Dar es Salaam jana, wengine (kulia) ni Naibu Mkurugenzi Mkuu, Wasia Mushi, Naibu Mkurugenzi Mkuu (wa tatu kulia), Samir Yassine, (wa nne kulia) ni Mkuu wa Kitengo cha Huduma kwa Wateja, Anna Mango. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Serikali ibainishe pombe zinazoleta shida kiafya'

**Na Christina Haule,** MOROGORO

MTANDAO wa asasi zinazopinga matumizi mabaya ya pombe (TAAnet) umeitaka serikali kutambua na kubainisha aina zote za pombe zinazoleta maradhi kwenye mwili wa binadamu na kuhakikisha zinazuiwa kutengenezwa na kusambazwa nchini ili kunusuru afya ya wananchi.

Katibu wa mtandao huo, Gladness Munuo, aliwasilisha hoja hiyo jana alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu Siku ya Maadhimisho ya Kupinga Matumizi ya Pombe Kupita Kiasi Duniani ambayo hufanyika Oktoba 3 kila mwaka.

Alisema kuwa matumizi ya pombe na athari zake ni tatizo linalozidi kukua nchini, hivyo kuna haja serikali na wadau kuchukua hatua.

Munuo alisema suala hilo linapaswa kudhibitiwa kwa haraka iwezekanavyo hasa wakati huu ambao kuna aina nyingi za vilevi vyenye kiwango kikubwa kwa kileo, hivyo kuharibu akili za watumiaji hasa vijana ambao ni tegemeo na nguvu kazi ya taifa.

Alisema ni dhahiri zipo nchi ambazo tayari zimeshachukua hatua stahiki kwa kuzuia matumizi ya pombe hizo ikiwamo Kenya, Uganda, Malawi, Zambia, Afrika Kusini na Burundi ambazo sasa zina sera za kudhibiti matumizi mabaya ya pombe na tayari matokeo chanya kwa jamii yao yameonekana.

Alisema wanaipongeza Wizara ya Elimu kwa kuanzisha mtaala wenye kuelezea madhara ya pombe na jinsi ya kuepuka, ukifundishwa shuleni.

"Tunayo imani kubwa kuwa mikakati ya kuwa na 'Sera ya Afya yenye kuweka katazo la matumizi mabaya ya pombe itazingatiwa ikiwa pamoja na kuwapo mwongozo wa kudhibiti utengenezaji, usambazaji na matumizi ya kinywaji chochote kile chenye kilevi nchini, utapewa kipaumbele," alisema.

Alirejea utafiti wa mwaka 2021 uliofanywa na Shirika la Kimataifa la IOGT-NTO Movement lenye ofisi zake jijini Dar es Salaam, ulioangalia kiwango cha matumizi ya kinywaji cha pombe kwa jamii na kubaini kuwa asilimia 40 ya wanawake mpaka sasa ndiyo wanaotumia pombe kwa kiasi cha kunywa mara mbili mpaka mara nne kwa wiki nchini.

Ripoti ya utafiti huo ilibainisha kuwa asilimia 51 ya wanaume hunywa pombe na ni kiasi cha zaidi ya mara tatu kwa wiki, bila kuzingatia aina ya pombe inayotumika.

Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Afya Duniani (WHO) ya Mei mwaka huu, matumizi mabaya ya pombe ni moja ya vyanzo cha magonjwa takribani 200, pia ajali za barabarani.

WHO inabainisha kuwa takribani watu milioni tatu kila mwaka hupoteza maisha kutokana na unywaji wa pombe, ikiyataja matumizi ya pombe kupita kiasi kuwa sehemu ya madhara makubwa katika jamii, yanayojumuisha kuongezeka kwa vitendo vya ukatili wa kijinsia na kuyumba kwa uchumi wa familia.

# Serikali yaridhishwa kasi ujenzi kinu cha kupoza umeme GGML

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

WAZIRI wa Madini, Dk. Dotto Biteko ameeleza kuridhishwa na kasi ya ujenzi wa kinu cha kupoza umeme (substation) kinachojengwa na Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) ili kuwezesha mgodi huo kuachana na uzalishaji wa umeme wa mafuta na kuhamia kwenye umeme wa Gridi ya Taifa ambao ni nafuu.

Mgodi huo unajenga kinu hicho kitakachokuwa na uwezo wa kupitisha umeme wenye kilovolt 13 kwenye mitambo yake ambapo hadi kikamilike kinatarajiwa kugharimu Sh. bilioni 50.

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) nalo linajenga njia ya kupeleka umeme katika mgodi wa GGML yenye urefu wa kilomita sita.

Katika ziara yake mgodini huko juzi, Dk. Biteko, pamoja na mambo mengine, alisema anaamini hadi kufikia Machi mwaka 2023, GGML itaanza kutumia umeme wa Gridi ya Taifa.

"GGML wanataka kuhama kutoka kwenye matumizi ya umeme unaozalishwa kwa mafuta kwenda kwenye umeme wa TANESCO kupitia 'substation' inayojengwa kwa dola za Marekani milioni 20.

"Wamekwenda kwenye hatua nzuri, ninaamini mpaka itakapofika Machi mwaka kesho (2023) tutawasha umeme wa TANESCO kuendesha mgodi wetu hapa ndani," alisema Dk. Biteko.

Awali Makamu Rais wa Kampuni ya AngloGold Ashanti inayomiliki GGML, Simon Shayo, alisema kukamilika kwa mradi huo kutapunguza gharama za uendeshaji wa mgodi kwa kutumia umeme kwa zaidi ya asilimia 50.

Alisema mgodi wa GGML unatumia zaidi ya MW 40 zinazozalishwa kwa kutumia jenereta linalotumia mafuta ya dizeli tangu mwaka 2018.

"Sasa tupo kwenye mchakato wa kujenga kinu cha kupozea umeme chenye thamani ya karibu Sh. bilioni 50 na TANESCO watajenga njia ya kilomita sita kufika hapa.

"Kwa hiyo, hadi kufikia Machi 2023, tutakuwa tumeingia kwenye umeme wa TANESCO na tutakuwa tumepunguza gharama yetu ya umeme kufikia asilimia 50 kutoka uniti moja kwa senti 19 kwenda kwenye uniti moja kwa senti tisa," alifafanua.

Ilibainishwa kuwa kukamilika kwa mradi huo wa kupeleka umeme GGML kunatarajiwa kuiwezesha TANESCO kupata Sh. bilioni tano kwa mwezi zitakazotokana na mauzo ya umeme.



Waziri wa Madini, Dk. Dotto Biteko (wa pili kulia), akipata maelezo kuhusu mradi wa kinu cha kupoza umeme kutoka kwa Meneja anayehusika na miundombinu ya GGML, Eliakimu Kagimbo, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## RC aonya lugha chafu vituo afya

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, amewaonya watoa huduma za afya mkoani hapo watakaobainika kutoa lugha chafu kwa wazee wanapokwenda kupata matibabu kwenye vituo vilivyoainisha, akisisitiza kuwa wakibainika watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Alitoa onyo hilo juzi wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wazee Duniani yaliyofanyika kimkoa katika Wilaya ya Ikungi mkoani hapo.

Kupitia hotuba yake iliyosomwa kwa niaba yake na Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Jerry Muro, Serukamba alisema serikali itahakikisha hakuna mzee atakayetolewa lugha mbaya na watoa huduma za afya.

Alisema serikali imedhamiria kuondoa kero ya upatikanaji wa dawa kwa wazee ambapo hivi sasa upatikanaji kwa mkoa umeongezeka hadi kufikia asilimia 94.

Serukamba aliagiza katika vituo vya kutolea huduma za afya vitengwe vyumba na madirisha ya kutoa huduma kwa wazee na kutolewe matangazo yenye ujumbe unaosomeka kuwa 'Mpishe Mzee Ahudumiwe Kwanza'.

Kuhusu vitendo vya ukatili kwa wazee, alisema Mkoa wa Singida hautakubali kuona vitendo hivyo vinajitokeza na kuwataka wananchi kuachana na imani potofu za kishirikina ambazo zinachochea mauaji dhidi ya wazee.

Mkuu wa Mkoa alisema hadi kufikia Juni 2022, mkoa ulikuwa unawatambua wazee 55,920 ambapo hadi sasa wazee 10,385 sawa na asilimia 19 wamepatiwa vitambulisho vya matibabu.

Aliagiza viongozi wakiwamo wakuu wa wilaya kuhakikisha wanasimamia wazee wote katika wilaya zao wanapatiwa vitambulisho vya matibabu haraka.

Kuhusu uundwaji wa mabaraza ya wazee, Serukamba alisema hilo ni agizo la serikali, hivyo lazima litekelezwe na kwa sasa yapo mabaraza 637 yaliyoanzishwa mkoani hapo katika ngazi za wilaya.

"Ninawaagiza wakurugenzi wa halmashauri za wilaya hakikisheni mnasimamia ili mabaraza yaliyoanzishwa yafanye kazi kwa ufanisi kama ambavyo yameainishwa kwenye Sera ya Wazee ya Mwaka 2913," alisema.

# Wanaopona TB wabainika kupata shida katika mapafu

**Na Devota Mwachang'a**

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dk. Seif Shekalaghe, amewataka wataalamu wa afya nchini kufuatilia maendeleo ya watu waliougua kifua kikuu (TB), ili kubaini magonjwa wanayopata baada ya kupona ugonjwa huo na kuyapatia ufumbuzi.

TB ni ugonjwa wa kuambukiza unaosababishwa na bakteria aitwaye mycobacterium tuberculosis.

Imebainika wagonjwa wa TB wakimaliza kutumia dawa na kupona, hupata shida zitokanazo na tiba hiyo ikiwamo mapafu kushindwa kufanya kazi inavyotakiwa.

Hayo yalibainishwa wakati wa mkutano wa wadau wa mradi wa TB Sequel uliofanyika makao makuu ya Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) mkoani Dar es Salaam mwishoni mwa wiki.

Dk. Shekalaghe alisema: "Matokeo ya utafiti yanaonyesha wagonjwa wa TB baada ya kutumia dawa, baadhi hupata madhara ikiwamo kupungua kwa uwezo wa mapafu yao kufanya kazi.

"Wataalamu wa afya wanapaswa kuwasaidia kwa kutambua matatizo hayo na kuwashauri njia ya kujilinda pamoja kutovuta sigara na kuepuka mazingira yenye moshi mwingi."

Kiongozi huyo pia alitoa wito kwa wanasayansi kuendelea kufanya utafiti wenye tija na wafikirie kwa upana ili kuangalia mambo yote na pia kuishauri serikali mambo ya msingi yanayotakiwa kuwekwa katika njia za matibabu. Madaktari wanapowatibu wagonjwa, wafanye kwa umoja (holistic approach) na kuwapa elimu."

Mkurugenzi wa Vikundi vya Watu Waliougua na Kupona TB, Dk. Willy Mbalawa alisema: "Mimi niliugua TB ya nje ya mapafu. Kwa kawaida mgonjwa huangaliwa pale tu anapokuwa anapatiwa matibabu lakini akipona, hakuna anayemfuatilia anaishije au mgonjwa amepatwa na madhara gani. Madhara tuyapatayo ni makubwa, inasadikiwa TB ni ugonjwa wa watu maskini."

Mratibu wa mradi huo na Mkuu wa Kituo cha NIMR Mbeya, Nyanda Ntinginya alisema: "Utafiti wetu ulianza mwaka 2017 kwa nchi nne kwa ufadhili wa Ujerumani ambao ndiyo watoa fedha, inakisiwa kuwa zaidi ya watu milioni 150 duniani waliofanyiwa utafiti wamegundulika kuwa hai baada ya kuugua TB na kutibiwa.

"Ujumbe mkuu kwetu ni kuangalia njia bora na kutoa mapendekezo na kuangalia mgonjwa baada ya kupewa tiba, anapata na shida gani.

"Wadau wa maendeleo na mashirika mengi ikiwamo WHO (Shirika la Afya Duniani) na programu nyingi za TB duniani zilikuwa hazijawaangalia wagonjwa baada ya kumaliza tiba kuangalia kama yule mdudu (bakteria) amepona, wengi wanahitaji kuangaliwa kwa kuwa wanaugua magonjwa mengine."

Mwaka 2020 jumla ya wagonjwa 85,597 wapya wa kifua kikuu waliripotiwa nchini. Kati yao, zaidi ya asilimia 90 walifanikisha matibabu yao.

Pamoja na kuwapo jitihada zenye matokeo chanya zilizofanyika na kusababisha kupunguza idadi ya wagonjwa wapya, Tanzania ni miongoni mwa nchi 30 duniani zenye idadi kubwa ya wagonjwa wa TB.

Mradi wa TB Sequel ni wa miaka mitano (2017-2022) ukifadhiliwa na serikali za Ujerumani na Tanzania, ukitekelezwa katika nchi nne za Tanzania, Afrika Kusini, Msumbiji na Gambia.

# Milioni 200/- kumaliza tatizo uhaba madarasa shule nne

**Na Allan Isack,** ARUMERU

SERIKALI imetenga Sh. milioni 200 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa katika shule nne za msingi za Halmashauri ya Arusha, hali itakayomaliza tatizo la wanafunzi kukaa chini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Seleman Msumi, aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari na kueleza kuwa mradi huo utahusisha ujenzi wa nyumba nne za walimu zitakazojengwa kila moja kwa gharama ya Sh. milioni 50.

"Nia ya serikali ni kuendeleza mpango wa kuboresha miundombinu ya shule, hasa ujenzi wa nyumba za walimu na vyumba vya madarasa ili kuweka mazingira rafiki ya kujifunza na kufundishia, kwa mwanafunzi na kwa walimu.

"Niishukuru sana serikali kwa kuona umuhimu wa kutoa fedha za kujenga nyumba za walimu kwa shule za pembezoni mwa mji. Shule ambazo katika maeneo hayo, walimu hulazimika kuishi mbali na shule, kwa kukosekana kwa nyumba za kupanga karibu na shule," alisema.

Shule zitakazonufaika ni Shule ya Msingi Ereto iliyoko Kata ya Laroi ambako kutajengwa nyumba za walimu na Shule ya Msingi Shikizi ya Engedeko ya Kata ya Oldonyowas.

Imo pia Shule ya Msingi Olokii, Shule Shikizi ya Olmapinuu iliyoko Kata ya Bwawani na Shule ya Msingi Olemedeye ya Kata ya Nduruma.

Kwa mujibu wa Msumi, shule zote hizo ziko umbali wa kati ya kilomita 40 hadi 60 kutoa makao makuu ya halmashauri hiyo.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Engedeko, Gideon Sombe, akizungumzia mradi huo, alipongeza serikali kwa kuwa shule hiyo ni mpya na imeanza mwaka huu.

"Shule ya Engedeko ilikuwa ni shule shikizi, baada ya ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa ya UVIKO- 19, imesajiliwa na kuwa shule ya msingi. Pia ina walimu wanne na haina nyumba hata moja.

Alisema: "Hivyo ujenzi wa nyumba hii, utakuwa ni miongoni mwa shule zinazokuwa kwa kasi kwa kukidhi mahitaji ya walimu na elimu kwa watoto wa Kijiji cha Losinoni Juu."

**Shule ya Engedeko ilikuwa ni shule shikizi, baada ya ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa ya UVIKO- 19, imesajiliwa na kuwa shule ya msingi. Pia ina walimu wanne na haina nyumba hata moja.**

# Wanafunzi shule za umma kunufaika ufadhili wa Samia

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda amesema asilimia 62 ya wanafunzi wanaostahili kupata ufadhili wa masomo kupitia 'Samia Scholarships' watatoka katika shule za umma.

Pia amefafanua kuwa wanafunzi 640 watakaobahatika kunufaika na ufadhili huo serikali itawashawishi kusomea sayansi, uhandisi na elimu tiba. Prof. Mkenda alitoa ufafanuzi huo jana kupitia Jukwaa la Kanda ya Kaskazini alipokuwa akijibu maswali ya wadau mbalimbali wa elimu, wanasiasa na wasomi wa kada mbalimbali nchini.

"Kwenye hili tunatafuta the best of the best (mwanafunzi mzuri zaidi), tuwashawishi wasome sayansi, uhandisi na elimu tiba. Tusichanganye jambo hili na umuhimu wa kutawanya fursa za elimu kwa usawa. Hili la usawa ni muhimu mno na lina mikakati yake na lazima tuongeze bidii huko.

**Kwenye hili, tunataka tuzalishe wanasayansi wazuri, wahandisi mahiri na madaktari bingwa, ukienda hospitali kufanyiwa upasuaji, utataka madaktari na wahudumu bora kabisa.**

"Kwenye hili, tunataka tuzalishe wanasayansi wazuri, wahandisi mahiri na madaktari bingwa, ukienda hospitali kufanyiwa upasuaji, utataka madaktari na wahudumu bora kabisa.

"Tunataka kupunguza wimbi la wahitimu bora wa sayansi kidato cha sita kuendelea zaidi kusoma biashara na masomo kama haya na kukwepa sayansi, teknolojia na elimu tiba. Tusipofanya hivi, tutabaki watu wa kulalama na kunung'unika tu na hatutaenda popote. Kumbuka, siyo madini wala rasilimali nyingine zinazonyanyua mataifa, ni sayansi na teknolojia," alisema.

Katika ufafanuzi wake, Waziri Mkenda, alisisitiza kwamba mpango huo hauondoi haja ya taifa kushawishi wenye vipaji kusoma sayansi, teknolojia na elimu tija.

Kuhusu suala la upendeleo, Prof. Mkenda, ameeleza kuwa suala la usawa na haki kwake ni jambo muhimu mno, hivyo wizara yake inawahakikishia Watanzania kwamba hakutakuwa na upendeleo.

Kwa mujibu wa Waziri Mkenda, moja ya kigezo cha kupata ufadhili ni mwanafunzi kudahiliwa kwenye vyuo vikuu vya ndani ya nchi ili kusoma masomo ya sayansi, uhandisi na elimu tiba.

Alisema, kwa mwanafunzi ambaye atadahiliwa kwenye masomo ambayo si ya sayansi, hatanufaika na ufadhili huo hata kama jina lipo kwenye orodha.

Wizara hiyo imetenga Sh. bilioni tatu, ambazo zinaweza kuwatosha wanafunzi 640 kwa mwaka wa kwanza.



Mwenyekiti mpya wa CCM Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Kiria Laizer (kushoto), akishukuru wanachama baada ya kushinda kwa kura 315 juzi, (katikati) ni Mbunge wa Simanjiro, Christopher Ole Sendeka na Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Dk. Suleiman Serera. **PICHA: GIFT THADEY**

# Tril. 14/- zahitajika kukabili athari mabadiliko tabianchi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

TANZANIA inahitaji zaidi ya Dola za Marekani bilioni 19.2 (Sh. trilioni 14.4) kwa ajili ya kufanikisha shughuli mbalimbali za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Kwa mujibu wa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, upatikanaji wa fedha hizo ni muhimu katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, ambayo kwa sasa athari zake zinashuhudiwa kila mahali ikiwamo ukame.

Dk. Jafo aliyasema hayo jana jijini Arusha alipofungua mkutano wa siku nne wa wataalamu wa mazingira ulioandaliwa na Benki ya Dunia (WB), kwa ajili ya kujadili pamoja na mambo mengine, jinsi ya kupata fedha za kukabiliana na tatizo hilo.

"Pamoja na kuwapo tatizo hilo, Tanzania imepiga hatua mbalimbali za kudhibiti mabadiliko hayo, ikiwamo kuanzisha Bwawa la Mwalimu Nyerere na Reli ya Kisasa (Standard Gauge) inayounganisha Bandari ya Dar es Salam na nchi jirani za Rwanda na Burundi," alisema.

Waziri huyo alisema Tanzania inapambana na mabadiliko hayo kwa kufanya uwekezaji mkubwa katika ujenzi wa Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere litakalozalisha megawati 2,115.

Alisema kwa sasa Tanzania inatumia dola za Marekani milioni 500 kila mwaka kwa ajili ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi ikiwamo kupanda miti milioni 276 katika halmashauri 184 zilizoko nchini.

Aliagiza mkutano huo wahakikishe wanatafuta jinsi ya kupata fedha hizo ili nchi iweze kupambana na mabadiliko hayo.

Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Omary Shajack, alisema warsha hiyo itawasaidia kutafuta mbinu mbalimbali za kupata fedha kwa ajili ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi ambayo kwa sasa yanasababisha uhaba wa mvua na kuleta athari kubwa kwa jamii, ikiwamo mmomonyoko wa ardhi kwenye fukwe za bahari.

Katika mkutano huo Mwakilishi wa Benki ya Dunia (WB), Nicholas Soikan, alisema benki hiyo imewakutanisha wadau hao ili kuwa na kauli moja itakayowezesha Tanzania kupata fedha zaidi katika mkutano wa kimataifa wa mazingira utakaofanyika nchini Misri Novemba mwaka huu.

Mkurugenzi wa Mazingira kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, Dk. Andrew Komba alisisitiza kuwa Zanzibar na Tanzania Bara, ni lazima serikali itafute njia za kuongeza fedha za kupambana na mabadiliko ya tabianchi ili waweze kukabiliana na athari zake.



# Mabadiliko tabianchi yaathiri ukuaji kahawa

**Na Mary Mosha,** MOSHI

TAASISI ya Utafiti wa Kahawa nchini (TaCRI) imesema kahawa katika baadhi ya mikoa imeathirika kwa kiwango kikubwa baada ya mibuni kushindwa kutoa maua na mbegu kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

Hayo yamo katika taarifa ya Mkurugenzi Mkuu wa TaCRI, Dk. Deusdedit Kilambo, aliyoitoa mwishoni mwa wiki wakati wa ufunguzi wa tamasha la kahawa lililofanyika katika Manispaa ya Moshi.

"Kutonyesha kwa mvua ya kutosha katika msimu wa masika mwanzoni mwa mwaka huu ni moja ya sababu kuu. Hii ni kwa sababu mvua ilinyesha chini ya kiwango kinachohitajika katika uzalishaji wa kahawa," alisema.

**Pamoja na upungufu huo wa mvua, zao hilo limekosa ustawi na hivyo kuchangia kuzorota kwa kilimo hicho.**

Dk. Kilambo alisema pamoja na upungufu huo wa mvua, zao hilo limekosa ustawi na hivyo kuchangia kuzorota kwa kilimo hicho.

Kutokana na hali hiyo, alisema TaCRI imeendelea kufanya utafiti kuhusu mbegu bora inayostahimili ukame pamoja na magonjwa ili kutoa tumaini jipya kwa wakulima nchini.

"Tunachofanya TaCRI hivi sasa ni kuwafundisha wakulima namna ya kuhifadhi unyevu katika udongo kwa kutandaza majani katika mashina ya mibuni ili ikue kama inavyohitajika," alisisitiza.

Mkurugenzi huyo alisema TaCRI inatarajia kuwasilisha aina hiyo mbegu katika Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSC) iliyoko mkoani Morogoro ili kuithibitisha na baadaye itawasilishwa Wizara ya Kilimo kwa ajili ya kutangazwa.

"Tayari tumefanya utafiti wa mbegu hiyo katika Wilaya za Rombo, Tarime, Buhigwe, Kigoma na Mbozi ili baadaye watu wa TOSC watazihakiki kisha zizalishwe kwa wingi na kugawiwa kwa wakulima," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya TaCri, Yahaya Morisa alisema kutokana na mabadiliko ya tabianchi ni lazima watafiti waje na mbegu mpya itakayosaidia kukabiliana na mazingira.




Wanafunzi wa Shule ya Saeronam ya nchini Korea wakishiriki kazi za kijamii ikiwamo kuchimba msingi wa ujenzi wa kituo cha kusaidia watoto na vijana wanaotoka kwenye mazingira magumu katika kijiji cha Shirinjoro Wilaya ya Moshi Vijijni mkoani Kilimanjaro jana, kituo hicho kinajengwa kwa ufadhili wa Shirika la Compassion International Tanzania. **PICHA: ASRAJI MVUNGI**

# ...Mkuu wa Mkoa aagiza utafiti kubaini sababu kahawa kudumaa

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, ameagiza kufanyika haraka kwa utafiti wa kina wa udongo, mbegu, dawa na pembejeo kama zinawafikia wakulima wa kahawa kwa wakati ili kubaini sababu zinazodidimiza ustawi wa zao hilo nchini kwa sasa.

Alitoa agizo hilo juzi wakati wa tamasha la kahawa liliiloandaliwa na Bodi ya Kahawa nchini (TCB).

"Kwa kuwa zao la kahawa ndiyo muhimili wa uchumi wa mkoa wetu na taifa kwa ujumla, ninaelekeza kufanyike utafiti huo.

"Yamo matatizo mengine, ikiwamo mabadiliko ya tabianchi yanasababisha kuchelewa kwa mvua, ukame, magonjwa na wadudu waharibifu wa zao hilo," aliagiza.

Awali Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Abbas Kayanda alisema zao hilo linahitaji jitihada za makusudi katika kufanya utafiti kuhusu udongo, mbegu, dawa na upatikanaji wa pembejeo za uhakika.

Alisema kahawa ni moja ya mazao makuu ya asili, ikichangia wastani wa asilimia tano ya thamani ya mauzo ya bidhaa zinazouzwa nje ya nchi, lakini linachangia asilimia 24 ya thamani ya mauzo ya mazao ya asili.

Kayanda alitia wito kwa wadau hao vikiwamo vyama vya ushirika, TCB, watafiti, halmashauri za wilaya zinazolima kahawa, Benki ya Ushirika (KCBL), kutoa mapendekezo kwa serikali namna ya kuondoa matatizo yanayobainika ili kupatiwa ufumbuzi wa kudumu.

Kaimu Mkurugenzi wa TCB, Primius Kimario alisema mpaka sasa kiwanda cha kukoboa kahawa cha TCCCo kina miaka 102 na kinazalisha chini ya kiwango.

"Kiwanda kilijengwa mwaka 1920, awamu ya kwanza kikiwa kinakoboa tani 500, wadau kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, tunajadili mbinu sahihi ili kurejesha uwezo halisi wa kiwanda hiki," alisema

Aliongeza kuwa wadau wanatumia maadhimisho hayo, kujiwekea malengo ya kuzalisha tani 300,000 za kahawa, kwa kuwa kwa sasa uzalishaji ni tani 3,000.

# Wakazi Kilimanjaro wapewa hadhari uuzaji akiba ya chakula

**Na Godfrey Mushi,** HAI

KATIBU Tawala wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Upendo Wella, amewasihi wakazi wa wilaya hiyo, wasiuze chakula cha akiba walichoanacho kwa sasa ili kuepukana na adha ya mfumuko wa bei na uhitaji wa chakula cha msaada.

Badala yake, ameelekeza kila kaya kutunza akiba ya chakula kilichoko kwa kuwa kwa namna hali inavyoendelea, huenda isiwe nzuri baadaye.

Wella alitahadharisha hayo juzi alipozungumza na wananchi wa Kata ya Weruweru wakati wa maadhimisho ya Juma la Elimu ya Watu Wazima.

"Juzi tulikuwa na wataalamu wa Wizara ya Kilimo ambao wamekuja kufanya tathmini ya hali ya chakula katika Wilaya yetu ya Hai, kuona uhalisia na kuwa na taarifa sahihi.

"Lengo ni kwamba ili kupeleka taarifa sahihi serikalini kuna mambo wanaangalia kwamba hali ikoje,ili mwisho wa siku ikifika tunauhitaji wa msaada wajue ni kwa kiwango gani.

Kutokana na tathmini kufanyika, zaidi Wella aliongeza: "Ninaomba tutunze chakula. Mwaka huu kama mnavyofahamu hali siyo nzuri, kwa sababu mvua hazikunyesha za kutosha hususani katika ukanda wa chini wa Wilaya ya Hai. Watu wengi hawakuweza kuvuna mazao kama ilivyotarajiwa.

"Mmeona hata TMA (Mamlaka ya Hali ya Hewa) wametuambia kwamba mvua za vuli zitanyesha lakini kwa kiwango cha chini. Kwa mkulima kuuza mazao yake sasa yeye anaona hiyo ndiyo tija kwake, kwa sababu ya soko.

"Rai yangu kwenu tusiuze chakula chote tukaja kutana na mfumuko wa bei na uhitaji wa msaada wa chakula."

**Lengo ni kwamba ili kupeleka taarifa sahihi serikalini kuna mambo wanaangalia kwamba hali ikoje,ili mwisho wa siku ikifika tunauhitaji wa msaada wajue ni kwa kiwango gani.**

Nipashe
# TESA
Jumanne • Oktoba 4, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

## Ukisikia 'baioteknolojia' yanatajwa mambo haya



Ukurasa 17




Ukurasa 16

## Hakuna mikopo bila kufunzwa ujasiriamali kufahamu ulipo, unachofanya na uendelevu

SAYANSI
**NA GAUDENSIA MNGUMI**

### EBOLA INATISHA, YA MUHIMU KUZINGATIA:

# Nawa mikono kama ilivyokuwa kwa corona

- Kuwahi hospitali usisubiri mpaka kutokwa damu
- Angalizo viko virusi aina tano, havina chanjo, tiba

HEH HEH, Ebola tena! Ndivyo watu wanavyoweza kusema wakisikia habari za ugonjwa hatari ambao sasa unatishia maisha kwenye nchi jirani ya Uganda baada ya kuripotiwa kwa wiki mbili sasa.

Itakumbukwa kuwa jina ebola ni mto ulioko Congo DRC, hivyo ugonjwa huo umepewa jina hilo kutokana na kuripotiwa kwenye kijiji jirani kilicho karibu na Mto Ebola.

Wakati Uganda ni hofu tupu, mlipuko wa ebola uliotangazwa DRC kuanzia Agosti mwaka huu umetokomezwa, linatangazwa Shirika la Afya la Umoja wa Mataifa (WHO) iliyokuwa inakabiliana na kirusi cha aina ya ebola Zaire chenye chanjo na tiba, lakini kilichoibuka nchi jirani ya Uganda ni virusi Sudan ambavyo havina chanjo wala tiba, vilivyoibuka wiki mbili sasa na kuua watu takribani 25 akiwamo daktari Mtanzania Mohammed Ali Hafidh.



Wataalamu waliojikinga kwa ajili ya kuikabili ebola. **PICHA: MTANDAO**

**AINA ZA VIRUSI**

Hadi sasa ebola ina aina tofauti za virusi vinavyotajwa kuwa ni Zaire ebolavirus vilivyobainika huko Congo DRC, vingine ni virusi vya Bundibugyo (BDBV) vilivyogunduliwa nchini Uganda na Reston (RESTV) kilichoripotiwa Marekani kati ya mwaka 1989 na 1990 vikiibuka kutoka kwenye jamii ya kima (macaques) walioingizwa Marekani wakitokea nchini Philippines kwa ajili ya utafiti wa kimaabara.

Virusi vingine ni Sudan ebolavirus (SUDV) ambacho mara ya kwanza kiliripotiwa Sudan Kusini Juni 1976 na virusi vya ebola vya msitu wa Taï pia vinajulikana kama virusi vya ebola vya Cote d'Ivoire vilivyogundulika kwa mara ya kwanza mwaka 1976 nchini Guinea, WHO inasema.

Aidha, mlipuko wa 2014 hadi 2016 huko Afrika Magharibi ulikuwa mkubwa zaidi tangu kugunduliwa kwa virusi kwa mara ya kwanza mwaka 1976, ukianzia Guinea na kisha kuvuka mipaka ya ardhi hadi Sierra Leone na Liberia.

Juhudi za kutafuta chanjo zinaendelea lakini hadi sasa virusi vyenye chanjo ya uhakika ni Zaireebola yenye majina kadhaa mojawapo ni V920 au rVSV-ZEBOV, iliyoanza kutolewa mwaka 2018, kadhalika kirusi cha Ebola Cote d'Ivoire kinatumia chanjo hiyo ambayo inaelekea kuwa na mafanikio.

**MAAMBUKIZO**

Ebola si kama COVID-19 au UVIKO -19 inayosambaa kwa njia ya hewa bali maambukizo ni kutoka virusi vya wanyama vinavyoingia kwa watu kutoka kwa wanyama wa porini kama swala -'duiker' popo, kima, nyani na hata gorilla.

Wataalamu wanaeleza kuwa uambukizo unaanzia kwa virusi vya ebola kuingia kwa binadamu kutokana na kumgusa mnyama au nyama ya kiumbe huyo mgonjwa.

Inawezekana pia kuenea na kuambukiza idadi kubwa ya watu kupitia kumgusa mnyama au kula nyama, virusi huingia mwilini kupitia michubuko na majeraha kwenye ngozi ya binadamu, kugusa damu au maji maji yanayotoka kwenye mwili wa mgonjwa au mnyama lakini kujamiiana nako ni chanjo cha maambukizo.

Virusi huenea kwa kugusana moja kwa moja ngozi au utando laini wa machoni, puani au mdomoni, kwa hiyo inaelezwa kuwa udhibiti wa ebola ni karibu

INAENDELEA UK. 18

ELIMU

NA SAID MUHIBU, SAUT

# Ufadhili wa masomo elimu ya juu, wa mahitaji maalumu wafikiriwe

SERIKALI imeonyesha nia njema na ubunifu wa kuboresha sekta ya elimu nchini, kwa kutoa ufadhili wa masomo ya elimu ya juu kwa wanafunzi waliohitimu kidato cha sita mchepuo wa sayansi na kupata ufaulu mkubwa.

Takribani Shilingi bilioni tatu zimetengwa kwa wanafunzi 640 kupata ufadhili wa asilimia 100 kwenye masomo ya elimu ya juu, huenda huo ukiwa ni mwarobaini utakaochagiza kukua kwa sekta ya elimu nchini na kuhamasisha wanafunzi kupenda kusoma sayansi, na kusaidia taifa kuwa na wasomi wengi wa fani mbalimbali.

Wengine wangedhani utaratibu uliotumika kutoa ufadhili huo ungeenda sawia na ule unaotumiwa kuomba mkopo wa elimu ya juu kwenye Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB).

Kama ambavyo inafahamika na inazingatiwa, moja ya kigezo kikuu kwa mwanafunzi wa elimu ya juu kupata mkopo ni uhitaji wake.

Mahitaji yanamaanisha mikopo inatolewa kufuatia uhitaji wa yule anayeomba ambao unafahamika kwa HESLB kupitia nyaraka muhimu atakazo ziambatanisha mwombaji wakati anaomba mkopo huo na bodi itabaini ikiwa mwombaji ana uhitaji ama hana kwa kupitia hizo nyaraka.

Hapa wengi miongoni mwa wahitaji ni wale wasiojiweza na wanaotokea kwenye familia maskini. Pengine hata ufadhili huo ungezitia utaratibu wa kuwakumbuka masikini wasiojiweza ambao wana uwezo mkubwa lakini uchumi, mazingira magumu utashi wa kijamii, vinawakwamisha kitaaluma.

Wapo wanaopambana na kujizatiti hadi kufikia mfuko wa uhisani wa masomo unaotolewa na Rais, lakini wapo baadhi wanaohitaji kuinuliwa au kushikwa mikono ili wasonge mbele, hao nao kama serikali inaweza kuwatazama pia.

Ikumbukwe Julai 29, mwaka huu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, akizungumza kwenye mkutano maalum wa kikazi unaohusisha wizara hiyo na wahariri wa vyombo vya habari, anatangaza kuwa ufadhili wa Samia Scholarships utatolewa kwa kigezo cha ufaulu mahiri, bila kujali mwanafunzi anatokea wapi au familia gani, ilimradi awe amefaulu kikamilifu masomo ya sayansi.

Ningeshauri kuwapo na utaratibu mwingine unaofanana na huo wa kuwakumbuka wale wenye mahitaji wa ufadhili lakini wana changamoto nyingi za kimahitaji hasa kuishi na ulemavu ambao unawafanya wasisonge mbele.

Kwa mfano, wapo wanafunzi wanaotokea kwenye familia za hali ya chini, wanasoma kwa taabu na misukosuko lakini wanafanya vizuri kwenye masomo yao pengine wangeinuliwa wangeweza kuwa 'supa', ndio sababu ya kufikiria 'Special Scholarship for the needy'.

Kama Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu inaweza kuwafikia na kuwapa mikopo wanafunzi wahitaji, basi Wizara ya Elimu kwa kushirikiana na HESLB wangeweza kuwafikia hawa wanafunzi wa hali ya chini waliofanya vizuri kwenye masomo ya sayansi licha ya kwamba wana ujuzi, wanajitihada lakini uduni wa maisha unawakwamisha.

Wanaweza kuwa na vikwazo vingi, pengine kukosa wazazi na walezi kunawarudisha nyuma, umbali wa kutoka nyumbani hadi shuleni, kukosa mahitaji kwa yatima ambao wanasoma, lakini wanajilea kwa sababu hawana msaada, na kama upo ni makazi labda wanaishi na babu au bibi.

Ninaamini wanafunzi waliofanya vizuri na wanatokea katika familia za hali ya chini wana nafasi ya ufadhili kupitia Samia Scholarship, lakini wanaweza kuhofia wapo wengi wenye uwezo na wanaweza kuwa mashujaa kielimu iwapo watasaidiwa kupitia mfuko maalumu wa wahitaji.



Wenye uhitaji kama huyu wakumbukwe kwenye ufadhili maalumu ili nao waifikie fursa ya kuwa wanasayansi bora. **PICHA: MTANDAO**

Lakini, hata wale ambao sasa hivi wako shuleni wanaweza kupitia mfuko huo wa uhisani kwa wenye ulemavu kusaidiwa ili kuwaondolea adha ya kuhangaika kulipa deni kubwa la serikali linalotokana na kupewa mkopo na elimu ya juu wanapohitimu elimu ya vyuo vikuu.

Kiuhalisia wanafunzi wanaotoka familia za hali ya chini wanapofanya vizuri kwenye masomo yao inaonyesha ni jinsi gani wanapambana kuondoa umaskini na dhiki za nyumbani kwao. Pamoja na kulipa fadhila za kusomeshwa na kodi za Watanzania wana jukumu kubwa la kuwaangalia walio nyuma yao ambao wanawaona kama ni mkombozi.

Katika hali hiyo watakuwa tayari kupambana kwa hali na mali pale watakapopewa ufadhili wa gharama za mafunzo, posho ya chakula na malazi, kulipiwa vitabu na viandikwa, mahitaji maalum ya vitivo, mafunzo kwa vitendo, utafiti na bima ya afya kwenye masomo ya elimu ya juu.

Wahitaji wengi wanaweza kufikiwa hata kwa maofisa wa ustawi na maendeleo ya jamii kuwatambua Watanzania hao ambao wapo sehemu mbalimbali vijijini na mijini na kuwainua kwa sababu wapo ambao wangefaulu lakini hawana vitabu, madaftari, peni wala chakula.

Kwa upande mwingine hawana visaidizi hasa wanaoishi na ulemavu mfano viti na magongo kwa wasiotembea, miwani kwa wenye uoni hafifu, miwani, vikuza herufi, mafuta maalumu na mavazi ya kujikinga na mionzi ya jua kwa wanaoishi na ualbino. Aidha, vitabu na machapisho mengine ya nukta nundu kwa wasioona.

Kuwaangalia kwa jicho la kipekee wenye ulemavu kwenye mfumo huo ni jambo jema kwa sababu wanahitaji pia kuinuliwa ili kuinuka na kufikia hatua za juu za kujiunga na vyuo vikuu kwa utaratibu wa uhisani wa Rais kwa wahitaji.

Wanafunzi wanaofanya vizuri wengi ni wale ambao wazazi na walezi wao wanawagharamia kielimu wapo wanaosoma hata nje ili kuwa 'supa' wapo pia wanaosomeshwa kwenye shule za msingi na sekondari zinazotoza ada kubwa hivyo ni lazima watafanya vizuri kwa hiyo huenda wale wenye 'maisha na familia bora' wakafaulu zaidi na kunufaika na Samia Scholarship kuliko wanafunzi ambao pengine wanatoka kwenye familia zenye maisha duni.

Yote hayo yaifikirishe Wizara ya Elimu na wadau na kupata majibu ya namna ambayo Watanzania wa ngazi zote wanaweza kunufaika na uhisani unaotolewa kwa uhisani wa 'special scholarships for the needy'.

ELIMU

NA SABATO KASIKA

# Waliokatishwa masomo kwa mimba wanapohoji waanzie wapi wasome

## • 50 wafunzwa kujitegemea, Ofisa Elimu awaelekeza...

LICHA ya serikali kuweka mipango ya kuwarejesha shuleni wasichana waliokatishwa masomo kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo mimba, inaelezwa kuwa wapo baadhi ya mabinti wanaotafuta fursa hiyo wanalalamika, hawajui pa kuanzia.

Wasichana wahusika wanadai kuwa wanasikia taarifa za utaratibu wa serikali wa Mpango wa Elimu Haina Mwisho, unaowarejesha madarasani waliokatishwa masomo kwa sababu mbalimbali lakini hawana taarifa inakuwaje, wanaanzi wapi, wanamwona nani, wanasoma wapi na makundi yepi yanayopewa nafasi katika sekondari au stadi za maisha.

Hayo yanabainishwa katika mafunzo kwa vitendo yenye lengo la kuwawezesha kiuchumi na pia elimu ya kujitambua, mabinti 50 kutoka kata 14 wilayani Serengeti mkoa wa Mara yakifanyika hivi karibuni mjini Mugumu.

Mabinti hao walikusanywa na shirika lisilo la kiserikali la Girls Education Support Initiatives (GESI), na kufunzwa na Kituo cha Sauti ya Jamii cha Kipunguni Dar es Salaam.

Ofisa Mradi wa GESI, Honoratha Patrick, anasema: “Wakati wa mafunzo tumebaini kuwa wapo baadhi ya mabinti walioathirika wanaotamani kuendelea na masomo, ili watimize ndoto zao, lakini hawajui waanzie wapi waweze kurudi shuleni.”

Anafafanua zaidi kuwa wasichana wamepata mafunzo hayo ili wajiajiri na kujisimamia na kwamba ni wale waliokwama kuendelea na masomo ya sekondari kuanzia mwaka 2018 hadi 2022.

Anaongeza kuwa wameamua kutoa mafunzo hayo, ili yawasaidie kujikimu kimaisha kwa kutumia ujuzi wanaopata ukiwamo wa kilimo cha mboga, utengenezaji wa mkaa mbadala kwa kutumia maboksi na sabuni za maji. Honoratha anasema hao wanatoka kata za Mugumu, Stendi Mpya, Getasamo, Ring'wani, Kenyamota, Machochwe, Nyamburreti, Kisaka, Nata, Majimoto, Isenye, Matare, Rung'abure na Maburi.

“Serengeti ina kata 30 lakini tumechukua kata hizo chache kwanza, na katika maeneo hayo tulichagua moja, kwingine wawili au watatu, lakini tunaamini kwamba wapo wengi ambao wanahitaji kusaidiwa, ili watimize ndoto zao,” anasema.

Anasema iwapo ndani ya kata 14 wamepatikana mabinti 50, inawezekana kwenye kata nyingine 16 zilizobaki, wanaweza kuwapo wengi zaidi wanaohitaji msaada, ukiwamo wa kurudi shule au mafunzo ya ujasiriamali.



Mkufunzi Seleman Bishagazi (katikati), akitoa mafunzo ya darasani.

“Tunafanya sehemu yetu kwa kuwapa mafunzo, na wapo wanaotaka kurudi shule kuendelea na masomo, lakini hawajui waanzie wapi, ili wapate nafasi hasa baada ya serikali kuruhusu waliopata mimba kurudi shule,” anasema.

Anafafanua kuwa baada ya mafunzo hayo yaliyofanyika kwa siku mbili, wamejiwekea utaratibu wa kuwatembelea mabinti hao kila baada ya miezi mitatu ili kuona jinsi wanavyotumia mafunzo kuendesha maisha.

“Lakini tutaendelea kuwasaidia, ili waweze kutimiza ndoto zao iwe ni kwa kurudi shule au kupitia mafunzo mbalimbali yanayotolewa na GESI,” anasema.

### CHA KUFANYA

Kuhusu mabinti wanaotamani kurudi shule kuendelea na masomo, Ofisa Elimu wa Wilaya ya Serengeti Antony Guzwile, anawataka wafike katika shule za sekondari za kata kwenye maeneo yao wapewe utaratibu.

“Hadi sasa kuna wanafunzi 19 waliorejea shuleni, wanasoma Serengeti Sekondari, hivyo na hao waende katika sekondari zilizo karibu nao, ili wapewe maelekezo ya jinsi ya kurudi shule,” anasema Guzwile.

Ofisa huyo anafafanua kuwa utaratibu uliowekwa na serikali, ni wanafunzi wa chini ya miaka 24 ndio wanaotakiwa kurudi shuleni kuendelea na masomo wakiwa chini ya walimu wao maalum.

Aidha, anawataka wazazi, walezi na jamii kwa ujumla kusimamia maadili ili kupunguza tatizo la mimba za utotoni, ambalo limekuwa likisababisha wanafunzi kushindwa kutimiza ndoto zao walizojiwekea kwenye elimu.

Guzwile anasema wilaya hiyo imekuwa ikikabiliwa na tatizo la ukeketaji unasababisha watoto wa kike kukatishwa masomo na kuingizwa kwenye ndoa na pia kuwapo kwa mimba za utotoni.

“Ninaamini kwamba wazazi, walezi na jamii kwa ujumla ikiachana na mila potufu na kusimamia maadili mema, watoto wengi wa kike watasoma na hatimaye kutimiza ndoto waliozojiwekea kwenye elimu,” anasema.

### NI UKATILI KIJINSIA

Mkufunzi wa mafunzo hayo, Seleman Biashangazi, kutoka Kituo cha Sauti ya Jamii cha Kipunguni, anasema kumpa mimba mwanafunzi hata kama wamekubaliana ni ukatili huo, kwa kuwa mwisho wake ni kusababisha akatishe masomo.

Anaongeza kuwa mbali na kuwafundisha ujuzi mbalimbali ukiwamo wa kilimo rahisi cha mboga, kutengeneza sabuni za maji, mkaa mbadala wa kutumia maboksi, wamefundishwa pia jinsi ya kutambua viashiria vya ukatili.

“Nimewaelekeza pia sehemu ya kutoa taarifa, ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya wale wanaowafanyia ukatili huo. Wapotongozwa wanatakiwa kutoa taarifa nyumbani, serikali ya kijiji na hata polisi,” anasema Bishagazi.

Mkufunzi huyo anasema mafunzo hayo yanahitaji kote nchini, kwa kuwa baadhi ya jamii, inawaona mabinti kama hawana thamani, na hunyimwa mahitaji muhimu na kusababisha warubuniwe na kuingia katika vishawishi.

“Lakini nimewakumbusha kuwa kushindwa shule si kukwama maisha, hivyo wanatakiwa kuzingatia mafunzo waliopata, ili yaweze kuwasaidia katika maisha yao kwa njia ya kilimo au kutengeneza bidhaa na kuuza,” anasema.

Bishagazi anasema mabinti wakipata mbinu sahihi za kujipatia kipato, hatua hiyo itawapunguzia uwezekano wa kupata mimba ambazo anadai kuwa wakati mwingine zinasababishwa na kurubuniwa kwa fedha.

### NDOTO KATIKA ELIMU

Mmoja wa mabinti hao 'Maria John', sio jina lake halisi, anasema alitamani kuwa mwalimu, lakini amekwama baada ya kukatisha masomo mwaka jana akiwa kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Magena.

“Nilipata ujauzito nikafukuzwa shule, nikajifungua Machi mwaka huu, lakini aliyenipa mimba amekimbia, hajulikani alipo baada ya mama kumwambia kuwa anamfikisha kwenye vyombo vya dola,” anasema Maria.

Anafafanua kuwa alirubuniwa kwa fedha na huyo aliyempa mimba kutokana na kwamba wazazi wake hawana uwezo kiuchumi, ambapo alijikuta akiingia kwenye mtego kirahisi na kuharibiwa ndoto zake.

“Nikipata nafasi ya kusoma, niko tayari kuendelea na masomo eneo lingine na sio huku kwetu Kata ya Majimoto, bali ningependa kupelekwa kata nyingine yoyote ya hapa wilayani kwetu Serengeti,” anasema.

Binti huyo anasema kwa sasa akili imekomaa na pia ameongezewa elimu ya kujitambua katika mafunzo yaliyotolewa na GESI, na kwamba hawezi kurubuniwa tena, badala yake ataelekeza akili kwenye elimu.



Mabinti wakijifunza kutengeneza mkaa mbadala baada ya mafunzo ya darasani. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Mkopo wa umma: Sharti darasa ujasiriamali, kufahamu ulipo, unachofanya, iwe uendelevu




Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko (katikati), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 156.4 kwa vikundi 11 vya ujasiriamali vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. **PICHA: MARCO MADUHU**

UTOAJI mikopo ya halmashauri bila kufuatilia miradi ya vikundi vinavyokopeshwa umepata dawa baada ya serikali kuwapa mitihani ya majiribio wanaokopa ili kujua umahiri na uendelevu wa mradi unaofikishwa kwenye dawati la mkopo.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, Jomaary Satura, anapozungumza na Nipashe anasema mikopo yao haina riba na wanaitoa kwenye vikundi ambavyo miradi yao inaonekana kuwa na tija na ni endelevu.

Anasema: "Zamani tulikuwa tukitoa mikopo bila kufuatilia miradi ya vikundi hivyo na baadhi vilikuwa vikizitumia fedha hizo ovyo na kushindwa kuwakwamua kiuchumi na hata vikundi vyao kusambaratika na manispaa kupoteza mapato yake."

Ukosefu wa mitaji kwa wananchi kujishughulisha na shughuli mbalimbali za ujasiriamali na kujikwamua kiuchumi ilikuwa ni tatizo kubwa, lakini serikali ikaja na mkakati wa kutoa mikopo fedha za halmashauri asilimia 10 kupitia mapato ya ndani.

Fedha hizo za mikopo asilimia 10, asilimia nne hutolewa kwa wanawake na vijana, huku asilimia mbili hupewa watu wenye ulemavu, lengo likiwa ni kuwawezesha mitaji na kufanya shughuli za kujikwamua kiuchumi.

Anaeleza kuwa mbali na kutoa mikopo wamenunua shamba la uwezeshaji vikundi kiuchumi lenye hekari saba lililoko Lubaga kwenye manispaa hiyo ambalo hutumiwa na vikundi kufanya shughuli zao za kilimo cha umwagiliaji ili kuwaingizia vipato.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii Manispaa ya Shinyanga, John Tesha, anaelezea zaidi kuhusu shamba hilo la uwezeshaji vikundi kiuchumi, akisema kuwa wanakikundi wakija na mawazo ya kufanya shughuli za kilimo, hupewa eneo kwenye shamba hilo bure na kufanya shughuli zao za kilimo cha umwagiliaji ndani ya miaka mitatu ili kupima ufanisi na uendelevu.

Anasema baada ya miaka hiyo mitatu watakuwa tayari wameshaimarika na kupisha eneo hilo na kuwaachia wengine, ili walitumie na kujikwamua kiuchumi kupitia kilimo cha umwagiliaji.

Aidha, anasema halmashauri hiyo kabla ya kutoa mikopo kwa vikundi hivyo vya ujasiriamali, huvitembelea kwanza na kuwapatia elimu ya usimamizi wa fedha, pamoja na kuwashauri juu ya kuanzisha miradi yenye tija ambayo inaendana na soko.

"Tunatoa fedha nyingi sana za mikopo asilimia 10 kwa ajili ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Tangu mwaka 2015 hadi sasa 2022 tumeshatoa Shilingi bilioni 1.4 kwa vikundi 170," anasema Tesha.

Awali Mkurugenzi, Jomaary Satura, anasema kuwa zamani fedha zilizotolewa zilikuwa chache lakini sasa wenye mawazo mazuri na shughuli zao kuonekana zina tija, wanatoa mkopo hadi Shilingi milioni 80 mpaka 100.

Katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 ulioisha Juni 30 Shilingi milioni 379 zilitolewa kwa vikundi 21 na Septemba 27 mwaka huu milioni 156.4 zimetolewa kwa vikundi 11, kwa mujibu wa Tesha.

> "Tunatoa fedha nyingi sana za mikopo asilimia 10 kwa ajili ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Tangu mwaka 2015 hadi sasa 2022 tumeshatoa Shilingi bilioni 1.4 kwa vikundi 170," anasema Tesha.

Meya wa Manispaa ya Shinyanga, Elias Masumbuko, anawaagiza maofisa maendeleo ya jamii halmashauri hiyo kuanzia ngazi za kata, kuhakikisha kuwa vikundi vyote ambavyo vimepewa mikopo wanavitembelea mara kwa mara, ili kuona maendeleo na kuvipatia ushauri ili visije kukwama na serikali kupata hasara.

"Maofisa Maendeleo mkivitembelea vikundi hivi mara kwa mara vitaendelea kufanya vizuri katika shughuli zao na kujikwamua kiuchumi, lakini mkivitelekeza havitawezi kukua mwisho wa siku mtasikia vimesambaratika," anaonya Masumbuko.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, anatoa wito kwa vikundi ambavyo vimepewa mikopo ya asilimia 10 na halmashauri kuwa fedha hizo wazitumie kwa madhumuni yaliyokusudiwa ili wajikwamue kiuchumi.

Anasema serikali inatoa fedha hizo za mikopo bila riba ili kuwanyanyua wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa vile makundi hayo yamezoeleka kuwa tegemezi na waondokane na dhana hiyo na kufanya shughuli za kuwaingizia kipato.

"Wanawake wa Shinyanga changamkieni fursa hii ya mikopo ya halmashauri asilimia 10, siku hizi hakuna mwanamama ambaye anapenda kukaa nyumbani bila kazi na kusubiri kuletewa na mwanaume na wakati mikopo ipo tena haina riba,"anasema Mboneko.

Anavisihi vikundi hivyo kuwa pale wanapokumbana na mkwamo wasisite kuwasiliana na Maofisa Maendeleo ya Jamii, ili kuwatatulia shida hizo na kuendeleza shughuli zao.

Aidha, anavitaka vikundi kujenga pia utamaduni wa kurejesha marejesho yao kwa wakati, ili vikundi vingine vipate mikopo na kuwaonya watakao zichezea fedha hizo watawachukulia hatua.

"Safari hii hatutaki mchezo kwenye marejesho, mkipata mkopo rudisha fedha ili watu wengine wakope, tayari kuna watu walikuwa wanafanya mchezo kwenye fedha hizi waulizeni kilichowakuta mtaishia gerezani,"anaongeza Mboneko.

Diwani wa Kitangili Manispaa ya Shinyanga, Mariam Nyangaka, anaipongeza juhudi za kuendelea kutoa fedha nyingi za mikopo asilimia 10 kwa vikundi vya ujasiriamali, ambayo imewainua wanawake wengi kiuchumi.

"Vikundi ambavyo mmepewa mikopo hii tumieni fursa vizuri kwa kufanya kazi kwa bidii ili muinuke kiuchumi,"anasema Nyangaka.

Asha Kahama ni mwenyekiti wa kikundi cha Amani ambao wanajihusisha na utengenezaji wa sabuni za mabaki ya makapi ya mafuta ya pamba, anasema wameanza shughuli hiyo mwaka 2017 kwa kupata mkopo wa Shilingi milioni 20 na sasa maisha yao yamebadilika kiuchumi.

Anasema awali kabla ya kujiunga kwenye kikundi hicho, alikuwa tegemezi kwa mumewe, lakini sasa hivi anajimudu na anaendesha maisha yake vizuri na kusomesha watoto wao.

Mwenyekiti wa kikundi cha Uamsho, Rosemary Masanja kinachojihusisha na kilimo cha umwagiliaji mboga katika shamba la uwezeshaji vikundi kiuchumi, anasema wako wanachama sita walipata mkopo wa halmashauri Shilingi milioni 4.3.

Anasema kwa sasa hali ya maisha yao ni nzuri siyo kama zamani, kabla ya kuanza shughuli hiyo ya kilimo cha umwagiliaji ambapo wanapata pesa na kuendesha maisha yao.

Daudi Nyahiti anaishi na ulemavu ambaye naye ni mnufaika wa mikopo ya halmashauri asilimia mbili katika kikundi chao wamepata Shilingi milioni 18 mwaka huu, anasema wanalenga kununua bajaji na wataziendesha wenyewe ili kuwainua kiuchumi na kulipa mkopo.

Anasema anapongeza juhudi za serikali kwa kuendelea kutoa pesa hizo za mikopo za halmashauri kwa asilimia 10, ambazo zimekuwa msaada mkubwa kwa watu wa hali ya chini na kuwainua kiuchumi.

ELIMU

NA GAUDENSIA MNGUMI

# Ukisikia 'baioteknolojia' yanatajwa mambo haya

- Mbegu bora, himilivu, kulima eneo dogo, mavuno tele
- Chanjo, kupanda figo, ini, tiba za saratani, sukari
- Ni hatari, chanzo silaha maangamizi ya 'wadudu'



Nyanya zilizoboreshwa na 'baiotek' (kushoto) dhidi ya mbovu zinazosumbuliwa na ugonjwa. **PICHA: MTANDAO**

PENGINE watu wengi wamesikia neno 'bio technology' au 'baioteknolojia' hata kufupishwa ikasomeka 'baioteki' na wakajiuliza hiki ni kitu gani?

Jibu linaweza kuwa huu ni utaalamu unaotegemea au kutumia baiolojia au viumbe hai kujifunza na kuunganisha michakato mingi ndani ya viumbe hao ambao ni wanyama na mimea kuwafahamu kwa kina na kuendeleza juhudi za kuboresha maisha, afya, uchumi na mazingira ya watu na dunia.

Ni teknolojia inayotumia michakato ya kibaiolojia hasa seli, nasaba au DNA na jeni (genes) kuanzia kwenye wadudu, wanyama, mimea na binadamu.

Neno baioteknolojia lilitumiwa kwa mara ya kwanza na mhandisi Karl Erkey wa Hangari mwaka 1919. Lakini haukuwa mwanzo wa baioteki. Baadaye baioteki ilifafanuliwa na wanasayansi tofauti, kulingana na mazingira na ukaelezwa kuwa ni "utumiaji wa kanuni za kihandisi na sayansi ya baiolojia kuunda bidhaa mpya kutokana na vitu kwa uasili wake kwa mfano, dawa za chanjo, kichocheo cha insulin kutibu tatizo la kisukari.

Au kwa maneno mengine inaweza pia kufafanuliwa kama ni matumizi ya viumbe hai au bidhaa zake kurekebisha au kuboresha afya ya binadamu na mazingira yake. Na matumizi yake yalipata msukumo zaidi miaka ya 1970.

Kwa mfano wanasayansi wametumia vijidudu kwa miaka mingi na wamezalisha bidhaa muhimu za chakula, kama vile hamira inayotengeneza mkate na mbinu za kuhifadhi vyakula yakiwamo maziwa.

Kwa kutumia michakato ya seli na kibaiolojia, wanasayansi wanaweza kufanya maendeleo na kukabiliana na changamoto nyingi katika nyanja mbalimbali kuanzia tiba, viwanda, kilimo, nishati na elimu.

Michakato yake inajumuisha viumbe hai katika hali ya asili na mambo yanayofanyika ni kuzalisha viumbe hai vipya, kurekebisha muundo wao wa kijeni (genetically modified) na kuboresha changamoto na udhaifu unaovikabili lakini kutumia bidhaa zake na kuboresha maeneo mengine ya maisha.

Baioteki imesaidia kuponya na kutibu dunia kwa kutumia 'zana za asili' na kutumia muundo wa binadamu kuanzia seli na kijeni (genes) zake kupata tiba za magonjwa hata kuyapunguza na kufanya utafiti wa kila aina kukabili changamoto za kiafya. Hivi sasa, kuna zaidi ya bidhaa 250 kuanzia dawa na huduma za kibaioteknolojia hata chanjo zinazopatikana kwa wagonjwa, wengi hasa kwa matibabu ambayo hapo awali yalikuwa hayatibiki mfano saratani, maradhi yanayotokana na virusi kama COVID-19 na ebola hata chanjo pia.

> "Kwa kutumia michakato ya seli na kibaiolojia, wanasayansi wanaweza kufanya maendeleo na kukabiliana na changamoto nyingi katika nyanja mbalimbali kuanzia tiba, viwanda, kilimo, nishati na elimu.

**KWENYE KILIMO**

Baioteki huboresha uzalishaji kwa kuandaa mbegu za kisasa zenye ukinzani wa wadudu wa mazao kwa mfano kupunguza uwezekano wa mahindi kubunguliwa, nyanya kushambuliwa na fangasi na pia mazao kuoza ovyo mashambani.

Aidha, inafanikisha kuongeza ustahimilivu na kupunguza dawa za mimea za viwandani na kuwezesha kutumia mbinu za kilimo endelevu zaidi zinazolinda mazingira kama kuzalisha katika eneo dogo na kupata mazao mengi badala ya kukata misitu na kulima mamilioni ya hekari huku misitu ikiteketea.

Kwa kutumia baioteki wakulima wamewezeshwa kuzalisha mazao mengi aidha, pembejeo chache kama mbolea, maji, viuatilifu kwa sababu mbegu zinaimarishwa zaidi na kuwa na ukinzani na mashambulizi hasa ya wadudu.

Kupitia utaalamu huo kilimo pia kinapunguza kiasi cha kemikali zinazohitajika na mazao na mazingira huku mkazo ukiwekwa kwenye kutumia vitu asilia kama mbolea za mboji, mimea yenye viuadudu kama utupa ili kulinda afya za wakulima, walaji na mazingira.

Aidha, ni ufunguo unaowezesha kutumia mazao ya kibaioteki ambayo yanahitaji matumizi machache ya pembejeo na wakulima kupunguza kulima mashamba na kilimo kinaweza kulifanyika hata ndani ya maji kwa mfano 'hydroponic'

teknolojia hii iko mezani kwa kuleta chakula bora kwani pamoja na kukuza kilimo cha mazao yenye sifa za kuimarisha lishe huzalisha chakula bora zaidi chenye virutubisho vingi, hukabili upungufu wa vitamini na virutubisho mwilini vinavyosababisha udhoofu na udumavu na maradhi.

Utaalamu huo umezalisha vyakula visivyo na 'aleji' au mzio na sumu kama vile sumu kuvu 'aflatoxins'na pia kutafiti na kugundua chakula na mafuta kutoka kwenye mazao mbalimbali ili kusaidia kuboresha afya hasa mishipa ya moyo na ya fahamu.

**AINA ZA BAIOTEKI**

Bioteki nyekundu au 'red biotech' inahusisha michakato ya kimatibabu kama vile kupata viumbe vya kuzalisha dawa mpya na kutumia seli za shina au seli mama (stem cells) kuzalisha upya tishu zilizoharibika za binadamu au hata kukuza upya viungo vyote.

Kwa mfano kutumia kipande cha ini kuzalisha na kupandikiza ini jipya, kadhalika kuotesha au kupanda upya uroto ndani ya mifupa ya binadamu kukabiliana na saratani ya damu.

Aidha, katika sekta ya dawa hutumia baioteki kupata tiba ya magonjwa, kuelewa baiolojia ya seli za binadamu na nasaba -DNA, kutengeneza chanjo na kuzalisha viuavijasumu 'antibitics' kudhibiti.

Ya pili ni 'baioteknolojia nyeupe' au kijivu' inahusisha michakato ya viwandani kama vile kutengeneza kemikali mpya au uundaji wa mafuta mapya ya magari na kupunguza sumu na uharibifu wa mazingira na afya ya binadamu..

Nyingine ni baioteknolojia ya kijani inatumika kwenye michakato ya kilimo kama vile kuzalisha mazao yanayostahimili ukame, kutumia maji kidogo, yasiyoshambuliwa na wadudu hata wanyama wanaostahimili magonjwa na kuchangia kupata maendeleo rafiki kwa mazingira.

Baioteknolojia ya bluu inajumuisha michakato katika mazingira ya baharini na majini, kama vile kudhibiti kuenea kwa viumbe hatari vinavyosambazwa na maji.

Utaalamu wa uongezaji wa virutubishi unaweza kuhusisha teknolojia ya kibaioteki kwani baadhi ya vyakula huongezewa virutubishi, vitamini, na madini vitu vinavyohitajika ili kusaidia katika kupanga chakula, lishe bora na kula kimatibabu.

Kadhalika iko baioteknolojia ya manjano inarejelea michakato inayosaidia uzalishaji wa chakula, kuvihifadhi na matumizi ya vitu hai zaidi kwenye kuchachusha mfano kusindika pombe, mvinyo, kutumia hamira kuchachusha mikate na kuhifadhi bidhaa za chakula ili zitumike kwa muda mrefu

baioteknolojia ya 'gizani' inaimarisha uwezo wa kutumia teknolojia ya kibaioteki kwa silaha hatarishi za maangamizi zinazotumia wadudu kama kimeta na virusi na utaalamu mwingine unaotishia usalama na amani.

Mifano ya silaha za kibaiolojia ni pamoja na yenye vimelea vya aflatoxin, kimeta, sumu ya botulinum, ugonjwa wa mguu na mdomo kwa wanyama na tauni.

***MITANDAO***

### EBOLA INATISHA, YA MUHIMU KUZINGATIA:

# Nawa mikono kama ilivyokuwa kwa corona

INATOKA UK. 13

sawa na wa UVIKO-19 usishike maeneo hayo kama hujanawa mikono na ikibidi kuna mlipuko vaa barakoa inayofunika kinywa, midomo na hata masikio.

Jiepushe kugusa damu au maji maji ya mwili kama mkojo, mate, jasho, kinyesi, matapishi, maziwa ya mama anayenyonyesha, maji maji ya uzazu na manii. Hata kwa mtu aliyekufa kutokana na ugonjwa wa virusi vya ebola usiguse.

Ogopa pia vitu kama mavazi, magodoro, shuka vilivyotumiwa na mwenye ebola au vilifunikia mwili wa mgonjwa aliyefariki kutokana na virusi vya ugonjwa huo.

Manii au mbegu za kiume kutoka kwa mwanamume aliyepona kutokana na ebola zinaweza kusambaza maradhi hayo kwa njia ya kujamiiana, iwe ngono ya mdomo, mke na mume au jinsia tofauti. Virusi vinaweza kubaki kwenye umajimaji fulani wa mwili hata kama mgonjwa amepona kutokana au hana dalili mbaya au hatarishi za maradhi hayo.



Wataalamu wakitoa chanjo ya Ebola nchini Congo DRC. **PICHA:WHO**

**ANGALIZO**

Hakuna ushahidi iwapo mbu au wadudu wengine wanaong'ata wanaweza kusambaza virusi. Zaidi ya hayo, virusi vya ebola havijulikani kama vinaweza kusambazwa kupitia chakula yaani kula pamoja na mgonjwa. Hata hivyo, kama vinaenea kwa kushika na kula nyama ya wanyamapori au wanyama waliowindwa walioambukizwa huenda hata kula pamoja kunasambaza kirusi hicho.

**VIASHIRI HATARI**

Dalili kuu na hatarishi ni kutokwa na damu bila sababu midomoni, puani, masikioni, machoni na sehemu nyingine zenye matundu mwilini lakini hata kwenye michubuko.

Kabla ya kujitokeza kwa hali hiyo inayotishia zipo dalili nyingine nyingi zinazoweza kuanza kuonekana kuanzia siku mbili hadi 21 baada ya mtu kupata virusi na kwa wastani wa kuanzia wiki moja hadi siku10 zitakuwa zinaonekana. Kipindi cha ugonjwa kwa kawaida hutajwa kuwa kinaanza na dalili 'kavu' kwa mfano mwanzoni hujitokeza homa, maumivu makali ya viungo, kuchoku na kisha huendelea hadi dalili zenye "majimaji" mfano kuharisha na kutapika kadiri mtu anavyozidi kubanwa na ugonjwa.

Homa kali, maumivu makali ya kichwa, misuli na viungo, kuwa dhaifa hata kushindwa kutembea au kunyanyuka, kukonda, kuchoka kupindukia, kuumwa koo, kukosa hamu ya kula, kuumwa tumbo, kuharisha na kutapika na baada ya hapo damu huanza kutoka.

Wataalamu wanataja kuwa na macho mekundu, vipele kwenye ngozi na kwikwi kali kwa hatua za mwisho kuwa ni mambo yanayoambatana na ugonjwa huo bila kuwapo magonjwa nyemelezi kama mafua makali, malaria au homa ya matumbo.

**KUJIEPUSHA**

Kusafisha mikono mara kwa mara ni silaha namba moja kama ilivyokuwa kwa COVID-19 inashauriwa kutumia sabuni na maji yanayotiririka kwa ukamilifu na kusugua sehemu mbalimbali za mikono na pia kutumia vitakasa mikono.

Kunawa ni muhimu kwa vile unaweza kushika makamasi au maji maji za mwenye virusi vya ebola bila kujua, hivyo unaponawa unadhibiti visisambae.

Kama ilivyokuwa kwa UVIKO-19 acha kupeana mikono wala kukumbatiana unaweza kupata maradhi kwa njia hiyo.

Inashauriwa pia kutokugusa pua, macho na mdomo kwa vile virusi vya ebola vinaweza kuingia mwilini kupitia sehemu hizo laini. Lakini watu wanashauriwa kukimbilia hospitalini wanapoona dalili za homa, kujisikia vibaya ni tofauti na maelekezo ya zamani kuwa ukae nyumbani ikiwa unajisikia vibaya.

Jingine la muhimu ni kujiepusha na ebola ni vyema kuepuka kuwinda na kula wanyamapori kama swala, kima, nyani hasa wakati huu wa milipuko na kukaa mbali na vitoweo kama hivyo na kama ili kuzuia kuenea kwa maradhi ni vyema kudumisha umbali kutoka kwa wanyama pori.

Lakini, kujiweka mbali na watu angalau mita moja kama ilivyokuwa kwa UVIKO -19 hasa kwenye hospitali hata kama wagonjwa hawaonekani kuwa wana dalili za ebola ambazo wengi wanazihusisha na kutoka damu sehemu zenye matundu mwilini kama masikio, maeneo ya haja, machoni, midomoni na puani.

## WANENAVYO MALENGA

# MTAMA NI KWA WATOTO

HII elimu ziada, ambayo tunaitaka,
Kula kula kawaida, huku mwili wakauka,
Kumbe twapoteza muda, seli zinaharibika,
Tuutumie mtama, kwa virutubisho bora.

Mtama ni kwa watoto, wakubwa wanahusika,
Hivyo tunatoa wito, hicho chakula hakika,
Watu wazima watoto, afya itaongezeka,
Tuutumie mtama, kwa virutubisho bora.

Seli mwili haribika, kwa mtama zafufuka,
Mtu unaimarika, afya ya kurukaruka,
Si kudondokadondoka, kisha kusahaulika,
Tuutumie mtama, kwa virutubisho bora.

Watafiti wetu TARI, kutujuza wahusika,
Mtama livyo mzuri, kwa afya kuimarika,
Kusikiza ni vizuri, kwenye menyu kutumika,
Tuutumie mtama, kwa virutubisho bora.

Ugonjwa wa kisukari, mwili unapoteseka,
Mtama kula vizuri, madini chuma yafika,
Yanaondoa dosari, damu inavyozunguka,
Tuutumie mtama, kwa virutubisho bora.

Bidhaa mtama pia, nyinginyingi zahusika,
Kama tukizitumia, mwili unachangamka,
Zingine twazijulia, mpya pia zasikika,
Tuutumie mtama, kwa virutubisho bora.

Unga mtama mzuri, mkate ukaumuka,
Ni kitafunwa kizuri, na afya yaimarika,
Tumia usisubiri, huku mwili wameguka,
Tuutumie mtama, kwa virutubisho bora.

Kwa kutengeneza bisi, mtama unahusika,
Keki oka kwa nafasi, biskuti pia pika,
Chakula cha mwendokasi, kwa mwili kuimarika,
Tuutumie mtama, kwa virutubisho bora.

Tusibaki na mahindi, mtama unahusika,
Wala tusiwe mafundi, ngano peke kuitaka,
Tuingie kwenye kundi, mtama uzidi lika,
Tuutumie mtama, kwa virutubisho bora.

Wachakataji bidhaa, hapo pia mwahusika,
Mtama uweze jaa, soko na kwenye maduka,
Nyumbani hatutakaa, huo utanunulika,
Tuutumie mtama, kwa virutubisho bora.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**

TEKNOLOJIA

NA BEATRICE PHILEMON

# Mashine za kusokota kisasa za Japan sasa zinakuja nchini

## •Zitakazosuka mazulia na mikeka
## •Bomba kuuzika kitaifa, kimataifa




Mourad Ben, Meneja Masoko wa Kampuni ya Asagoe MFG Co Ltd (kulia), akionyesha wateja mati za mezani walipotembelea banda lao wakati wa maonyesho Dar es Salaam. **PICHA: BEATRICE PHILLEMON.**

UNAPOZUNGUMZIA mashine za kisasa za kusokota, si wajasiriamali wengi hasa wanaotengeneza mikeka, majamvi, mazulia yawe ya ndani , vyumbani au milangoni na mati za mezani wanazifahamu.

Ukweli ni kwamba mashine hizi zinazoingizwa nchini na kampuni za Japan zinazokusudia kuanzisha viwanda vidogo vya usokotaji zinauwezo wa kutengeneza au kusokota bidhaa za aina mbalimbali kwa kutumia malighafi kama majani ya asili kutengeneza matumizi mbalimbali.

Mashine hizo zinaweza kutengeneza zaidi ya bidhaa za kusokota zinazalisha pia bomba za plastiki zinazojulikana kama P.P pipe, kwa ajili ya biashara, utalii na shughuli nyingine nyingi kutegemeana na mtumiaji.

Ni mkakati wa kuzileta nchini na kuwafundisha teknolojia yake, anasema, Meneja Masoko wa Kampuni ya Asagoe MFG Company ya Japan, Mourad Ben, akiwa Dar es Salaam kutangaza na kusaka masoko ya bidhaa zake.

Anazisifia kuwa zina teknolojia za kutengeneza mikeka inayoweza kutumika kwenye ibaada, nyumbani, sehemu za burudani kama ufukweni, kwenye kambi za kiutalii pia mashine hizo zinaweza kutumiwa kuzalisha mati za mezani, mazulia mbalimbali na vitambaa vya kufunika mito ya makochi ( cushion) na vitu vingine vya kuegemea.

Akizungumza na Nipashe katika maonyesho ya kimataifa ya biashara ya bidhaa za chakula, vifungashio, uchapishaji, plastiki na zana za kilimo, yanayofanyika Dar es Salaam hivi karibuni, Meneja Masoko wa Kampuni ya Asagoe MFG Company, anaongeza kuwa kampuni hiyo ndiyo inayoleta teknolojia hiyo Tanzania.

Aidha, anaahidi kuwasaidia Watanzania walio tayari kununua mashine kutoka Japan ili waweze kutumia mashine zenye tekinolojia ya kisasa, kuweka vitega uchumi na kuzalisha bidhaa mbalimbali kulingana na mahitaji ya soko .

Anasisitiza kuwa, mashine zinaweza kutumia malighafi za nchi zinazohusika kwa mfano mianzi na mikoche kwa Tanzania inaweza kutumiwa na kwamba hakuna sababu wala ulazima wa kuagiza malighafi kutoka nchini kwake.

Ben, anasema wanasaka wasambazaji wa bidhaa zao ili kusaidia Watanzania kupata mashine hizo zinazotumia tekinolojia ya hali ya juu na kurahisisha usokotaji.

"Hii ni mara yangu ya kwanza kuja Tanzania kushiriki maonyesho, nimefanikiwa kuleta mashine za aina mbalimbali za kusokota 'weaving machines' kama vile za kusokota majani asilia, kusokota mati za mezani za kubana na kuzitangaza nchini," anasema.

Anasema, wanaleta teknolojia hiyo kusaidia wajasiriamali na wananchi wanaotaka kuanzisha viwanda vidogo, kuzalisha bidhaa za aina mbalimbali kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi lakini kuwezesha kupata ajira kwa vijana ili kuzuia vijana kujiingiza kwenye uhalifu ukiwamo wizi, ujambazi na ukahaba kwa madai ya hali ngumu ya maisha na kukosa kipato.

"Kwa kuanzia, kampuni yetu inalenga wateja wanaopenda kuanzisha kiwanda kinachoanza kwa gharama ya dola za Marekani 160,000 takribani Shilingi milioni 372.8. Mbali na hilo, hata Watanzania wanaopenda kununua mashine kutoka Japan kwa ajili ya kuanzisha kiwanda kidogo chenye gharama inayoanzia dola 15,000 karibu milioni 34.95 mpaka dola 50,000 karibu sawa na Shilingi milioni 116.5 ."

Hadi sasa kampuni yake imeuza zaidi ya mashine 10,000 za kusokota katika nchi mbalimbali za Afrika, anasema Ben na kuongeza kuwa kati ya hizo, mashine 3,000 zimeuzwa Nigeria, 500 Togo, nyingine 100 nchini Chad, zaidi ya 400 Senegal na 400 Cote d'Ivoire-Ivory Coast .

"Tunafahamu watu wengi katika nchi za Afrika ikiwamo Tanzania wanapenda hela na kazi, kama mtu akifanya kazi ya kumpatia hela hawezi kufanya uhalifu wala kuwa tapeli ," anasema Ben.

### KUVUTIA WANUNUZI

Ben akizungumzia mikakati ya kufikia mataifa mbalimbali, anasema hadi sasa kampuni yake ina tawi Japan katika eneo la Mishima, Minami-ku, katika mji wa Okayama lakini haina tawi nje ya nchi hiyo.

Anasema, kwa wafanyabiashara au wajasiramali ambao wapo tayari kununua mashine hizo kutoka Japan kampuni yake itawasaidia kupata mashine hizo ili waweze kuanzisha viwanda vidogo au biashara.

"Wafanyabiashara au Mtanzania atakayenunua mashine kutoka Japan watapata pia fursa ya kwenda kutembelea kiwanda chao nchini humo bila gharama ili kujifunza jinsi wanavyofanya kazi, kufunga mitambo kuikarabati au kuifanyia matengenezo na hata kujifunza utamaduni wa Kijapan hasa jinsi ya kufanya kazi na kupata fedha," anasema Ben.

Lakini, mara baada ya mashine kuwasili Tanzania kutoka Japan, anaahidi kuwa kampuni yake itatuma wahandisi au mainjinia nchini kutoa mafunzo kwa wateja jinsi ya kufunga mashine hizo, kufanya matengenezo na masuala mengine au changamoto zitakazoibuka.

Katika mahojiano yake anasema amekuwapo nchini kwa siku kadhaa akiambatana na Mhandisi wa Kampuni, Masanori na kushiriki maonyesho ya kimataifa yaliyoanza Septemba 22 hadi 24 yakifanyika katika ukumbi wa Diamond Jubilee jijini Dar es Salaam na kushirikisha wafanyabiashara mbalimbali .

Mbali na hilo, pia Asagoe MFG Company, ilikuja kufanya utafiti kuhusu soko la Tanzania, kuangalia mifumo ya kibenki na kujifunza ni jinsi gani mteja anaweza kutuma pesa Japan kama akinunua mashine kutoka kwao.

"Nawashukuru waandaaji wa maonyesho haya kwa sababu kupitia jukwaa hili tumekutana na watu mbalimbali wakiwamo wafanyabiashara kutoka India, Palestina na Tanzania na wamependa mashine zetu na kutoa email na oda ambazo bado zipo kwenye hatua ya mwanzo, lakini tunaamini zitaleta mafanikio chanya," anasema.

Maonyesho haya yamewapa mwangaza na mawazo mapya kwa sababu wamekutana na Wahindi na Wachina wengi wanaofanya biashara nchini hivyo, wanaamini kuwa wao wataweza kufanya biashara na Watanzania kwa sababu kuna fursa nyingi za kibiashara, anasema Ben.

Anaeleza kuwa kampuni ya Asagoe MFG Co Ltd, imeanzishwa mwaka 1939, hadi sasa bidhaa zake zimepata umaarufu duniani kutokana na ubora wa hali ya juu na kuboresha teknolojia kila wakati ili kuendana na mahitaji ya soko.

"Tuna uzoefu na nchi za Afrika, ni ukweli kwamba Afrika na Japan tunajitahidi kuwa karibu, tunaona kuwa bara hili kuna fursa nyingi za kibiashara ambazo pande zote mbili zinaweza kuwa na faida kwa kila upande " anasema Ben.

## HABARI PICHANI




Mwenyekiti mpya wa CCM Wilaya ya Muheza, Tanga, Laick Gugu mwenye kipaza sauti, akitoa maelekezo kwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa chama wilaya baada ya kushinda katika uchaguzi juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Madereva wa bodaboda wakivuka barabara ya Bagamoyo eneo la Mwenge, Manispaa ya Kinondoni Dar es Salaam jana, bila kusubiri taa ziwaruhusu, kitendo kinachoweza kusababisha ajali. **PICHA: SABATO KASIKA**




Katibu Mkuu wa Chama cha ACT- Wazalendo, Ado Shaibu, akifurahia jambo na wanachama wa chama hicho katika Jimbo la Tandahimba mkoani Mtwara juzi, ikiwa ni ziara yake ya kukaagua uhai wa chama. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

### CHEMSHABONGO NA -00 8 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com


Dondoo: Kulia
1. aina mojawapo ya ngoma za wanawake waswahili
4. mnyama ambaye ni mlinzi
6. tabia njema
8. vipindi vya miezi 12
11.nyanyua
12.alama katika maandishi (,)
14.chukua kitu kwa siri
15.kuku dume
16.Jakarta ni mji wake mkuu

Chini:
1. nchi ya mwisho kujitangazia uhuru kutoka Urusi
2. nchi yenye mto Gambia
3. maksi
5. shina la mtama
7. ndugu wa kiume wa Baba
9. beta
10.tundu
12.mji mkuu wa Rwanda
13.fikira



Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

UCHOKOZI UZI
AMINA SAA
AMURU UDI
JAWABU AMU
DARASA SUMU
DARAJA ADA
DUNIA RADI
IKAMA TAA
ANIKA UTU
AMANA INSI
RUDIWA
UNGUA
MATUNDA
UREMBO




Majibu toleo lililopita




maoni: 0755429240



## Aomba nguvu kwa viongozi wa dini kusaidia wanafunzi

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

MKURUGENZI wa Shule za Patrick Mission ya jijini Dar es Salaam na Paradise Mission Pre and Primary School ya mkoani Mbeya amewaomba viongozi wa dini kufanya maombezi kwa wanafunzi wa madarasa ya mitihani ili wafanye mitihani wakiwa salama na kufikia ndoto zao kielimu.

Ndele Mwaselela alitoa rai hiyo juzi wakati wa ibada maalum ya kuwaombea wanafunzi wa darasa la saba mkoani Mbeya.

Ibada hiyo ilifanyika katika Kanisa la Tanzania Assemblies of God (TAG) Revival Temple la jijini Mbeya.

Mwaselela alisema katika kipindi hiki ambacho wanafunzi wa darasa la saba wanaelekea kufanya mitihani, huwa yanatokea matatizo ambayo yanaweza kuwakwamisha.

Alisema madarasa yote ya mitihani ambayo ni la saba, la nne, kidato cha pili na cha nne yanatakiwa kuombewa mara kwa mara ili wanafunzi wake kufanye vizuri katika mitihani hiyo.

"Kuna watoto wengine ambao wanahitaji maombi lakini hawajafika hapa kanisani leo. Kwa hiyo, ninawaomba sana viongozi na waumini wenzangu tuwaweke kwenye maombi, mimi shule zangu zote maombi ni muhimu sana," alisema Mwaselela.

Alisema baadhi ya wanafunzi hao wanaweza wakawa wanaugua na hivyo wanahitaji maombi ili wapone na wafanye mitihani pamoja na wenzao na wafikie ndoto za maisha yao.

Vilevile, aliomba viongozi hao wa dini kuliombea taifa pamoja na viongozi wake ili amani iliyopo iendelee na shughuli za maendeleo ziendelee kufanyika.

Aliwaomba viongozi hao kuhubiri amani kwa maelezo kuwa wao wana watu wengi ambao wanawaamini na wanawasikiliza kile wanachowaambia kuliko mtu mwingine yeyote.

Mchungaji wa Kanisa hilo la TAG Revival Temple, Aman Mwasote, aliahidi kuendelea kuwaombea wanafunzi wote nchini ili wafanye mitihani na kufaulu vizuri huku akiwataka wazazi kuhakikisha wanawasaidia watoto wao.

Alisema watoto wanatakiwa kulelewa kwenye misingi ya Mungu ili kujenga taifa lenye watu wenye hofu ya Mungu ambayo itasaidia kupunguza matukio mabaya ndani ya nchi.

Mwasote alisema Watanzania wanakusanyika na kumwabudu Mungu kwa sababu taifa lina amani na hivyo akasisitiza kuwa wataendelea kuomba amani hiyo iendelee kudumu.

Mwasote alisema serikali imeweka mazingira rafiki kwa wananchi wake kuwa na uhuru wa kuabudu tofauti na mataifa mengine ambayo huwa wananchi wanashindwa kuabudu kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo vita.

# Wizara yatekeleza agizo la Rais huduma ya maji

**Na Nebart Msokwa,** TUKUYU

WIZARA ya Maji imetekeleza agizo la Rais Samia Suluhu Hassan la kuhakikisha wananchi wa Mji wa Tukuyu wilayani Rungwe katika Mkoa wa Mbeya wanapata maji ya bomba ndani ya kipindi cha miezi miwili.

Rais Samia alitoa agizo hilo Agosti 7, mwaka huu, alipokuwa ziarani mkoani Mbeya baada ya wananchi wa Tukuyu kulalamika wanakabiliwa na tatizo la ukosefu wa maji ya bomba kwenye mji huo, hali inayowafanya watumie muda mwingi kutafuta huduma hiyo.

Kufuatia agizo hilo, Wizara ya Maji ilianzisha mradi wa kupeleka maji katika Mji wa Tukuyu kutoka katika chanzo cha Mto Mbaka, mradi ambao sasa umekamilika kwa asilimia 52 na wananchi wa mji huo kuanza kupata maji.

Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi juzi alitembelea wilayani Rungwe kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa agizo hilo la Rais, akifika kwenye chanzo cha maji cha Mto Mbaka ili kujiridhisha maendeleo ya mradi huo.

**Kwa sasa tunaendelea na mradi huu na tunaamini kuwa wananchi wataanza kupata huduma kwa muda wa saa 24 kila siku kwa sababu chanzo ni cha uhakika.**

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi huo mbele ya Naibu Waziri, Mkurugenzi wa Ufundi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA), Barnabas Komba alisema mradi huo unaendelea kujengwa.

Komba alisema kutokana na mradi huo kuanza kuhudumia wananchi wa Tukuyu na hali ya upatikanaji wa majisafi na salama utaongezeka kutoka asilimia 32 za awali mpaka asilimia 100 ifikapo Novemba mwaka huu.

Alisema kwa sasa baadhi ya wananchi wa mji huo wameshaanza kunufaika baada ya mtandao wa mabomba kulazwa kwa zaidi ya kilomita tano katika mji huo.

"Kwa sasa tunaendelea na mradi huu na tunaamini kuwa wananchi wataanza kupata huduma kwa muda wa saa 24 kila siku kwa sababu chanzo ni cha uhakika," alisema Komba.

Mkurugenzi wa Mbeya-WSSA, Gilbert Kayange alisema mradi huo unazalisha lita milioni 25 wakati mahitaji ya Mji wa Tukuyu ni lita milioni 15 pekee na hivyo maji mengine yatakuwa yanapelekwa kwenye vijiji jirani.

Kayange alisema mradi huo umetekelezwa kwa Sh. bilioni nne ambazo zilitolewa na Wizara ya Maji na mamlaka imeutekeleza kwa kutumia wataalamu wa ndani.

Naibu Waziri wa Maji, Mahundi, aliwapongeza wataalamu wanaojenga mradi huo kutokana na kukamilisha mradi huo ndani ya muda uliopangwa.

Alisema hiyo ilikuwa ni awamu ya kwanza na awamu ya pili itakuwa ya kusambaza maji kwenye maeneo ya wananchi ambayo awali hayakuwahi kupata huduma ya maji.

"Awamu ijayo tutawaletea Sh. milioni 500 ili zitumike kusambaza huduma hii kwenye mji huu wa Tukuyu, tutakuwa tumetimiza lengo la Rais Samia la kusogeza huduma kwa wananchi," alisema Mahundi.

Alisisitiza wizara hiyo itaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maji nchini ili kuhakikisha wananchi wanasogezewa huduma karibu na maeneo ya makazi yao.




Baadhi ya wagombea wa nafasi ya ujumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Mbeya Mjini wakionyesha wapigakura namba zao za kuwapigia katika uchaguzi uliofanyika juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Waanzisha kiwanda kuzalisha maji tiba

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HOSPITALI ya Rufani ya Kanda Mbeya imeanzisha kiwanda cha kuzalisha maji tiba ili kuondokana na uagizaji wa maji hayo kutoka nje ya nchi.

Mkurugenzi wa Hospitali hiyo, Dk. Godlove Mbwanji, alibainisha hayo jana alipozungumza na Nipashe, akisema wanazalisha maji hayo yenye ujazo wa mililita 250 na 500 ambazo awali walikuwa wanalazimika kuagiza nje.

Alisema kiwanda hicho kimesaidia kuboresha huduma za matibabu kwa wananchi wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambao wanatibiwa kwenye hospitali hiyo.

Alisema hospitali hiyo ilikuwa inatumia fedha nyingi kwa ajili ya kuagiza maji tiba hayo kutoka nje na sasa fedha hizo zimehamishiwa kwenye uboreshaji wa huduma zingine za matibabu.

"Kiwanda chetu kimekamilika kwa asilimia 100 na kimeshaanza kuzalisha, kina uwezo wa kuzalisha lita 120 ambazo zinatosheleza mahitaji ya hospitali yetu," alisema Dk. Mbwanji.

Alisema kwa sasa wana mpango wa kuanzisha kiwanda cha kutengeneza dawa za kutibu macho ambacho pia kitasaidia kuondokana na uagizaji wa dawa hizo nje ya nchi.





# Wazee wamwomba waziri kutimua waliovamia makazi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZEE wamemwomba Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Doroth Gwajima kuchukua hatua kufuatia baadhi ya watu kuvamia eneo la makazi ya wazee Nunge, Kigamboni mkoani Dar es Saalam na kujenga vibanda vya biashara na makazi.

Mwenyekiti wa Baraza la Wazee mkoa huo, Salum Matimbwa alibainisha hayo juzi wakati akitoa neno la shukrani kwenye kongamano la wazee lililofanyika jijini hapo.

Matimbwa alisema kituo hicho kilijengwa mwaka 1936 lakini inasikitisha kwa sasa kila upande wa eneo hilo lililokuwa na zaidi ya ekari 50 umevamiwa.

**Ni wakati sasa kwa watu binafsi kuanzisha vituo vya kuwahudumia wazee kama ilivyo kwa maeneo mengine.**

"Hili eneo lilikuwa na ukubwa wa zaidi ya ekari 50 lakini sasa ninasikia serikali kutokana na kuvamiwa imekubali kubaki na ekari 20 wakati bikoni zipo pale hata wakati wa mkoloni.

"Tunachoweza kuona umetusaidia ni kuisimamia sera ya wazee ili izae sheria ambayo kwani kumekuwa na sintofahamu ya muda mrefu hata tunashindwa kusimamia kile tunachokitaka kwa muda mrefu," alisema Matimbwa.

Waziri Dk. Gwajima alisema ni wakati sasa kwa watu binafsi kuanzisha vituo vya kuwahudumia wazee kama ilivyo kwa maeneo mengine.

Alisema hivi sasa wanasuka mpango wa huduma kwa wote ambao utakwenda kusaidia maboresho makubwa ya jinsi ya kuwahudumia watu.

Kuhusu Sera ya Wazee alisema kwa sasa inafanyiwa mapitio kwa ajili ya kuiboresha iweze kuendana na hali ya sasa huku wakiendelea kuusuka upya mpango wa huduma kwa wazee.

Kuhusu makazi ya wazee alisema kuwa, yanafanyiwa ukarabati nchi nzima ili yawe kwenye ubora unaotakiwa na kuepusha uvamizi kwa watu ambao wamekuwa kila wakati wakiyanyemelea.

Kamishna wa Ustawi wa Jamii, Nandela Muhando, alisema kongamano hilo limekusanya takribani wazee 300, kutoka mikoa yote Tanzania bara, kwamba tangu jana walikuwa na mada mbalimbali kwa ajili ya kuwajenga na upimaji wa afya.




Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), Mhandisi Victor Seff, akizungumza na waandishi wa habari katika ukumbi wa Maelezo jijini Dodoma jana, kuhusu shughuli za TARURA na mwelekeo wa utekelezaji kwa mwaka wa fedha. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mwenyekiti CCM Wilaya ya Dodoma abwagwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

ALIYEKUWA Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Dodoma Mjini, Meja mstaafu Johnick Risasi, ameshindwa kutetea kiti chake baada ya kushindwa katika uchaguzi uliofanyika juzi.

Uchaguzi wa viongozi wa CCM Wilaya ya Dodoma ulifanyika Oktoba Mosi, 2022, chini ya usimamizi wa Mkuu wa Wilaya hiyo, Jabir Shekimweri.

Risasi alishindwa na aliyekuwa Mjumbe wa Kamati ya Siasa CCM Dodoma, Charles Mamba ambaye alipata kura 1,094 kati ya kura 1,344 zilizopigwa sawa na asilimia 73.1.

Akitangaza matokeo hayo, Shekimweri alitaja idadi ya kura alizopata Meja mstaafu Risasi ni 206 wakati mgombea wa tatu Vanessa Malesa alipata kura 21.

Kwa matokeo hayo, CCM Dodoma Mjini itaongozwa na viongozi wapya kwa sehemu kubwa baada ya wenyeviti wa jumuiya za vijana, wazazi na UWT kupoteza viti vyao.

Wengine waliochaguliwa ni wajumbe wa halmashauri, Christina Kamunya, Christina Mlugu, Jesca Mbogoni na Bushura Mohamed (kundi la Wanawake).

Kundi la vijana waliochaguliwa ni Enock Mwaliko, Fredrick Mwinje, Chris Madaha na Happy Mwajunga wakati wajumbe kundi la wazazi ni Mussa Luhamo na Adam Msendo.

Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa waliochaguliwa ni Anthony Kanyama, Neema Mkobalo na Julian Bruno wakati mkutano wa mkoa ni Hawa Pyuza na Taus Ayubu.

# Wanaotetea ndoa jinsia moja wapewa angalizo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MWENYEKITI wa Bodi ya Mashirika yasiyokuwa ya kiserikali nchini, Mwantumu Mahiza ameyaonya mashirika ambayo yanajihusisha na kutetea ndoa za jinsia moja kinyume na mila za kitanzania kwa madai ya kulinda haki za binadamu kuacha mara moja.

Alitoa onyo hilo juzi jijini Dodoma wakati akifungua mkutano mkuu wa mwaka wa wakurugenzi wa mashirika yasiyokuwa ya kiserikali nchini.

Alisema katika kipindi chake akiwa mwenyekiti wa bodi hiyo hatopenda kuona jambo hilo linatokea kwa kuwa ni kinyume na mila na desturi za Watanzania.

"Kama kuna shirika lolote ambalo katika utekelezaji wa majukumu yake limepanga kufanya vitu kama hivyo naomba lifute mpango huo mara moja hatuwezi kuviruhusu vitu kama hivi katika taifa hili ambalo serikali ipo na dini zipo,"alisema Mwantumu.

Alisema siyo jambo la busara kwa taifa kuruhusu vitendo vya ndoa za jinsia moja kwa mwanamke kuolewa na mwanamke mwenzake au mwanamume kuoa mwanamume mwenzake.

"Hatuwezi kuruhusu haki za binadamu zinazopingana na mila zetu hata mara moja leo hii hata wewe mwanao wa kiume unasikia anaolewa na mwanamume mwenzake utajisikiaje?" alihoji Mwantumu.

Pia alisema takwimu zinaonyesha kuwa idadi ya wanawake ni kubwa kulinganisha na wanaume, hivyo ndoa za jinsia moja ni jambo ambalo halipaswi kupewa nafasi.

"Hata ukienda leo hospitali kati ya watoto 10 wanaozaliwa kwa siku wanawake ni saba wanaume ni watatu, hivyo kama tusipokuwa makini hii nchi itakuwa ya wanawake tupu, wanaume watakwisha kwa sababu wanaoana wao kwa wao," alisisitiza.

Aliyataka mashirika kufanya kazi kwa kushirikiana na serikali ili kuondoa dhana iliyojengeka kuwa asasi za kiraia ni adui wa serikali.

"Hapo zamani ilijengeka kuwa asasi za kiraia ni adui na serikali jambo hilo siyo sawa kwani wote kila tunachokifanya ni kwa ajili ya maslahi ya taifa letu hivyo tunajenga nyumba moja hatipaswi kugombania fito," alisisitiza Mahiza.

Aliyataka mashirika kutotumia upungufu uolipo katika maeneo mbalimbali yanayosimamiwa na serikali kama fursa ya kupata fedha kwa wafadhili.

"Leo hii tumefika mahala tunavuana nguo ili tupate fedha kwa wafadhili nawaombeni kama shirika linabaini kuna tatizo fulani basi kuwasiliana na uongozi wa eneo husika ili zifanyiwe kazi badala ya kupiga picha na kutuma huko duniani," alisema.

Mkurugenzi wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), Onesmo Olengurumwa, alisema lengo la mkutano ni pamoja kupata fursa ya kukumbushana mambo mbalimbali.

Pia aliiomba serikali kuifanyia marekebisho sera inayosimamia mashirika yasiyo ya kiserikali ikiwa ni pamoja na kuyaondolea kodi katika vitu mbalimbali ambavyo wamekuwa wakiingiza kutoka nje ya nchi.

Mrajis wa Asasi za Kiraia Zanzibar, Khalid Adulla, aliwataka washiriki wa mkutano huo kutumia fursa hiyo kujadiliana matatizo yaliyoko kwenye jamii na kuzifanyia kazi.



# ‘Wazee wanakabiliwa na matatizo ya kiafya’

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema wazee wanakabiliwa na matatizo mengi ya kiafya ikiwamo shinikizo la damu, moyo, kisukari, maradhi ya viungo na macho, hali ambayo huwaathiri na kupunguza uwezo wa kufanya kazi na kujipatia kipato.

Amesema katika kukabiliana na matatizo hayo, serikali yake imejenga majengo ya kisasa ya hospitali yanayoendana na hali ya wazee, kuajiri madaktari bingwa, vifaa vya kisasa na dawa za kutosha ili kutoa huduma bora kwa wananchi wakiwamo wazee.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki katika hotuba yake iliyosomwa na Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdullah katika kilele cha Siku ya Wazee Duniani.

Rais Mwinyi alisema tangu mwaka 1964 serikali inaendeleza jitihada za kuwalea na kuwatunza wazee na kwa sasa kuna wazee 66 ambao wanalelewa katika nyumba maalum za serikali.

Hivyo, aliitaka jamii kutokwepa majukumu ya kuwalea wazee wao na kuacha tabia ya kuwapeleka kulelewa katika makao ya wazee serikalini.

Alisema wazee wanahitaji mapenzi na huruma kutoka kwa watoto wao na jamii inayowazunguka.

**Hadi kufikia Septemba mwaka huu wazee 28,706 wamesajiliwa kwa ajili ya malipo ya pensheni hiyo ambayo hutolewa kila mwezi, wakipatiwa kila mmoja Sh. 20,000.**

Rais Mwinyi alisema familia inayowatunza wazee, hupata baraka na neema, hivyo ni vyema jamii kuwalea wazee katika familia zao kama ambavyo wazee hao walivyotumia muda, nguvu na rasilimali zao kuwatunza watoto wao.

Alisema kwa kuona umuhimu na mchango mkubwa wa wazee katika kuleta maendeleo, mwaka 2016 serikali ilianzisha mpango maalum wa kuwapatia pensheni wazee wote wenye umri wa kuanzia miaka 70.

Alisema hadi kufikia Septemba mwaka huu wazee 28,706 wamesajiliwa kwa ajili ya malipo ya pensheni hiyo ambayo hutolewa kila mwezi, wakipatiwa kila mmoja Sh. 20,000.

Rais Mwinyi alisema pensheni hiyo imewasaidia wazee kuimarisha maisha yao na serikali inaendelea kuimarisha huduma za wazee ikiwamo afya na usafiri na imeanza kutoa vitambulisho maalum vya kuwasaidia wazee kupata huduma hizo kwa urahisi.

Shafika Ahmed Salum alisema wazee wa Zanzibar wanakabiliwa na matatizo mengi katika sekta mbalimbali ambazo zinakwaza katika kufikia malengo yao.


Rais Mwinyi alizitaja miongoni mwa matatizo hayo ni mafao yanayotolewa kwa wazee kupitia pensheni jamii bado ni kidogo kutokana na hali ngumu ya maisha.

Alisema lishe duni ya wazee hasa wa vijijini bado ni tatizo ambalo haliangaliwi vyema pamoja na wazee kudhalilishwa kwa tuhuma za uchawi.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, alisema serikali inafanya kazi kubwa ya kuhakikisha wazee wanaishi katika maisha ya heshima kama wanadamu wengine jambo ambalo limedhihirika katika katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Alisema hata Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 imeelekeza kulindwa haki za binadamu wakiwamo wazee.

Mkurugenzi wa Shirika la Helpage Tanzania, Smart Daniel, alisema kitendo cha Zanzibar kuwa na mpango wa kutoa pensheni ya jamii kwa wazee ambayo hutolewa kila mwezi na kudhaminiwa na serikali kwa asilimia 100 kimeiheshimisha Tanzania jambo lililopelekea nchi zingine kufika Zanzibar kujifunza jambo hilo.




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akisalimiana na Balozi wa Uganda nchini, Fred Mwesigye (kushoto), alipofika Ikulu Zanzibar jana kwa mazungumzo pamoja kujitambulisha. **PICHA: IKULU**

## Wizara yatakiwa kusimamia maadili na mila kwa watalii

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdullah ameutaka uongozi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kusimamia nidhamu, mila, silka, tamaduni na maadili ya Zanzibar kwa watalii wote wanaoingia nchini.

Alitoa agizo hilo jana wakati akiahirisha Mkutano wa Nane wa Baraza la 10 la Wawakilishi Chukwani Zanzibar.

Alisema serikali itachukua hatua kali za kisheria kwa mtalii yeyote atakayekwenda kinyume cha sheria na miongozo iliyopo kwa maslahi mapana ya Zanzibar.

Alisema utalii ni sekta yenye mchango mkubwa kwa uchumi wa Zanzibar na kwa sasa sekta hiyo inaendelea kukua vizuri.

Alisema kuna ongezeko la watalii 133,541 na kufikia watalii 394,185 kwa mwaka 2021 kutoka watalii 260,644 kwa mwaka 2020.

“Hali hii inatokana na amani na utulivu iliopo nchini pamoja na utoaji wa huduma zilizo bora na kwa haraka katika viwanja vya ndege, bandari na hoteli yetu.

“Ninapenda kuipongeza sana Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale pamoja na sekta binafsi zinazoendelea kutoa huduma katika sekta ya utalii kwa juhudi za makusudi wanazozichukua katika kuhakikisha sekta hii inapata ufanisi zaidi,” alisema.

Aliongeza kuwa serikali inasikitishwa kuona kuna baadhi ya watendaji wasiokuwa waaminifu na weledi katika kazi zao kwenye taasisi za serikali.

“Tunashuhudia matumizi mabaya ya fedha za umma kwa ufisadi na rushwa, wizi wa mali za umma na upotevu wa fedha kama ilivyoelezwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG),” alisema.

Alibainisha kuwa vitendo hivyo vinaitia aibu serikali na kusababisha kutupiwa lawama kutoka kwa wananchi wake.

Makamu huyo aliwataka viongozi wenye dhamana kuwasimamia watendaji walio chini, ili kuvidhibiti vitendo hivyo na kuhakikisha kila mtu anapata haki yake kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa.

Alisema serikali haitakuwa na msamaha wa aina yoyote kwa mtendaji atakayebainika anafanya mambo kinyume cha taratibu za nchi na wala haitamwonea mtu yeyote na uchunguzi wa kina utafanywa kuhakikisha haki inatendeka.

# SMZ yaguswa na kifo cha dokta Mtanzania Uganda

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imetoa pole kwa familia ya Daktari Bingwa, Ali Mohamed Hafidha, aliyefariki dunia Uganda kwa ugonjwa wa ebola.

Waziri wa Wizara ya Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alitoa salamu hizo wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Mjini Zanzibar kuhusu kifo hicho pamoja na tahadhari zinazochukuliwa na Serikali ya Zanzibar katika kukabiliana na ugonjwa huo.

Waziri huyo alisema taifa limepokea kwa mshtuko kifo cha daktari huyo ambaye alikuwa akisomea tiba ya kibingwa.

Alisema kifo hicho kimeacha pengo kubwa kwa taifa kutokana na daktari huyo alikuwa akisomea tiba ya maradhi ambayo madaktari wake ni wachache.

Aliitaka familia ya marehemu kuwa wastahamilivu na subira katika kipindi chote cha msiba.

Mazrui aliwataka wanafunzi wote wa Zanzibar wanaosoma Uganda kuchukua aina zote za tahadhari kuhusu ugonjwa huo ili kuepuka athari zinazoweza kuwapata.

Alisema Wizara ya Afya ya Serikali ya Zanzibar imeanza kuchukua tahadhari ikiwamo kwa wageni wanaowasili nchini katika kufanya uchunguzi wa afya zao ikiwa ni tahadhari ya mlipuko wa ugonjwa huo tishio.

Alisema: “Tumeanza kutoa tahadhari kwa wanafunzi wetu wanaosoma Uganda katika vyuo mbalimbali kuchukuwa tahadhari ya ugonjwa huo ambao ni tishio kwa afya ya binaadamu.. lakini kwa wageni wanaoingia nchini tumeanza kufanya uangalizi mkubwa,” alisema.





# Mwanamume ang'atwa ulimi na mpenzi wake

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

**Mkasa huo ulitokea Septemba 29 mwaka huu majira ya saa tatu usiku na baada ya ndugu yake huyo kupata majeraha hayo.**

MKAZI wa Kijiji cha Mwamakalanga wilayani Shinyanga, Gembe Singu (32) anadaiwa kung'atwa ulimi na mpenzi wake, Leticia Elias (40) wakati wakifanya tendo la ndoa.

Inadaiwa kuwa wapenzi hao walikuwa na ugomvi na siku ya tukio mwanamke huyo alimwita Singu nyumbani kwake ili wazungumze na kumaliza tofauti zao.

Baaada ya mazungumzo walifikia mwafaka na wakaanza kufanya tendo la ndoa usiku, ndipo mwanamke huyo akatumia mwanya huo kumng'ata ulimi.

Akisimulia undani wa tukio hilo, kaka wa kijana huyo, Makoye Singu alidai mkasa huo ulitokea Septemba 29 mwaka huu majira ya saa tatu usiku na baada ya ndugu yake huyo kupata majeraha hayo, walimpelekea Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga kupata matibabu.

Alisema hali ya ndugu yake siyo nzuri licha ya kupatiwa matibabu kwa kuwa sababu hawezi kuongea vizuri na anakula chakula kwa shida na anaendelea na matibabu.

"Mdogo wangu huyu alikuwa na ugomvi na mpenzi wake, na siku ya tukio alimwita nyumbani kwake ili wakazungumze na kumaliza tofauti zao, ndipo wakaanza kufanya mapenzi na kutokea mkasa huo wa kung'atwa ulimi," alisema Singu.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Janeth Magomi, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kubainisha kuwa mtuhumiwa anashikiliwa na upelelezi unaendelea, akiahidi kuwa ukikamilika atafikishwa mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria.



Mhandisi Mwandamizi wa Mgodi wa Bucreef, Erick Yohana, akizungumza na washiriki wa maonyesho ya kitaifa ya teknolojia ya madini waliotembelea mgodi wa Bucreef ulioko Kijiji cha Lwamgasa mkoani Geita jana. **PICHA: JOCTAN NGELLY**

# Polisi, wananchi watunukiwa tuzo kwa kukomesha ukatili

**Na Vitus Audax,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza limewatunuku vyeti vya sifa na zawadi askari polisi na raia walioshiriki kufanikisha mapambano ya kukomesha vitendo vya uhalifu.

Tuzo hizo pia zimetolewa kwa askari hao kwa kusaidia kukomesha ukatili wa kijinsia katika maeneo mbalimbali.

Akiwatunuku vyeti hivyo, Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Mwanza, Ramadhani Ng'anzi aliwataka wananchi mkoani humo kutoa taarifa kuhusu vitendo vya kiuhalifu ili kuinusuru jamii.

Kamanda Ng'anzi alibainisha kuwa utendaji mzuri wa Jeshi la Polisi unategemea kuwapo wadau wanaolisaidia kwa kutoa ushirikiano kutoka kwa jamii inayowazunguka.

"Ninapenda kuwapongeza askari hawa wa vyeo vya chini kwa kulileteа sifa Jeshi la Polisi sambamba na vyeti na zawadi hizi tutafikisha taarifa zao makao makuu kwa ajili ya kuwasaidia kutunukiwa vyeo pamoja na ongezeko la mashahi," alisema.

Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Mkoa wa Mwanza, Yesaya Edward, alisema jeshi hilo lipo tayari kupokea taarifa katika vituo vyote vilivyoko karibu na wananchi huku akiwaondoa hofu juu ya usiri wa taarifa zao.

"Leteni taarifa kwa wakuu wa vituo vyote vilivyoko karibu yenu wapo tayari kuwasikiliza na mkiona taarifa zenu hazichukuliwi hatua nipigieni mimi simu muda wowote mahali popote nitafika," alisema.

Baadhi ya askari pamoja na wadau wengine wa Jeshi la Polisi waliotunukiwa vyeti vya sifa na zawadi kutokana na juhudi zao katika kupambana na vitendo vya kihalifu, waliahidi kuendeleza mapambano dhidi ya vitendo hivyo.

"Kupitia tuzo hii imeniongezea moyo wa kuzidi kupambana na vitendo vya kiuhalifu katika jamii ili kuhakikisha inakuwa salama pamoja na mali zao kwa kushirikiana na wananchi," alisema.

Mwananchi mwingine aliyepewa tuzo, Gasto Alex alisema: "Tutazidi kufanya kazi bega kwa bega na Jeshi la Polisi ili kutokomeza vitendo vya kiuhalifu vikiwamo matumizi ya dawa za kulevya pamoja na unyanyasaji unaozidi kushamili katika jamii zetu."

# Wenye ulemavu waiomba halmashauri pembejeo

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WATU wenye ulemavu wanaofanya shughuli za kilimo wameiomba Manispaa ya Kahama kuwasaidia kupata pembejeo bila malipo ili kuwawezesha kufanya kazi hiyo na kujipatia kipato.

Waliwasilisha maombi hayo jana kwa nyakati tofauti wakati wakizungumza na Nipashe kuhusu namna wanavyoshiriki katika kilimo na kujiingizia kipato hususani kwa mazao ya chakula na biashara yakiwamo ya pamba, tumbaku, alizeti, mahindi na choroko.

Halmashauri ya Manispaa ya Kahama imekuwa na utaratibu wa kutenga fedha kila mwaka wa fedha kutoka katika vyanzo vyake vya ndani kwa ajili ya kununua pembejeo na kuzigawa bure kwa vijana wenye uwezo wa kulima mazao ya chakula na biashara, lengo likiwa ni kuwainua kiuchumi.

Katika mwaka wa fedha 2019/20, serikali ilitenga Sh. milioni 17.94 na vijana 39 walinufaika na pembejeo hizo za ambao walilima ekari 195 na mwaka 2020/21 ilitenga Sh. milioni 24.58 kwa ajili ya wakulima na vijana 45 walionufaika kwa kulima ekari 225 za mazao hayo.

Mmoja wa watu wenye ulemavu, Tatu Nalimi ambaye ni mkulima na mkazi wa Nyandeka, alisema wanayo maeneo ya kulima mazao ya chakula na biashara lakini wanakosa fedha za kununulia pembejeo za kilimo.

Alisema wengi wao wamevuka umri wa ujana na hivyo kukosa sifa za kupata pembejeo hizo, hivyo katika mikopo inayotolewa kwao ya asilimia mbili kupitia mapato ya ndani, wanunulie pembejeo za kilimo na kuwagawia wale wenye uhitaji ili wajikite kwenye kilimo chenye tija.

Mkazi mwingine wa Manispaa ya Kahama, William Joseph alisema yeye amekuwa akijihusisha na kilimo cha alizeti, mpunga na mahindi, lakini vikwazo wanavyokutana navyo ni pamoja na ukosefu wa pembejeo.

Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Anderson Msumba, alisema wamekuwa wakitenga fedha kila mwaka na kununua pembejeo za kilimo na kuzigawa bure kwa wakulima vijana bila kujali hali zao za kimaumbile na mazao wanayoyapata ni yao na siyo ya halmashauri.

"Vijana wetu wananufaika na uwapo wa pembejeo ambazo tumekuwa tukizitoa kila mwaka wa kilimo, fedha za ununuzi wake zinatokana na mapato yetu ya ndani, mwaka jana tulitenga Sh.milioni 54 na mwaka huu tumetenga zaidi Sh. milioni 84," alisema Msumba.

HABARI KIMATAIFA

# Kiongozi aliyepinduliwa Burkina Faso ajiuzulu

**OUAGADOUGOU, Burkina Faso**

KIONGOZI wa kijeshi nchini Burkina Faso, Paul-Henri Sandaogo Damiba, amekubali kujiuzulu siku mbili baada ya maofisa wa kijeshi kutangaza kumuondoa madarakani.

Taarifa iliyotolewa na viongozi wa kidini na wa kijamii ilieleza kuwa Luteni Kanali Damiba, aliomba kujiuzulu jana ili kuepusha madhara yanayoweza kusababishwa na makabiliano dhidi ya raia na uharibifu wa mali.

Ilielezwa kuwa hatua hiyo inatokana na mazungumzo yaliyofanyika kati ya Damiba na kiongozi mpya aliyejitangazia madaraka, Kapteni Ibrahim Traore.

Viongozi wa kidini waliosaidia katika juhudi za upatanishi walisema Damiba ametoa masharti saba ili aweze kuondoka madarakani, ikiwamo kuhakikishiwa usalama na haki yake pamoja na usalama wa washirika wake katika jeshi.

Pia, aliwataka waliochukua madaraka kuheshimu ahadi aliyoitoa kwa Jumuiya ya Uchumi ya Nchi za Afrika Magharibi, (ECOWAS) ya kurejesha utawala wa kiraia katika kipindi cha miaka miwili.

Kwa mujibu wa viongozi hao wenye ushawishi mkubwa nchini Burkina Faso, Traore, mwenye umri wa miaka 34 aliyakubali masharti yaliyowekwa na Damiba, huku akitoa wito kwa wananchi kuwa watulivu, kujizuia na ghasia na kuswali.

Taarifa iliyotolewa jana na wanajeshi wanaomuunga mkono Traore, ilisema kuwa, ofisa huyo wa jeshi ataendelea kuwa kiongozi wa nchi hadi atakapoapishwa rais wa Burkina Faso aliyeteuliwa na vikosi vya jeshi la taifa hilo la Afrika Magharibi, katika tarehe ambayo haijatajwa.

AWAKABILI WANAOSABABISHA MACHAFUKO

Traore pia, alitangaza kuwa anaungwa mkono na makamanda wa kijeshi ili kuimarisha upya mapambano dhidi ya wapiganaji wa jihadi.

Aidha, katika taarifa ya, ECOWAS imepongeza hatua ya pande zote kukubali kukabidhi madaraka kwa njia ya amani na kuondoa tofauti zao.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, ujumbe wa ECOWAS ulienda Ouagadougou jana.

Vilevile, ilielezwa kuwa baada ya kufanya mapinduzi, kiongozi huyo wa kijeshi alikutana na baraza la mawaziri na kusema kuwa nchi nzima iko katika hali ya tahadhari, na hivyo wanahitaji kuharakisha mambo.

"Kila mmoja katika hali hii anapaswa kufanya haraka na kuachana na urasimu na kufuata sheria. Burkina Faso kila kitu ni muhimu na cha haraka. Kuanzia usalama hadi ulinzi, afya, huduma za kijamii hadi miundombinu. Tunalazimika kusonga mbele haraka," alisisitiza Traore.

Wakati huo huo, taarifa za kidiplomasia za kikanda zilieleza kuwa Damiba ambaye naye alichukua madaraka kwa njia ya mapinduzi ya kijeshi mwezi Januari, 2022 Jumapili alikimbilia kwenye mji mkuu wa Togo, Lome.

Huku hayo yakijiri Ufaransa imelaani shambulizi lililofanywa na waandamanaji wenye hasira katika Ubalozi wake na majengo mengine nchini Burkina Faso.

Wizara ya mambo ya nje ya Ufaransa imekanusha madai ya uongozi mpya wa kijeshi wa Burkina Faso kwamba Damiba alipewa hifadhi kwenye kambi ya kijeshi ya Ufaransa.

Mapinduzi ya Ijumaa yamekosolewa vikali na jumuia ya kimataifa ikiwamo Marekani, Umoja wa Afrika, Umoja wa Ulaya na ECOWAS.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres alisema Burkina Faso inahitaji amani, utulivu na umoja katika kupambana na makundi ya kigaidi na mitandao ya uhalifu inayoendesha shughuli zake kwenye maeneo ya nchi hiyo.

*DW*



Kiongozi wa kijeshi aliyejiuzulu baada ya mapinduzi Burkina Faso Luteni Kanali Paul-Henri Sandaogo Damiba. **PICHA DW.**

## NATO: Ukraine inauwezo wa kurudisha maeneo yake

**KYIV, Ukraine**

KATIBU Mkuu wa Muungano wa Kijeshi unaojumuisha Marekani, Uingereza, Ufaransa na Ujerumani (NATO) Jens Stoltenberg amesema vikosi vya kijeshi vya Ukraine vinapiga hatua na vinaweza kukabiliana vilivyo na uvamizi wa Urusi.

Stoltenberg, aliyabainisha hayo jana wakati alipofanyiwa mahojiano na televisheni ya NBC.

"Wiki hii tuliona kwamba waliweza kuchukua jiji jipya, Liman, na hii inaonyesha kwamba Waukraine wanafanya maendeleo, wanaweza kurudisha nyuma askari wa Urusi kwa ujasiri, ushujaa, ujuzi, na bila shaka, shukrani kwa silaha ambazo Marekani na wengine wanatoa washirika," alisema Stoltenberg.

Aliongeza kwa kusisitiza kwamba njia bora ya kukabiliana na vitendo vya Urusi na majaribio yake ya kunyakua maeneo ya Ukraine ni kuendelea kuunga mkono Ukraine.

"Tutaendelea kusambaza zana za kijeshi, kutoa usaidizi wa kisiasa na kiuchumi, hii ndiyo njia bora ya kuisaidia Ukraine kukomboa maeneo yake," alisema Stoltenberg.

Aidha, alieleza kuwa kuidhibiti tena Lyman ni umuhimu wa kimkakati kwa Ukraine. Huku akibainisha kwamba mji huo ulikuwa umetumiwa kama kitovu cha vifaa na Urusi, na ungeweza kuwapa wanajeshi wa Ukraine nafasi ya kuyafikia maeneo zaidi katika mikoa ya Donetsk na Luhansk.

Pia, picha za video zilizochapishwa mtandaoni zilionesha wanajeshi wa Ukraine wakipeperusha bendera yao ya taifa nje kidogo ya mji walioutwaa.

**"Tutaendelea kusambaza zana za kijeshi, kutoa usaidizi wa kisiasa na kiuchumi, hii ndiyo njia bora ya kuisaidia Ukraine...**

# Mwanzilishi mwenza wa Al-Shabab auawa Somalia

**MOGADISHU, Somalia**

SERIKALI ya Somalia imetangaza kuwa mwanzilishi mwenza na mwanamgambo mkuu wa al-Shabab, Abdullahi Nadir, aliuawa Oktoba Mosi katika eneo la kusini la Jubba ya Kati.

Wizara ya habari wa Somalia jana, ilisema kwamba Nadir alikuwa mkuu wa kitengo cha uenezaji wa kidini cha al-Shabab, na kwamba alikuwa akisakwa na mtu ambaye akifanikisha kukamatwa kwake angepewa kiasi cha dola za Marekani milioni tatu.

Iliongeza kuwa, al-Shabab walimchukulia Nadir kama mrithi anayetarajiwa na kiongozi wake wa sasa, Ahmed Omar Diriye, almaarufu Abu Ubaidah, ambaye kwa muda mrefu imekuwa ikisemekana kuwa yuko katika afya mbaya.

Aidha, vyombo vya habari vya kibinafsi viliripoti kwamba Nadir aliuawa katika shambulio la ndege zisizo na rubani.

Wizara ya habari ilisema kuwa, vikosi vya usalama vya Somalia na washirika wa kimataifa walimuua Nadir katika operesheni ya pamoja, lakini haikutaja shambulio la ndege zisizo na rubani.

Vikosi maalumu vya Marekani barani Afrika, ambavyo mara nyingi huwalenga wanamgambo na nyadhifa za juu za al-Shabab, bado havijatoa maoni yoyote kuhusu maendeleo hayo.

Wakati huo huo, Ethiopia imetuma wanajeshi zaidi katika mji wa kusini magharibi mwa Dolow nchini Somalia kupambana na al-Shabab.

Pia, inaelezwa kuwa kutumwa kwa wanajeshi hawo kumekuja baada ya jimbo la eneo la Jubbaland nchini Somalia kutangaza kuwa linajiandaa kwa mashambulizi mapya dhidi ya al-Shabab.

*BBC*

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## TANGAZO NYUMBA INAUZWA

**ALOYCE MAKIRE & FAMILY WANAUZA NYUMBA NO.3 ILIOPO TARIME BUHEMBA MTAA WA WAIRANGA ROAD.**



**MAJ. KYAMBILE (rtd)**
**0715047304**

## KUPOTEA KWA CHETI



**RACHEL EUZEBIO MVANDA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2702-0042** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **NYALUMBU SECONDARY SCHOOL** mwaka **2013.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DSM/PHQ/RB/338063/2022**

---

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA SONGEA ILIYOPO SONGEA**

**RUFAA YA JINAI NA. 12 YA MWAKA 2022**

**CHRISTIAN KAYOMBO..................MWOMBA RUFAA**

**DHIDI YA**

**TAMU KISINZA NDUGULILE...............MJIBU RUFAA**

**WITO WA KUITWA SHAURINI**

**KWA:-**
**TAMU KISINZA NDUGULILE**
**POPOTE ULIPO**

Hii ni kukutaarifu kwamba Rufaa ya jinai tajwa hapo juu imepangwa kusikilizwa tarehe 6 mwezi Octoba mwaka 2022 saa 3.00 asubuhi mbele ya Mh. A.C JEMBE hakimu mkazi wa wilaya ya Songea. Kwa hiyo unapaswa kuhudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako anayeruhusiwa kisheria. Endapo hutahudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako shauri hilo la rufaa litasikilizwa bila wewe kuwepo.

Imetolewa kwa mkono wangu na muhuri wa mahakama hii leo tarehe 22 mwezi 9 mwaka 2022

HAKIMU MKAZI WA WILAYA YA SONGEA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya Njombe**
**Kituo cha Njombe Mjini**
**Mkoa Njombe**
**Usimamizi wa mirathi Na 49/2022**
**AGNUS THOMAS MELLI......................................Marehemu**
**PREDIKANDA AGNUS MELLI...........................Msimamizi**

**TAARIFA KWA WADAI**
**[kanuni ya 9(1) ya nyongeza ya V ya sharia ya mahakimu wa Mahakama Sura ya ii Rejeo la 2019]**

**TAARIFA** inatolewa hapa kwa wote wanaodai kuwa na madai yanayohusiana na mali za marehemu mtajwa hapo juu **AGNUS THOMAS MELLI,** aliyefia Hospitali ya Rufaa Njombe, tarehe **28/03/2022,** na mahakama kunipa barua ya usimamizi wa mirathi hiyo mimi **PREDIKANDA AGNUS MELLI** siku ya tarehe 20 mwezi wa 09 mwaka 2022, hapa sasa wanatakiwa kunipa madai yao kwangu kupitia sanduku langu la barua......Njombe au namba ya simu **0765835606,** au kuniletea kwa binafsi, ndani ya siku 14 kuanzia tarehe ya kutangazwa taarifa hii ambapo muda wake utapoisha nitaendelea kukabidhi mali za marehemu kwa warithi wanaostahili, nikizingatia tu mada ambayo kwao nitakua nmearifiwa.

PREDIKANDA AGNUS MELLI

## KUPOTEA KWA CHETI



**MASANJA JOHN** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0151-0635** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **SHULE YA SEKONDARI YA SENGEREMA mwaka 2014.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: SIM/BAR/RB/ 501645/2019**

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA RUNGWE LILILOKO TUKUYU**

**MAOMBI NA. 07/2016**

**MARIA RAPHAEL......................MDAI**

**DHIDI YA**

**HURUMA JOSEPH (Msimamizi wa mirathi ya marehemu JOSEPH JAMES MWALUKOBA).......................MDAIWA WA 1**
**MOSES K. MAGANGA.....................................MDAIWA WA 2**
**HTT IN FRANCO LIMITED................................MDAIWA WA 3**
**VODACOM TANZANIA LIMITED.......................MDAIWA WA 4**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA: MOSES K. MAGANGA**

Fahamu kwamba, kwa amri ya Mahakama kuu shauri tajwa hapo juu lilirudishwa katika baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Rungwe kwa ajili ya kusikilizwa upya. Shauri hilo limepangwa kutajwa tarehe 26/10/2022 saa mbili na nusu asubuhi. Unaamriwa kufika bila kukosa wewe mwenyewe au wakili wako au mtu yeyote anayeruhusiwa kisheria utakayempa maelezo kamili. Usipofika baraza litatoa amri stahiki ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri upande mmoja na hukumu kutolewa dhidi yako.

AMRI hii imetolewa na mkono wangu na mhuri wa baraza hili tarehe 25/08/2022.

B. J. CYRIL
MWENYEKITI WA BARAZA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MJINI MOROGORO**
**KITUO CHA CHAMWINO**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na......18/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: HAYUPO MWINYIMVUA WA MOROGORO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI YALIYOLETWA NA SHUKURU HAYUPO MWINYIMVUA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 05 Mwezi 10 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Zingatia;
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

**Imetolewa leo tarehe 14 mwezi 10 mwaka 2022**

**HAKIMU MFAWIDHI**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**Wilaya ya Morogoro**

**Mkoa Wa Morogoro**

**MAOMBI MADOGO NAMBA 1011 YA 2021**

**PAPAA SOKOINE..........................MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**VALERIAN FELIX CHUWA(Msimamizi wa mirathi ya marehemu Emmanuel Mleka Bulugu)..............MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA VALERIAN FELIX CHUWA**

Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza za Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro tarehe 06/10/2022 mbele ya mwenyekiti E.Mogasa wewe mwenyewe binafsi au utume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa.Endapo hautahudhuria maombi yatatajwa na kusikilzwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.

Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza leo tarehe 22 Mwezi September 2022.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MJINI MOROGORO**
**KITUO CHA CHAMWINO**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na........18/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: HAYUPO MWINYIMVUA WA MOROGORO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI YALIYOLETWA NA SHUKURU HAYUPO MWINYIMVUA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe **05 Mwezi 10 Mwaka 2022** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

**Imetolewa leo tarehe 14 mwezi 10 mwaka 2022**

**HAKIMU MFAWIDHI**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SAIDI ABDALLAH** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA DYNA** yenye usajili namba **T 773 BNE, CHASSIS NAMBA: BU1020001794 na ENGINE NAMBA: 2L3240391.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: TAT/TAN/RB/378670/2022**


**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0782253676**

**KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

BURUDANI



# DICAPRIO, GIGI NDANI YA MAHABA MAZITO

**PARIS, Ufaransa**

WIKI mbili baada ya kuonekana wakiwa pamoja wakati wa Wiki ya Mitindo ya jijini New York, Leonardo DiCaprio na Gigi Hadid, walipigwa picha wakiwa pamoja kwenye hoteli moja jijini Paris, Ufaransa na tetesi zinadai kwamba wapo kwenye penzi zito.

Licha ya kujaribu kuficha, lakini TMZ.com imethibtisha kwamba, wawili hao, DiCaprio na Gigi wapo kwenye mapenzi.

Mwonekano mpya katika onyesho la mitindo la kule Messika, mwanamitindo Gigi alipigwa picha akirejea hotelini kwake, Royal Monceau mapema mwishoni mwa wiki.

Usiku huo huo, DiCaprio mwigizaji aliyeshinda tuzo ya Oscar ambaye alitengana na mpenzi kwa muda mrefu, Camila Morrone wiki iliyopita, pia alipigwa picha akiondoka kwenye hoteli hiyo hiyo ya kifahari.

Wiki mbili tu mapema, wawili hao walizua uvumi wa mapenzi walipoonekana wakiwa pamoja jijini New York.

Kama gazeti la Daily Mail liliripoti, Gigi mwenye umri wa miaka 27 na Leo mwenye miaka 47, wapo kwenye mapenzi.

Picha ziliwanasa wawili hao wakiwa wameegemeana karibu walipokuwa wakitembea.

Ingawa wawili hao bado hawajathibitisha hadharani hali yao ya uhusiano, chanzo kimoja kiliiambia E! kuwa ni wapenzi.

## KAYUMBA: UWOYA NI MSHIKAJI TU

**Na Mwandishi Wetu**

MSANII wa Bongo Fleva, Kayumba amefunguka juu ya ukaribu wake wa sasa na nyota wa kike wa bongo muvi, Irene Uwoya.

Kayumba, ambaye ni zao la kipindi cha kusaka vipaji cha BSS (Bongo Star Search), amesema kuwa yeye na Uwoya ni washikaji na kuna muda huwa anamsaidia fedha za kushuti video za muziki wake.

Akizungumza katika kipindi kimoja cha redio, Kayumba alisema yeye na Uwoya ni marafiki wazuri sana.

"Mimi na Irene Uwoya ni washikaji yaani marafiki wazuri, hakuna kingine chochote kinachoendelea kati yetu," alisema Kayumba.

Aliongeza: "Hivi sasa Uwoya amebaki kama mshikaji, tunawasiliana pia kuna muda ananisaidia fedha za kushuti video za nyimbo zangu, hakuna chochote zaidi ya ushikaji tu."



## BARNABA AFUNGUKA ALI KIBA KUMTOSA

**Na Mwandishi Wetu**



NYOTA wa muziki wa Bongo Fleva, Barnaba Classic ametolea ufafanuzi kwa nini msani mwenzake, Ali Kiba hakuhudhuria kwenye uzinduzi wa albamu yake.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Barnaba aliulizwa kuhusu ukaribu wake na Kiba na kwa nini hakuhudhuria kwenye uzinduzi wake.

Barnaba alifunga kwa kusema kwamba, alimualika Kiba, lakini nyota huyo alikuwa Mombasa, Kenya.

Aidha, alisema licha ya kushindwa kuhudhuria, pia alimposti kwenye ukurasa wake wa Instagram kumtakia kila la kheri.

"Kiba alikuwa Mombasa na aliweka 'post' moja ambayo aliithamini sana kwani angeweza kuposti vitu vingine, namshukuru kwa hilo."

Aidha, aliongeza kwamba, yeye hajawahi kumuongelea vibaya Kiba kwa sababu ni mmoja wa watu wake wa karibu.

# NMB YAIHAKIKISHIA JWTZ UDHAMINI ZAIDI CDF TROPHY

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imemhakikishia Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Tanzania (CDF), Jenerali Jacob Nkunda, udhamini endelevu wa Mashindano ya Gofu ya Mkuu wa Majeshi (NMB CDF Trophy), ambayo ni sehemu ya maadhimisho ya kuzaliwa kwa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ).

Ahadi hiyo imetolewa na Afisa Mkuu wa Biashara na Wateja Binafsi wa NMB, Filbert Mponzi, wakati wa hafla ya utoaji zawadi kwa washindi wa NMB CDF Trophy 2022, iliyofanyika katika viwanja vya Gofu Lugalo, Dar es Salaam, ambako kwa siku mbili wakali wa mchezo huo wapatao 243 walichuana.

Hafla hiyo ilihudhuriwa pia na Mkuu wa Majeshi Mstaafu Tanzania Jenerali George Waitara na Mwenyekiti wa Klabu ya Gofu Lugalo, Brigedia Jenerali mstaafu Michael Luwongo, pamoja na Mkuu wa Majeshi wa Malawi, Jenerali Vicent Nundwe, aliyeambatana na nyota wa timu za Jeshi la nchi hiyo.

Awali, akiwasilisha salamu za Afisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna na Mwenyekiti wa Bodi, Dk. Edwin Mhede, Mponzi alimpongeza Jenerali Nkunda kwa kuaminiwa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuteuliwa, na kuahidi kumuunga mkono ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

"Kwa kutambua umuhimu wa mchezo wa gofu, pia mahusiano ya NMB na JWTZ, tumeona umuhimu wa kuendelea kudhamini mashindano haya ya Mkuu wa Majeshi na tumefanya hivyo kwa miaka sita sasa. Mwaka huu katika CDF Trophy, NMB imetoa Sh. milioni 60 za kugharamia zawadi na vifaa mbalimbali.

"Nikuahidi CDF Nkunda, NMB tukiwa benki ya kizalendo, benki ambayo serikali ina hisa za kutosha na ukweli kuwa sisi ni wadau wakubwa wa serikali na kwa kutambua umuhimu wa JWTZ, tutaendelea kudhamini CDF Trophy kwa miaka mingi ijayo," alisema na kuongeza:

"Jioni wakati tunakabidhi zawadi za watoto (juniors), kocha alilalamika vijana wake kukosa viatu, nasi NMB tukalichukua hilo, baada ya kuambiwa Sh. milioni tano zinatosha kuwezesha vijana wale kupata viatu na jezi ili kuwachagiza kushiriki kwa ufanisi mchezo huu na kupata mafanikio," alisema.

Mponzi, alitumia nafasi hiyo kumueleza Generali Nkunda kuwa NMB inayo Matawi Maalum kadhaa nchini kwa ajili ya maofisa 'private banking' na kwamba kwa Dar es Salaam, wana matawi ya Oyster Plaza na Makao Makuu, hivyo kuwakaribisha majenerali wa jeshi na maofisa wengine kufika kuhudumiwa.

Kwa upande wa Jenerali Nkunda, alianza kwa kuipongeza na kuishukuru NMB kwa udhamini uliofanikisha mashindano hayo kwa kiwango cha kimataifa, huku akisisitiza kuwa matumaini yake ni benki hiyo kuendelea kuisapoti JWTZ na kuiunga mkono serikali.

"Nimefurahishwa na udhamini wa NMB kwa mwaka wa sita mfululizo sasa, hii inaonyesha na kuthibitisha ni kwa namna gani NMB ilivyo karibu na JWTZ, pia inatumia fursa hiyo kurudisha fadhila kwa jamii.

"Nitoe wito kwa taasisi za serikali na mashirika mengine kuiga mfano wa NMB na wadhamini wengine katika kushirikiana na jeshi kwa kudhamini mashindano haya na pia kusaidia ushiriki wa timu za majeshi katika mashindano ya majeshi ndani na nje ya nchi," alisisitiza.

Aidha, Jenerali Nkunda alimpongeza CDF wa Malawi, Vicent Nundwe, kwa kuacha majukumu yake na kuja kushiriki CDF Trophy 2022 yeye na timu za maofisa wa Jeshi la Malawi, ushiriki ambao umeliongezea shindano hilo hadhi kimataifa.

Katika mashindano hayo yaliyoanza Oktoba 1, Koplo Marius Kajuna aliibuka mshindi wa jumla wa CDF Trophy, yaliyohusisha 'kategori' za 'Combat Competition,' 'Professional,' 'Main Event CDF Trophy,' 'Juniors' na 'Sponsors Competition,' ambako Abdallah Gunda wa NMB aliwagaragaza wadhamini wengine.



Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Jenerali Jacob John Mkunda (wa pili kushoto), akimkabidhi kombe la ushindi wa wadhamini katika mashindano ya Gofu ya Mkuu wa Majeshi, mfanyakazi wa Benki ya NMB, Abdallah Gunda, katika hafla ya kufunga mashindano hayo kwenye viwanja vya gofu vya Lugalo, Dar es Salaam. Kulia ni Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi na kushoto ni Mkuu wa Majeshi wa Malawi, Jenerali Vicent Nundwe. **MPIGAPICHA WETU**

# Mganda kocha mkuu Simba Queens

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Simba umefikia makubaliano na Kocha Charles Lukulu kufundisha kikosi cha timu ya Wanawake, Simba Queens kwa mkataba wa miaka miwili.

Kabla ya kujiunga na kikosi cha Simba Queens, Lukulu alikuwa akikinoa kikosi cha SHE Corporates ambao ni mabingwa wa Ligi Kuu Wanawake nchini Uganda.

Lukula, ana Leseni A ya Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), hivyo inamuwezesha kukiongoza kikosi cha Simba Queens kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika yanayotarajiwa kutimua vumbi nchini Morocco, Novemba mwaka huu.

Pia, Lukula anakumbukwa kwa kukiongoza kikosi cha SHE Corporates kufika fainali ya michuano ya CECAFA iliyofanyika hapa nchini Agosti mwaka huu na Simba Queens kuibuka na ushindi wa bao moja.

Miongoni mwa timu alizowahi kuzifundisha kocha huyo tangu mwaka 2016 ni Nyamityobora FC, Kirinya Jinja S.S.S FC, Uganda Cranes U-23, MUBS FC na SHE Corporates.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Simba Queens, Selemani Erasssy, alisema tayari kocha huyo raia wa Uganda ameshaanza kazi ya kukinoa kikosi cha timu hiyo tangu jana.

Alisema wanaimani na Lukula kulingana na uwezo wake wa kufundisha soka na wanatarajia kupata matokeo mazuri katika timu hiyo chini ya kocha huyo mpya.

"Ni kweli uongozi umemalizana na Lukula na tayari ameanza kazi yake leo (jana) kwa ajili ya kukinoa kikosi cha Simba Queens kuelekea michuano ya kimataifa," alisema meneja wa timu hiyo.

Ujio wa Lukula ni baada ya aliyekuwa kocha wa timu hiyo, Sébastien Nkoma kutokuwa na Lesseni A ambayo inamruhusu kukaa katika benchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

# Wachezaji Kipanga watolewa hofu CAF

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Msaidizi wa Klabu ya Kipanga ya Zanzibar, Hamis Hassan, amewataka wachezaji wake kuondoa wasiwasi na hofu kuelekea mchezo wao wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Club Africain ya Tunisia wakataoucheza Jumamosi wiki hii.

Kipanga ambayo imetinga raundi ya kwanza ya michuano hiyo kwa kuitoa Al Hilal Wau ya Sudan Kusini kwa mikwaju ya penalti 4-3 kutokana na matokeo ya bao 1-1 nyumbani na ugenini itaanzia nyumbani katika mechi hiyo itakayopigwa Uwanja wa Amaan Zanzibar Jumamosi.

Akizungumza na gazeti hili jana kutoka visiwani Zanzibar, kocha huyo alisema baada ya kumaliza mchezo wao wa kirafiki dhidi ya Simba wiki iliyopita, alianza kazi ya kuwajenga kisaikolojia wachezaji wake hao.

"Baada ya kumaliza mchezo wetu na timu ya Simba, nimeanza kuwajenga kisaikolojia wachezaji wangu ikiwamo kuwapa mbinu za kujiamini kwa lengo la kupata matokeo mazuri nyumbani," alisema Hassan.

Kocha huyo alisema anatambua mchezo huo utakuwa mgumu hasa ukizingatia timu yake haina uzoefu wa mashindano hayo.

Kocha huyo alisema wapinzani wao wanatarajiwa kuwasili Zanzibar Alhamisi wiki hii majira ya saa mbili asubuhi.

# Mbuni FC tishio Championship

**Na Adam Fungamwangwo**

KATIKA hali isiyotarajiwa, timu ya Mbuni FC imeonekana kuwa tishio kwenye Ligi ya Championship, baada Jumapili kupata ushindi mkubwa wa mabao 4-0 dhidi ya Pan African, mechi ikichezwa Uwanja wa Uhuru Dar es salaam.

Huo unakuwa ushindi wa tatu mfululizo kwa timu hiyo kwenye ligi hiyo ikionekana kabisa ina dhamira ya kupanda Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Kwenye mechi ya ufunguzi, iliitandika Ndanda FC mabao 3-0, kabla ya kushinda kwa idadi kama hiyo ya mabao dhidi ya Green Warriors mechi zote ikicheza nyumbani, Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha.

Mabao ya washindi kwenye mechi ya juzi yalifungwa na Shaaban Hussein, akifunga mawili, Jonathan Masimba na Abdul Ramadhani kila mmoja akifunga bao moja.

Kwa matokeo hayo, Mbuni FC bado inaendelea kuziburuza timu za Championship, ikiwamo zile maarufu kama Mbeya, Biashara United, Pan African, Ndanda, Pamba, JKT Tanzania, Transit Camp ambazo zilionekana kama ndizo zitatawala ligi hiyo.

## ZISIKUPITE

### MARTIAL AWANIWA LALIGA

SEVILLA na Valencia zina nia ya kumsajili mshambuliaji wa Ufaransa, Anthony Martial mwenye umri wa miaka 26 kutoka Manchester United. ***(Todofichajes)***

### MAKOCHA WATAJWA WOLVES

KOCHA wa zamani wa Olympiacos, Pedro Martins huenda akawa mshindani mkubwa katika kuchukua nafasi ya Bruno Lage kama kocha wa Wolves, huku kocha wa Sevilla, Julen Lopetegui akizingatiwa na Ange Postecoglou wa Celtic. ***(Telegraph)***

### AMORIM NAYE ATAJWA

KOCHA wa Sporting Lisbon, Ruben Amorim pia ni miongoni mwa wanaowania kazi ya Wolves, ingawa itaigharimu klabu hiyo pauni milioni 20 kama fidia. ***(Sun)***

### CHELSEA NA NKUNKU

CHELSEA walitaka kuweka siri habari kuwa Christopher Nkunku tayari amefanyiwa uchunguzi wa matibabu na klabu hiyo kwa kuwa bado hawajakubaliana ada na RB Leipzig kwa ajili ya fowadi huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 24. ***(Fabrizio Romano)***

### TIELEMANS LULU ULAYA

LIVERPOOL itakabiliana na ushindani kutoka kwa Juventus na Real Madrid kuwania saini ya kiungo wa kati wa Ubelgiji, Youri Tielemans mwenye umri wa miaka 25, ambaye mkataba wake na Leicester unamalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Calciomercato)***

### LOCATELLI ANUKIA ARSENAL

ARSENAL wameulizia kuhusu kumsajili Manuael Locatelli katika dirisha la usajili la Januari. ***(Calciomercato)***

### RANDON ATAKIWA UARABUNI

KLABU ya Falme za Kiarabu, Sharjah FC imeonyesha nia ya kutaka kumsajili mshambuliaji wa Everton, Salomon Rondon, ingawa mchezaji huyo wa kimataifa wa Venezuela mwenye umri wa miaka 33, anaonekana huenda akasalia pale Goodison Park. ***(Liverpool Echo)***

### BALOGUN MKATABA WA KUDUMU

KLABU ya Reims inataka kubadilisha mkopo wao wa msimu mzima wa mshambuliaji wa Arsenal, Folarin Balogun mwenye umri wa miaka 21, kuwa uhamisho wa kudumu. ***(Ekrem Konur)***

### VLAHOVIC AWINDWA ARSENAL

ARSENAL wanaweza kukabiliwa na ushindani kutoka kwa Chelsea, Bayern Munich na PSG kwa mshambuliaji wa Juventus, Dusan Vlahovic mwenye umri wamiaka 22. ***(Il Bianconero)***

### UNITED HOI KWA LOCATELLI

MANCHESTER United ilishindwa katika jitihada za kumsajili kiungo wa kati wa Italia, Manuel Locatelli mwenye umri wa miaka 24, kutoka Juventus msimu wa majira ya joto. ***(Sport Mediaset)***

### MOURA AWANIWA SPURS

WINGA wa Tottenham Hotspur Mbrazil Lucas Moura mwenye umri wa miaka 30, atalengwa na Sevilla katika dirisha la uhamisho la Januari. ***(Vamos Mi Sevilla)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# TEN HAG AKUBALI UNITED KUKOSA UBORA KWA CITY

## ●●●Tazama kiwango cha Arsenal, Liverpool, kama hautapigana, basi tuna tatizo dhidi ya...

**MANCHESTER, England**

ERIK ten Hag, amekiri kwamba, timu yake ya Manchester United ilikabiliwa na 'kutokuwa na imani' wakati wa mechi yao ya kichapo dhidi ya wapinzani wao Manchester City, Jumapili.

Kikosi cha kocha huyo wa Uholanzi kilikuwa nyuma kwa mabao 6-1 pale kwenye Uwanja wa Etihad kabla ya Anthony Martial, kufunga mabao mawili ya dakika za lala salama.

Akizungumza na Sky Sports baada ya kipigo hicho, Ten Hag alikiri kuwa kikosi chake hakina imani, alipoulizwa nini kilienda vibaya siku hiyo.

"Kutokuwa na imani. Ninashangaa kwa nini hatukuleta (imani) uwanjani. Nimeona - ni wazi wiki nne zilizopita - timu tofauti, roho tofauti, kujiamini tofauti na leo (juzi) hatukuwa na imani.

"Kuanzia dakika ya kwanza na kuendelea hatukuwa kwenye mchezo, hatukuwa jasiri katika kumiliki mpira.

"Siku zote ni vigumu kujua. Lazima nizungumze na wachezaji wangu na mimi lazima nijue.

"Wanajua wanaweza kufanya vizuri zaidi - tazama kiwango cha Arsenal, tazama kiwango cha Liverpool - lakini ikiwa hautapigana, na hatukupigana, basi tuna tatizo dhidi ya timu kama Man City."

Man United, watatarajia kurejea katika njia ya ushindi Alhamisi jioni watakapomenyana na Omonia kwenye Ligi ya Europa.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,037,3

JACKPOT MECHI WIKI HII
TAREHE: 04 NA 05 OKTOBA 2022
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 04/10/22 | 19:45 | Marseille vs Sporting Lisbon | 2.23 | 3.40 | 3.15 |
| 02. 04/10/22 | 21:45 | Plymouth vs Sheffield Wed | 2.56 | 3.26 | 2.61 |
| 03. 04/10/22 | 21:45 | Hartlepool vs Doncaster | 2.65 | 3.20 | 2.55 |
| 04. 04/10/22 | 21:45 | Walsall vs Northampton | 2.54 | 3.19 | 2.69 |
| 05. 04/10/22 | 22:00 | Porto vs Bayer Leverkusen | 2.20 | 3.49 | 3.14 |
| 06. 04/10/22 | 22:00 | Ajax vs Napoli | 2.20 | 3.69 | 2.99 |
| 07. 04/10/22 | 22:00 | Cardiff vs Blackburn | 2.48 | 3.19 | 2.74 |
| 08. 05/10/22 | 21:45 | Hull City vs Wigan | 2.45 | 3.19 | 2.79 |
| 09. 05/10/22 | 21:45 | Rotherham vs Millwall | 2.41 | 3.19 | 2.85 |
| 10. 05/10/22 | 22:00 | Sevilla FC vs Borussia Dortmund | 2.80 | 3.40 | 2.34 |
| 11. 05/10/22 | 22:00 | Preston vs West Bromwich | 2.86 | 3.21 | 2.39 |
| 12. 05/10/22 | 19:45 | Pyunik Yerevan vs Zalgiris | 2.40 | 3.22 | 2.92 |
| 13. 05/10/22 | 22:00 | Midtjylland vs Feyenoord | 2.89 | 3.64 | 2.23 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ANCELOTTI AKATAA KUMLAUMU BENZEMA




**MADRID, Hispania**

CARLO Ancelotti alikataa kumtupia lawama, Karim Benzema baada ya mshambuliaji huyo kukosa penalti na kuifanya Real Madrid kugawana pointi dhidi ya Osasuna kwenye mchezo wa Ligi Kuu kwa sare ya bao 1-1.

Licha ya kurejea kwa Benzema kutoka kwenye chumba cha majeruhi baada ya kuwa nje ya uwanja kwa wiki tatu, Madrid hawakuwa kwenye kiwango bora Jumapili, na kupoteza bao la kuongoza kipindi cha kwanza wakati Kike Garcia, aliposawazisha lile la Vinicius Junior.

Benzema, alipata nafasi ya kuipa Madrid ushindi wa saba mfululizo wa ligi wakati David Garcia alipotolewa nje kwa kadi nyekundu kwa kumsukuma mshambuliaji huyo umbali wa yadi sita, lakini nyota huyo wa Ufaransa shuti lake iligonga mwamba wa goli.

Osasuna ikiwa na wachezaji 10 uwanjani walipambana sana kuhakikisha wanaondoka angalau na pointi kwenye mchezo huo.

Ancelotti alikataa kumlaumu Benzema kwa matokeo hayo na kusisitiza Madrid haikufanya vibaya, akiiambia DAZN: "Karim huwa anafunga."

"Mechi haikuwa ya kuvutia, lakini baada ya bao tulilofungwa, timu ilicheza kama inavyopaswa kucheza.

"Karim hakuwa na matatizo ya kuanza kucheza dakika 90. Anatakiwa kuwa katika hali nzuri zaidi kwa kucheza.

"Ni ajali ya soka ambayo wakati mwingine inaweza kutokea, tulikuwa na uwiano mzuri."

Kushindwa kwa Madrid kupata bao la ushindi kuna maanisha kubaki nyuma ya Barcelona kwa tofauti ya mabao kwenye msimamo wa Ligi Kuu Hispania.

# Allegri: Juventus lazima ichukue hatua

**TURIN, Italia**

KOCHA wa Juventus, Massimiliano Allegri amesema ni lazima timu yake ichukue "hatua moja baada ya nyingine" kutokana na kumaliza mwezi mmoja bila kushinda na kuibuka na mabao 3-0 dhidi ya Bologna, Jumapili.

Bianconeri hao walishinda 3-0 kwenye Uwanja wa Allianz, na kupata ushindi wao wa kwanza katika mashindano yote tangu mwishoni mwa Agosti shukrani kwa mabao ya Filip Kostic, Dusan Vlahovic na Arkadiusz Milik.

Matokeo hayo yaliifanya Juventus kuporomoka katika msimamo wa ligi hadi katikati, ingawa sasa wamebakia pointi nne kutoka kwa timu nne za juu na saba nyuma ya viongozi wa msimu wa mapema, Napoli.



Ugumu wa changamoto inayowakabili Juve haujapotea kwa Allegri, ambaye amesema timu yake inahitaji kuepuka kupoteza katika wiki zijazo.

"Tunahitaji kuchukua hatua moja kwa wakati, na tunatumaini, tunaweza kuziba pengo," alisema akiiambia DAZN.

"Tuliifunga msimu uliopita, kwa hiyo tunajua tunaweza kufanya hivyo tena.

"Tulihitaji uvumilivu na umakini ili kujenga uchezaji na kupata matokeo. Karibu nilihisi kama hatukuamini tuliporudi kwenye chumba cha kubadilishia nguo.

"Inahitaji kuwa hatua moja ndogo kwa wakati mmoja. Hatuwezi kufanya tofauti hiyo kwa wakati mmoja."

## HABARI MICHEZO

# 361,877/-

# KAPOMBE, BANDA SASA KUIKOSA DE AGOSTO CAF

**Na Hadija Mngwai**

NYOTA wa Simba, Shomari Kapombe na Peter Banda wakaukosa mchezo wa kimataifa wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Primeiro de Agosto ya Angola kutokana na majeraha waliyokuwanayo.

Simba inatarajia kuvaana na Primeiro de Agosto Jumapili wiki hii nchini Angola kabla ya kurudiana Oktoba 16, mwaka huu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Kapombe, alishindwa kusafiri na kikosi hicho kilichokwenda visiwani Zanzibar katika michezo ya kirafiki kabla kuvaana na Dodoma Jiji FC juzi na kuibuka na ushindi wa mabao 3-0.

Kwa upande wa Banda na Jimson Mwanuke, walipata majeraha visiwani Zanzibar wakati wakicheza kwenye mechi za kirafiki.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja Habari na Mawasiriano wa Simba, Ahmed Ally, alisema nyota hao wana hatihati ya kwenda Angola kutokana na majeraha yanayowakabili.

"Kikosi chetu kipo vizuri baada ya mchezo wa jana (juzi) kimepewa mapumziko ya siku moja na kesho (leo), watarudi kambini kuanza maandalizi ya kuelekea Angola.

"Wachezaji Shomari Kapombe ambaye anasumbuliwa na nyama za paja hatakuwa sehemu ya kikosi kitakachokwenda Angola, kwa sasa anaendelea na matibabu na hata akipona leo hatakuwa sawa kutokana na kutofanya mazoezi.

"Wachezaji wengine ambao waliumia timu ilipokuwa Zanzibar ni pamoja na Peter Banda na Jimson Mwanuke, wanaendelea na matibabu hivyo hawatoweza kusafiri na timu," alisema Ahmed.

Aidha, alimalizia kwa kusema kuwa wanafanya taratibu za tiketi na vitu vingine na jana walitarajia kukaa kupanga siku ya kwenda Angola.

## KILIMO MARATHON...




Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Fatma Abubakar Mwasa (kushoto), akikabidhi tuzo na cheti cha ushindi wa 'Chapa Bora ya Kilimo 2022' kwa Meneja wa Biashara wa Kampuni ya Sukari ya Kilombero, Bruno Daniel, katika hafla ya utoaji tuzo kwa washindi kwenye sekta ya kilimo wakati wa kilele cha Maonesho ya Kilimo na Mbio za Kuhamasisha Kilimo (Kilimo Marathon), zilizofanyika hivi karibuni katika Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro. **MPIGAPICHA WETU**

## TFF yavuna mil. 376/- mapro Simba, Yanga

INATOKA UK. 32

mchezaji mmoja wa kigeni.

Ruvu Shooting inayonolewa na mzawa Boniface Mkwasa, ndiyo timu pekee ambayo haijasajili mchezaji hata mmoja wa kigeni msimu huu.

Kuhusu matumizi ya fedha hizo, Ofisa Habari wa TFF, Cliford Ndimbo, ameliambia Nipashe kuwa hutumiwa na shirikisho hilo kwa matumizi mbalimbali ikiwamo kwa shughuli za timu za taifa.

## Mgunda: Akili sasa kwa de Agosto CAF

INATOKA UK. 32

wa Ligi ya Mabingwa, hii itatuongezea morali katika mechi yetu ya ugenini nchini Angola.

"Maandalizi ya mchezo huo tayari yameanza na kitu kizuri hatutakuwa na mchezo wa ligi, tutapata muda wa kufanya marekebisho ya matatizo yaliyojitokeza," alisema Mgunda.

Alisema ushindi huo umetokana na wachezaji wake kufuata maelekezo ambayo aliwapa katika mazoezi.

"Dodoma haijaanza ligi vizuri msimu huu, lakini ni miongoni kwa timu bora, tumewafanyia kazi baada ya kuwaangalia, hivyo tukafanikiwa kupata ushindi huu mkubwa," alisema Mgunda na kuongeza;

"Ushindi huu umeongeza hali ya kujiamini na morali kwa wachezaji wangu kuelekea katika mchezo wa kimataifa ambao ndio unafuata, ninaimani napo huku tutafanya vizuri," alisema Mgunda.

Kocha wa Dodoma Jiji, Masoud Djuma, yeye alisema wachezaji wake walikuwa na uchovu kutokana na muda mchache waliokuwa nao tangu kucheza mechi ya mwisho huku wakisafiri kwa umbali mrefu kuja kucheza na Simba.

"Kipindi cha pili wachezaji wangu walichangamka tofauti na ilivyokuwa mwanzo wa mchezo na hapo tuliwapa ushindani wa kutosha Simba," amesema Djuma aliyewahi kuwa kocha msaidizi wa Wekundu wa Msimbazi hao.

## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 08/10/22 | 17:00 | Millwall vs Middlesbrough | 2.63 | 3.13 | 2.73 |
| 02. 08/10/22 | 17:00 | Swansea vs Sunderland | 2.33 | 3.28 | 3.03 |
| 03. 08/10/22 | 17:00 | Wigan vs Cardiff | 2.35 | 3.18 | 3.08 |
| 04. 08/10/22 | 17:00 | Birmingham vs Bristol City | 2.59 | 3.24 | 2.69 |
| 05. 08/10/22 | 19:30 | Brighton vs Tottenham | 2.90 | 3.35 | 2.37 |
| 06. 08/10/22 | 19:30 | Sevilla FC vs Athletic Bilbao | 2.69 | 3.19 | 2.64 |
| 07. 08/10/22 | 22:30 | Pacos Ferreira vs Vitoria Guimaraes | 3.00 | 3.10 | 2.48 |
| 08. 09/10/22 | 14:00 | Huddersfield vs Hull City | 2.36 | 3.33 | 2.93 |
| 09. 09/10/22 | 15:00 | Valladolid vs Betis | 3.03 | 3.33 | 2.30 |
| 10. 09/10/22 | 16:00 | Salernitana vs Verona | 2.53 | 3.37 | 2.68 |
| 11. 09/10/22 | 16:00 | Udinese vs Atalanta | 2.63 | 3.37 | 2.58 |
| 12. 09/10/22 | 16:00 | Angers vs Strasbourg | 2.44 | 3.33 | 2.78 |
| 13. 09/10/22 | 17:15 | Cadiz CF vs Espanyol | 2.88 | 3.18 | 2.48 |
| 14. 09/10/22 | 18:30 | Arsenal vs Liverpool | 2.64 | 3.45 | 2.53 |
| 15. 09/10/22 | 18:30 | Hertha BSC vs SC Freiburg | 3.02 | 3.41 | 2.25 |
| 16. 09/10/22 | 19:30 | Real Sociedad vs Villarreal | 2.53 | 3.23 | 2.78 |
| 17. 09/10/22 | 20:30 | Stuttgart vs Union Berlin | 2.61 | 3.15 | 2.71 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMANNE - 04/10/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 1558 | Polisi Tanzania vs Geita Gold FC | 2.85 | 2.65 | 2.90 |
| 14:30 | 2717 | Guangzhou RF vs Shenzhen | 3.24 | 3.34 | 2.03 |
| 16:00 | 1531 | Kedah vs Johor Darul Takzim | 7.64 | 5.10 | 1.29 |
| 16:00 | 5433 | Alia Club vs DAR AL Dawa | 3.09 | 3.14 | 2.19 |
| 17:00 | 3628 | US Tataouine vs Club A Bizertin | 2.43 | 2.64 | 3.23 |
| 17:00 | 4105 | Dinamo Bucuresti vs Unirea Slobozia | 2.65 | 3.04 | 2.55 |
| 17:00 | 4423 | US Monastir vs Africain | 2.25 | 2.64 | 3.62 |
| 18:00 | 5270 | Sekhukhune United vs Orlando Pirates | 3.40 | 2.75 | 2.37 |
| 19:45 | 2513 | Marseille vs Sporting Lisbon | 2.18 | 3.35 | 3.10 |
| 19:45 | 2963 | Bayern Munchen vs Viktoria Plzen | 1.04 | 11.98 | 29.95 |
| 20:00 | 4449 | Osters IF vs Brommapojkarna | 2.23 | 3.46 | 3.10 |
| 20:15 | 3752 | AL Akhdood vs Alshoulla | 2.21 | 3.10 | 3.30 |
| 20:30 | 3643 | Golden Arrows vs Cape Town City | 2.85 | 2.85 | 2.65 |
| 20:30 | 3982 | TS Galaxy FC vs Marumo Gallants FC | 2.29 | 2.66 | 3.76 |
| 20:30 | 4685 | Baalama vs Kfarsoum | 2.24 | 3.19 | 2.94 |
| 20:30 | 5372 | SuperSport Utd vs Bloemfontein Celtic | 2.24 | 2.94 | 3.39 |
| 20:30 | 5961 | Stellenbosch vs Maritzburg Utd | 2.41 | 2.85 | 3.20 |
| 21:00 | 2936 | Mansfield vs Derby | 2.43 | 3.23 | 2.64 |
| 21:45 | 1706 | Guingamp vs Rodez Aveyron | 1.77 | 3.45 | 4.50 |
| 21:45 | 2154 | Stevenage vs Sutton United | 1.88 | 3.40 | 3.95 |
| 21:45 | 2169 | Plymouth vs Sheffield Wed | 2.70 | 3.30 | 2.46 |
| 21:45 | 2204 | Cheltenham vs Bolton | 3.41 | 3.36 | 2.05 |
| 21:45 | 2415 | Montrose vs Airdrieonians | 2.42 | 3.34 | 2.69 |
| 21:45 | 3124 | Luton Town vs Huddersfield | 1.77 | 3.44 | 4.49 |
| 21:45 | 3287 | Bristol City vs Coventry | 2.18 | 3.35 | 3.10 |
| 21:45 | 3300 | Gateshead vs Altrincham | 2.06 | 3.44 | 3.24 |
| 21:45 | 3564 | Burton vs Fleetwood Town | 2.05 | 3.45 | 3.30 |
| 21:45 | 3881 | Southend vs Woking | 2.34 | 3.23 | 2.88 |
| 21:45 | 4085 | Hartlepool vs Doncaster | 2.65 | 3.20 | 2.55 |
| 21:45 | 4208 | Queens Park vs Morton | 2.05 | 3.43 | 3.28 |
| 21:45 | 4292 | Ross County vs Motherwell | 2.66 | 3.11 | 2.66 |
| 21:45 | 4641 | Colchester vs Charlton | 2.86 | 3.35 | 2.22 |
| 21:45 | 4687 | Notts County vs Wrexham | 2.58 | 3.38 | 2.49 |
| 21:45 | 4868 | Walsall vs Northampton | 2.44 | 3.14 | 2.84 |
| 21:45 | 5266 | Cove Rangers vs Dundee FC | 3.40 | 3.45 | 2.00 |
| 21:45 | 5276 | Ipswich vs Cambridge Utd | 1.36 | 4.51 | 8.02 |
| 21:45 | 5342 | Swindon Town vs Newport | 2.26 | 3.24 | 3.04 |
| 21:45 | 5723 | Sheffield Utd vs QPR | 1.71 | 3.60 | 4.60 |
| 21:45 | 5798 | Sunderland vs Blackpool | 1.94 | 3.40 | 3.70 |
| 22:00 | 1019 | Reading vs Norwich City | 3.60 | 3.40 | 1.97 |
| 22:00 | 1232 | Porto vs Bayer Leverkusen | 2.13 | 3.49 | 3.09 |
| 22:00 | 1526 | Ajax vs Napoli | 2.19 | 3.66 | 2.86 |
| 22:00 | 2187 | Liverpool vs Rangers | 1.14 | 7.57 | 14.94 |
| 22:00 | 2505 | Brugge vs Atletico Madrid | 3.55 | 3.30 | 2.02 |
| 22:00 | 3279 | Cardiff vs Blackburn | 2.45 | 3.19 | 2.79 |
| 22:00 | 5123 | Eintracht Frankfurt vs Tottenham | 3.35 | 3.45 | 2.03 |
| 22:00 | 5590 | Inter vs Barcelona | 3.80 | 3.60 | 1.86 |
| 22:30 | 3282 | Godoy Cruz vs San Lorenzo | 2.17 | 3.10 | 3.15 |
| 22:30 | 5549 | NewellS Old Boys vs Arsenal Sarandi | 2.21 | 3.04 | 3.13 |
| 23:15 | 1917 | Deportivo Municipal vs UTC Cajamarca | 2.35 | 3.29 | 2.70 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumanne Oktoba 4, 2022
Nipashe



UKURASA 30

## Ancelotti akataa kumlaumu Benzema

PHIRI MABAO...



Mshambuliaji wa Simba, Moses Phiri (kulia), akimpongeza straika mwenzake, Habib Kyombo baada ya kufunga bao la tatu wakati wakishinda 3-0 dhidi ya Dodoma Jiji FC kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi. Katika mchezo huo Phiri alifunga bao la pili huku la kwanza beki Abdallah Haji Shaibu 'Ninja' akijifunga. **MPIGAPICHA WETU**

# MGUNDA: AKILI SASA KWA DE AGOSTO CAF

●●●Azidi kuandika rekodi ya ushindi Simba, kuwakosa Kapombe, Banda Angola, lakini...

**Na Saada Akida**

BAADA ya ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Dodoma Jiji FC kwenye Ligi Kuu Bara juzi, Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, amesema sasa kazi kubwa iliyopo mbele yake ni kukiandaa kikosi chake kuelekea mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Primeiro de Agosto ya Angola ili kwenda kusaka matokeo chanya.

Mgunda juzi aliendelea kuiongoza vema timu hiyo kupata matokeo chanya tangu akaimu nafasi hiyo kutoka kwa Mserbia Zoran Maki aliyeachana na klabu hiyo hivi karibuni, huo ukiwa ni ushindi wa nne kwenye mechi za kimashindano na wa sita ukichanganya zile za kirafiki.

Alianza kuipa ushindi Simba kwa mabao 2-0 ugenini kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Nyasa Big Bullets ya Malawi Septemba 10, mwaka huu kabla ya siku nne baadaye kurejea Ligi Kuu Bara na kuiongoza kuichapa bao 1-0 ugenini Tanzania Prisons.

Septemba 18, akaiongoza tena miamba hiyo kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Nyasa Big Bullets katika mchezo wa marudiano Uwanja wa Benjamin Mkapa na kisha kwenda Zanzibar kwa mechi mbili za kirafiki dhidi ya Malindi SC na Kipanga FC akishinda kwa 1-0 na 3-0.

Mchezo wa juzi dhidi ya Dodoma Jiji ambao alishinda 3-0, ni wa sita kwake, shukrani zikiwaendea Moses Phiri na Habib Kyombo walioifungia pamoja na bao la kujifunga la beki Abdallah Haji Shaibu 'Ninja'.

Simba ambayo inatarajia kuondoka nchini Jumamosi kwa ndege ya kukodi kuelekea nchini Angola kwa ajili ya mchezo huo wa hatua ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika, itashuka katika Uwanja wa Estadio de Novembro Jumapili wiki hii majira ya saa 12 jioni kwa saa za Afrika Mashariki.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mgunda alisema maandalizi dhidi ya de Agosto yameanza mara moja kabla ya kikosi kupaa kuelekea Angola.

Alisema mapungufu yaliyoonekana kwenye mchezo wa juzi yatafanyiwa kazi mazoezini kabla ya kukutana na de Agosto mwishoni mwa juma hili.

"Tunamshukuru Mungu tumepata ushindi mnono kabla ya mchezo wetu

INAENDELEA UK. 31

## TFF yavuna mil. 376/- mapro Simba, Yanga

**Na Hadija Mngwai**

ONGEZEKO kubwa la wachezaji wakigeni ('mapro') waliosajiliwa na klabu husussan za Ligi Kuu Tanzania Bara, limeliingizia Shirikisho la Soka nchini (TFF), jumla ya Sh. milioni 376 zilizotokana na malipo ya kuombewa leseni za kucheza na klabu zao, imefahamika.

Kwa mujibu wa kanuni za TFF, ili mchezaji wa kigeni aweze kupata kibali cha kucheza soka nchini, klabu iliyomsajili inalazimika kumlipia ada kiasi cha Sh. milioni nne kwa kila mchezaji kabla ya kuanza kumtumia.

Pia kwa mujibu wa kanuni, klabu moja inaruhusiwa kusajili wachezaji wakigeni wasiozidi 12 na kwa msimu huu ni Simba, Yanga, Azam FC na Singida Big Stars pekee ambazo zimefikisha idadi hiyo, huku klabu zingine zikisajili chini ya hapo.

Kwa klabu zote 16 zinazoshiriki Ligi Kuu msimu huu, wamesajiliwa jumla ya nyota wa kigeni 94, hivyo kwa kila mmoja kulipiwa Sh. milioni nne, zinaifanya TFF kuvuna kiasi cha Sh. milioni 376.

Mbali na Simba, Yanga, Azam FC na Singida Big Stars ambazo kila moja imesajili mapro 12, klabu nyingine inayofuata kwa kusajili nyota wengi wa kigeni ni Coastal Union yenye wageni nane ikifuatiwa na Namungo FC iliyosajili sita, Ihefu (5), Kagera Sugar (5) huku Mtibwa Sugar, Polisi Tanzania, KMC na Dodoma Jiji FC kila moja ikisajili wageni wanne.

Geita Gold yenyewe imesajili mapro watatu, Mbeya City wawili, huku Tanzania Prisons kwa mara ya kwanza tangu kuanzishwa kwake, nayo ikisajili

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >